Mungu Akijificha Kwa Urahisi, Halafu Akijifunua Kwa Jinsi Hiyo

Asante, Ndugu Neville. Bwana na akubariki. Habari za asubuhi, marafiki. Kwa kweli ninauhesabu huu mmoja wa nyakati kuu sana za maisha yangu, kuwapo katika maskani hii tena asubuhi ya leo, kuona mpangilio wake unaopendeza, na uzuri wa watoto wa Mungu wakiwa wameketi katika nyumba Yake leo.

2 Nilishangaa sana nilipofika hapa jana na kuona sura ya jengo hili. Sijawazia kamwe kwamba lingekuwa namna hii. Nilipoona ramani zake, vile wakati walipokwisha kuzichora zile ramani, niliona tu chumba kingine kidogo kimekaa upande, lakini sasa ninapaona kuwa ni mahali pa—pazuri. Nasi tunamshukuru Mwenyezi kwa ajili ya mahali hapa pazuri. Nasi tunaninii . . .

3 Ninawaleteeni asubuhi ya leo, salamu kutoka kwa mke wangu na watoto wangu, ambao wanatamani kuwapo hapa wakati huu kwa ajili ya ibada hii ya kuweka wakfu, na juma hili la kujiweka wakfu kwa Kristo. Lakini watoto wako shuleni, na ni vigumu kuondoka. Nao karibu wamechoka kabisa kwa shauku yao ya kutaka kuwa nyumbani wakiikumbuka nyumba, lakini hatutachoka hata kidogo kuwaonea shauku ninyi watu. Huko hakuishi. Kuna kitu kama kuwa na marafiki. Nami na—nawapenda marafiki, kila mahali, lakini kuna jambo fulani kuhusu marafiki wa zamani. Haidhuru ni wapi utapata marafiki wapya, bado sio wale wa zamani.

4 Haidhuru ningezunguka wapi, mahali hapa daima patakuwa ni pa heshima sana. Kwa kuwa, kama miaka thelathini iliyopita, chini kwenye kile kidimbwi chenye matope, niliweka wakfu sehemu hii ya ardhi kwa Yesu Kristo wakati haikuwa cho chote ila lu—lundo la matope. Hapa pote palikuwa ni kidimbwi. Hiyo ndiyo sababu barabara haikupitia hapo, ba—barabara ilibidi izunguke, kusudi ikwepe hicho kidimbwi kilichokuwa hapa ndani. Na ndani hapa, palikuwa na mayungiyungi, mayungiyungi ya kidimbwi yaliota.

5 Na yu—yungiyungi ni ua la ajabu sana. Ingawa huzaliwa kwenye matope, halina budi kupenyeza njia yake kupitia kwenye matope, na halafu kupitia kwenye maji na matope yanayoteleza, ili lipate kutokeza juu, kuonyesha uzuri wake.

6 Nami na—nafikiri, asubuhi hii, ya kwamba hivyo ndivyo karibuni hasa ilivyotukia hapa. Ya kwamba, tangu wakati huo, yungiyungi dogo la kidimbwi limejipenyeza; na wakati lilipotokeza juu ya maji, lilitandaza mbawa zake, petali zake ndogo zikatokeza, na likaakisi Ua la Uwandani. Naomba lidumu kwa muda mrefu! Na iwe nyumba iliyowekwa wakfu kabisa kwa Mungu!

7 Maskani yenyewe ilikwisha wekwa wakfu katika mwaka wa 1933. Lakini nikiwa ninawazia, asubuhi hii, lingekuwa ni jambo zu—zuri sana kufanya tu ibada ndo—ndogo ya kuwekwa wakfu tena, na hasa kwa watu ambao, kwa upendo wao na kujitolea kwao kwa Kristo, wamefanya jambo hili lote liwezekane. Nami nataka kumshukuru kila mmoja wenu kwa ajili ya matoleo yenu, na kadhalika, ambayo mmetoa kwa ajili ya kuliweka wakfu kanisa hili kwa Kristo.

8 Nami ninafurahi sana, na ninalishukuru kusanyiko, kusema maneno haya kwa niaba ya ndugu zetu wazuri hapa wa kanisa hili, ambao wamejitolea huduma zao kwa ajili ya jambo hili. Ndugu Banks Wood, ndugu yetu mzuri sana; Ndugu Roy Roberson, ndugu yetu mzuri sana; na wengine wengi ambao, kwa unyofu na kwa weupe wa moyo, wamejitolea miezi mingi katika kupajenga mahali hapa jinsi ambavyo pamekuwa, wakakaa hapa kuona ya kwamba palijengwa vile hasa inavyotakiwa.

9 Nami nilipoingia ndani, kuona mimbara hii, ya aina ile ambayo daima nimetamani, maishani mwangu mwote! Mimi . . . Ndugu Woods alijua kile nilichopenda. Hakusema hata kidogo angeijenga, lakini ameijenga.

10 Nami naliangalia jengo hili na jinsi lilivyojengwa, ni ninii tu, loo, ni zuri mno. Na sasa sina maneno ya kuelezea ninavyojisikia. Hakuna tu njia ya kujieleza, mnaona. Na, lakini, Mungu anafahamu. Nami naomba kila mmoja wenu apate thawabu kwa ajili ya michango yenu na yote yale mliyoyafanya kupafanya mahali hapa jinsi vile palivyo, katika namna ya jengo, nyumba ya Bwana. Na sasa ni—ningetaka kusema maneno haya. Sasa, jengo hili, likiwa zuri kama lilivyo, ndani na nje . . .

11 Shemeji yangu, Junior Weber, alishughulikia kujenga matofali. Sioni jinsi lingeweza kuwa kitu kizuri zaidi ya vile lilivyo sasa, kazi iliyo kamili.

12 Ndugu mwingine aliyeko hapa, sijawahi kukutana na mtu huyo hata kidogo, ndiye aliyeweka mitambo ya mawasiliano. Lakini ukiangalia hata kwenye jengo lenye kulala usawa kama hili, ninaweza tu . . . Hakuna mwangwi wa sauti. Hizo ziko kwenye dari hapa, njia mbalimbali. Haidhuru nisimame wapi, ni mamoja tu, unaona. Na kila chumba ki—kimejengwa, hivi kwamba ndani mna maspika, na unaweza kufanya namna yo yote unavyotaka kusikia. Ni ninii, ninaamini ni mkono wa Mwenyezi Mungu uliofanya mambo haya. Sasa kama . . .

13 Hivyo Bwana wetu ametupa basi jengo tunamoweza kumwabudia, kwa zaidi ya, karibu miaka thelathini. Tulianza na sakafu ya udongo, ungambao, na tukaketi hapa karibu na yale majiko ya zamani ya makaa. Naye kondrakta, Ndugu Woods, mmoja wao, na Ndugu Roberson, alikuwa akiniambia ya kwamba mahali pale zile nguzo zilipokuwa, na yale majiko ya kale yalipokuwa yakikaa kwenye zile pao zilizokingama, hizo zilishika moto na kuungua kabisa, labda futi mbili ama tatu. Sababu ya kutoteketea kabisa, ni Mungu tu aliyezihifadhi. Na halafu baada ya kuungua, na uzito wote wa maskani ukiegemea juu ya hizo, kilichoizuia kuporomoka, ni mkono tu wa Mungu. Sasa zimeimarishwa kwa mihimili ya chuma cha pua na ni imara sana zikisimama kwenye ardhi, zimejengwa imara.

14 Sasa nafikiri ni wajibu wetu kupafanya ndani pawe pazuri, kwa neema ya Mungu, kuwa na shukrani sana kwa Mungu ya kwamba ninii yetu. . .Hili halitakuwa tu ni jengo zuri tutakamohudhuria, lakini kila mtu anayeingia ndani na aone tabia nzuri ya Yesu Kristo ndani kila mtu anayeingia ndani. Na pawe mahali palipowekwa wakfu kwa Bwana wetu, watu waliowekwa wakfu. Kwani, hata jengo hili liwe ni zuri namna gani, hilo hakika twalifurahia, uzuri wa kanisa ni tabia ya watu wake. Ninatumaini daima litakuwa ni nyumba ya Mungu, ya uzuri.

15 Sasa, katika ile ibada ya kuwekwa wakfu kwa lile jiwe la kwanza la pembeni lilipokuwa likiwekwa, ono kuu lilikuja. Nalo limeandikwa kwenye hilo jiwe la pembeni, asubuhi ile nilipoiweka wakfu.

16 Nanyi huenda mlishangaa, dakika chache zilizopita, ni kwa nini nilichelewa sana kutoka. Wajibu wangu wa kwanza, nilipokuwa ninakuja kwenye kanisa hili jipya, niliwaunganisha katika ndoa kijana mwanamume na mwanamke wakiwa wamesimama ofisini. Na iwe ni mfano, ya kwamba nitakuwa mhudumu mwaminifu kwa Kristo, kumtayarishia Bibi-arusi kwa ajili ya sherehe ya Siku hiyo.

17 Na sasa hebu na tufanye kama tulivyofanya pale mwanzo. Tulipoanza kwenye kule kuwekwa wakfu kwa kwanza kwa kanisa, nilikuwa mimi ni kijana tu mwanamume na, jamani, labda umri wa miaka ishirini na moja, miaka ishirini na miwili wakati tulipoweka jiwe la pembeni. Ilikuwa ni kabla hata sijaoa. Nami daima nilitaka kuona mahali palipo katika utaratibu halisi, katika ninii ya Mungu. . . Mungu apate kuabudu, unaona, pamoja na watu Wake. Nasi tunaweza tu kufanya jambo hilo, si kwa jengo zuri, bali kwa maisha yaliyowekwa wakfu ndiyo njia tu tunayoweza kulifanya jambo hilo.

18 Na sasa, kabla ya kuweka wakfu, maombi ya kuweka wakfu, na tusome Maandiko machache, kisha tuliweke kanisa wakfu kwa Mungu. Na halafu nina baadhi. . .Nina ujumbe juu ya

uinjilisti, asubuhi ya leo, kuweka utangulizi kwenye Ujumbe wangu unaokuja.

19 Na, usiku wa leo, ninataka kuchukua sura ya 5 ya Ufunuo, ambayo inaunganika pamoja, kutoka kwenye—kutoka katika zile nyakati saba za kanisa, kuingia katika ile Mihuri Saba. Ambayo nitaninii . . . Ndipo tutakuwa na ninii . . .

20 Jumatatu usiku itakuwa ni yule mpanda farasi mweupe. Jumanne usiku . . . Mpanda farasi mweusi, na kuendelea, wale wapanda farasi wanne. Na halafu Mhuri wa Sita ukifunuliwa.

21 Na halafu Jumapili asubuhi, Jumapili ijayo asubuhi, Bwana akipenda . . . Tutaona baadaye, tutalitangaza baadaye. Labda, Jumapili ijayo asubuhi, tutakuwa na mkutano wa maombi kwa ajili ya wagonjwa hapa kwenye jengo hili.

22 Na halafu Jumapili usiku, tumalizie na . . . Bwana na atusaidie kuufungua ule Mhuri wa Saba, ambapo pana aya fupi tu. Nao unasema hivi, "Kulikuwa na kimya Mbinguni kwa muda wa nusu saa," kwa kimya hicho.

23 Sasa, mimi sijui Mihuri hii inachomaanisha. Sijui kabisa, habari zake, kama vile labda wengine wenu wasivyojua habari zake asubuhi ya leo. Tuna mawazo ya kidini ambayo yametolewa na wanadamu, lakini hayo hayataugusa Huo hata kidogo. Na kama mtaona, Huo hauna budi kuja kwa uvuvio. Haina budi kuwa ni Mungu, Mwenyewe, Ndiye pekee anayeweza kufanya jambo hilo, huyo Mwana-Kondoo.

Na usiku wa leo ni kile Kitabu cha Ukombozi.

24 Sasa, katika jambo hili, sababu ya mimi kutotangaza mikutano ya maombi kwa ajili ya wagonjwa, ama cho chote kile, ni kwa sababu ya kwamba mimi nina ninii . . . Ninakaa na baadhi ya marafiki, nami ninatoa kila dakika ya wakati wangu katika kusoma na kuomba. Nanyi mnajua ono lile nililokuwa nalo kabla tu ya kuondoka na kuelekea magharibi, la wale Malaika saba waliokuwa wakija wanaruka. Basi, mtafahamu baadaye kidogo.

25 Kwa hiyo sasa, sasa, ndani ya jengo hili, ninafikiria ya kwamba inatupasa kuwa na ninii, katika jambo hili, kama limewekwa wakfu, ama litaenda kuwekwa wakfu, mnamo dakika chache, kwa ajili ya kumwabudu Mungu, inatupasa kulidumisha jinsi hiyo. Haitupasi kamwe kununua ama kuuza ndani ya jengo hili. Haitupasi kamwe kufanya biashara yo yote katika jengo hili hapa la kukutania. Hayo yasifanyike kamwe hapa ndani, yaani, mambo kama kuwaruhusu wahudumu waje waingie na kuuza vitabu na kila kitu. Hata iwe ni nini, kuna sehemu zingine za kufanyia mambo hayo. Kwa maana, ha—hatupaswi kununua wala kuuza katika nyumba ya Bwana wetu. Panapaswa kuwa ni mahali pa—pa kuabudia; patakatifu, palipowekwa wakfu kwa kusudi hilo. Mnaona? Sasa, Yeye ametupa mahali pazuri. Hebu na tupaweke wakfu kwa ajili

Yake, pia tujiweke wakfu sisi wenyewe, pamoja na mahali hapa, Kwake.

26 Na sasa jambo hili linaweza kidogo kuonekana kama ni kali, lakini, si mahali pa kutembelea. Ni mahali pa kuabudia. Haitupasi hata kidogo kunong'onezana hata neno moja ndani hapa, nje ya kuabudu, mmoja kwa mwingine, labda iwe ni jambo muhimu kabisa kabisa. Mnaona? Hatupaswi kamwe kufanyia shughuli zo zote hapa. Hatupaswi kukimbia ndani ya jengo hili, ama kuwaacha watoto wetu wakimbie humu jengoni. Na kwa hiyo tukifanya hivi, tulipojisikia si muda mrefu uliopita, kwamba tufanye jambo hili, tulipajenga kusudi tuweze kushughulikia mambo yote. Sasa, tuna jambo hili limewekwa hapa. Bila shaka, watu wengi ni wageni. Watu wa maskani hii wanajua jambo hili, ya kwamba jengo hili litawekwa wakfu kwa ajili ya kumtumikia Mwenyezi. Kwa hiyo, tunapojiweka wakfu sisi wenyewe, hebu na tukumbuke, tunapoingia kwenye madhabahu ile, tunyamaze, sisi kwa sisi, na kumwabudu Mungu.

27 Kama tunataka kutembeleana, kuna mahali tunapoweza kufanya hivyo. Lakini, kamwe, kusiwe na kutembea-tembea, ambapo mtu huwezi kujisikia unawaza, na mtu anaingia ndani na hajui la kufanya, unaona, ni kelele nyingi sana na kadhalika. Ni jambo la kibinadamu tu, nami nimeliona makanisani hata limenifanya kujisikia vibaya sana. Kwa sababu, hatuji kwenye madhabahu ya Bwana kukutana sisi kwa sisi. Tunakuja hapa ili tumwabudu Mungu, kisha tunaenda majumbani kwetu. Madhabahu hii imewekwa wakfu kwa ajili ya ibada. Wakati . . . Simameni huko nje, zungumzeni yote mtakayo, mradi tu ni mambo mazuri na matakatifu. Tembeleaneni manyumbani. Tembeleaneni ninyi kwa ninyi kwenye sehemu mbali mbali. Lakini mnapoingia kwenye mlango ule, nyamazeni.

28 Unakuja hapa kuzungumza Naye, unaona, nawe mwache Yeye akujibu. Shida yenyewe ni kwamba, tunazungumza mno kupita kiasi, na hatusikilizi vya kutosha. Halafu, tunapoingia humu, na tumngojee.

29 Sasa, katika ile maskani ya zamani, huenda kusiwe na hata mtu mmoja aliyepo asubuhi ya leo ambaye alikuwako katika ile siku ya kuweka wakfu, wakati Jemadari Ulrich alipopiga muziki. Nami nilisimama nyuma ya misalaba mitatu hapa, kupaweka mahali hapa wakfu. Singemruhusu mtu ye yote . . . Mabawabu walisimama mlangoni, kuona ya kwamba hakuna mtu anayezungumza. Wakati, ulipokwisha kuzungumza huko nje. Uliingia ndani. Kama ungetaka, kimya kimya, ungekuja madhabahuni na kuomba kimya kimya. Ungerudi kwenye kiti chako, ukafungua Biblia. Alilofanya jirani yako, hilo lilikuwa ni shauri lake. Hukuwa na jambo la kusema. Ukitaka kuzungumza naye, unasema, "Nitaonana naye huko nje. Niko hapa ndani

kumwabudu Bwana." Ulisoma Neno Lake, ama ukaketi kwa utulivu.

30 Halafu, basi, muziki. Dada Gertie, sijui kama yuko hapa asubuhi ya leo, ama hayuko, Dada Gibbs. Lile piano la zamani, ninaamini, anaketi nyuma hapa pembeni, sana sana ninavyoweza kukumbuka. Naye angepiga kwa utulivu, "Pale msalabani alipokufa Mwokozi wangu," muziki fulani mzuri, mwororo sana, na—na, halafu, mpaka wakati wa ibada ulipowadia. Naye kiongozi wa nyimbo akasimama na kuongoza nyimbo chache za kusanyiko lote. Halafu kama walikuwa na nyimbo nzuri sana za kuimba mtu mmoja-mmoja, waliziimba. Lakini, kwa hali yo yote isiwe ni kupigapiga makelele tu. Halafu basi muziki uliendelea kupigwa. Nami nilipousikia, nilijua ilikuwa ni wakati wangu wa kutoka umewadia.

31 Wakati mhudumu anapoingia katika kusanyiko la watu wanaoomba, na ule upako wa Roho, hamna budi kusikia kutoka Mbinguni. Ni hayo tu. Hakuna njia ya kuzuia jambo hilo. Lakini kama ukiingia penye mchafuko, ndipo una—unaninii . . . ume—umechanganyikiwa sana, na Roho amehuzunishwa; nasi hatutaki jambo hilo, la. Tunataka kuja hapa kuabudu. Tuna nyumba nzuri sana, jambo ambalo nitalizungumzia, hivi punde, na kadhalika; huko majumbani, ambako tunawatembelea marafiki zetu na kuwapeleka huko. Hii ni nyumba ya Bwana.

32 Sasa, kuna watoto wadogo, sasa, watoto wachanga. Lakini, wao hawana wanachojua. Wao, njia pekee wanayoweza kupata wanachokitaka, ni kukililia. Na wakati mwingine ni maji ya kunywa, na wakati mwingine wanataka kushughulikiwa. Na kwa hiyo, kwa neema ya Mungu, tumeweka chumba kimoja wakfu. Kiliitwa, kwenye ile orodha, "chumba cha kulialia," lakini kiko moja kwa moja mbele yangu. Ni, kwa maneno mengine, mahali ambapo akina mama wanaweza kuwapeleka watoto wao.

33 Sasa, hata kidogo haisumbui, labda, mimi hapa mimbarani. Labda hata sitakuwa na habari juu ya jambo hilo, kwa kuwa nina upako. Lakini kuna watu wengine wanaoketi karibu, na linawasumbua, unaona, nao wanakuja hapa kusikiliza ibada. Kwa hiyo akina mama ni . . . Watoto wenu wachanga wanaanza kulialia; hamwezi kuzuia jambo hilo. Mbona, hakika, ni ninii . . . Unapaswa, unapaswa kumleta. Mama halisi anapenda kumpeleka mtoto wake mchanga kanisani, na hivyo ndivyo ungepaswa kufanya.

34 Nasi tuna chumba kule ambapo unaweza kuona kila kona ya jengo, chumba kizima cha mkutano; na spika iko kule, ambapo unaweza kurekebisha ukubwa wa sauti vyo vyote vile utakayo; pamoja—pamoja na msalani mdogo kule mwisho, na bakuli la maji, na kila kitu kwa manufaa halisi ya mama. Pamoja na viti na vitu vinginevyo, unaweza kuketi; mahali pa kumbadilishia

mtoto wako mchanga, kama atahitaji kubadilishiwa, na kila kitu kipo hapo. Kila kitu kimeandaliwa.

35 Na halafu, mara nyingi, watoto matineja na wakati mwingine watu wazima, wataninii . . . Mwajua, vijana watapitishiana vijikaratasi, ama kumuudhi mtu, ama kitu fulani, kanisani. Sasa, ninyi ni watu wazima vya kutosha kujua jambo lililo jema. Mnaona? Unapaswa kujua jambo lililo jema. Unaona? Hupaswi kuja hapa . . . Kama unatarajia kuwa mtu wa maana kweli kweli siku moja, na ukalee jamaa fulani kwa ajili ya Ufalme wa Mungu, basi anza tangu mwanzo, unaona, na— na utende mambo yanayofaa na kufanya mambo yanayofaa, na sasa, hiyo ni kweli.

36 Sasa, mabawabu wanasimama pembeni mwa majengo, na kadhalika. Na kama kuna upuzi wo wote, wao—wao wamechaguliwa, kama wajibu wao, na wadhamini wanaketi hapa mbele, ili kwamba kama mtu fulani anaanza kukosa adabu, wameagizwa kumwambia mtu huyo anyamaze.

37 Halafu, kama hawastahili heshima hiyo, ni afadhali kwamba mtu mwingine angekalia kiti hicho, kwa maana kuna mtu anayetaka kusikia. Kuna mtu fulani aliyekuja kwa kusudi hilo, kusikiliza. Na hilo ndilo lililotuleta hapa, ni kusikia Neno la Bwana. Na kwa hiyo kila mtu anataka kulisikia, na anawataka wawe kimya iwezekanavyo. Kimya tu kama wawezavyo kuwa; hiyo ni kusema, si kuzungumza tu na kupiga makelele.

38 Bila shaka, mtu anayemwabudu Mungu, hilo ndilo linalotazamiwa. Hivyo ndivyo ingepaswa kuwa. Hilo ndilo lililokuleta hapa, ni kumwabudu Bwana. Ukijisikia tu kama kumsifu Mungu, ama kupaza sauti, endelea tu, unaona, kwa maana hilo ndilo lililokuleta hapa, unaona, lakini, ni kumwabudu Bwana kwa njia yako mwenyewe ya kuabudu. Lakini hakuna mtu anayemwabudu Mungu wakati mtu unazungumza na kupitishiana vijikaratasi, na unamsaidia mtu mwingine atoke kwenye kumwabudu Bwana, unaona, kwa hiyo tunaona ya kwamba jambo hilo halingekuwa sawa. Na tunataka kufanya uamuzi huo kanisani mwetu, ya kwamba katika kusanyiko letu, ya kwamba, kwenye jengo hili, kanisa hili litawekwa wakfu kwa ajili ya Ufalme wa Mungu na kwa ajili ya kuhubiriwa kwa Neno. Ombeni! Abuduni! Hiyo ndiyo sababu inawapasa kuja hapa, kuabudu, basi.

39 Halafu jambo lingine, wakati ibada imemalizika, kwa kawaida watu makanisani . . . Sidhani—sidhani hilo liko hapa, maana . . . Mara nyingi nimesafiri, mnaona, maana mimi huondoka.

40 Kwa kawaida, hata katika kuhubiri ibada nyingine, upako unakuja, na maono yanatokea. Nami nimeishiwa na nguvu kabisa, na ninaondoka kwenda kwenye chumba kile. Na labda Billy, ama baadhi ya hao watu pale, wananipeleka nyumbani, na

kuniacha nipumzike muda kidogo, mpaka nitokapo katika hilo, kwa maana inachosha akili sana.

41 Na halafu nimeona makanisa, hata hivyo, ambapo watoto wanaachiwa kukimbia kila mahali madhabahuni, na—na watu wazima wamesimama na kuitana tokea upande wa pili wa chumba, wao kwa wao. Hiyo ni njia nzuri ya kuua ibada inayokuja usiku huo, ama wakati wo wote ule uwao. Unaona?

42 Mara ibada inapokwisha, ondokeni kwenye ukumbi wa kukutania. Ndipo mmemaliza, ibada. Basi tokeni nje mkazungumze, na lo lote mnalotaka kufanya. Kama mtu una jambo fulani unalotaka kuzungumza na mtu fulani, ku—kuwaona, vema, fuatana nao, ama nyumbani kwao, ama cho chote kile, lakini usifanye jambo hilo kwenye ukumbi wa kukutania. Hebu na tupaweke hapa wakfu kwa Mungu. Mnaona? Hapa ni mahali Pake pa kukutania, mahali ambapo tunakutana Naye. Mnaona? Na Sheria hutokea kwenye madhabahu, bila shaka. Nami ni—ninaamini ya kwamba jambo hilo lingempendeza Baba yetu wa Mbinguni.

43 Na basi wakati mnapokuja, na mnaanza kuona ya kwamba karama zinaanza kushuka miongoni mwenu . . . Sasa, kwa kawaida ni . . . Ninatumaini hilo halitatukia hapa; lakini, watu wanapopata kanisa jipya, muda si muda unajua, kusanyiko linajivuna. Hutaki jambo hilo litukie hata kidogo. Hata hivyo, hapa ni mahali pa kuabudia. Hii ni nyumba ya Bwana. Na kama karama za kiroho zinaanza kuja kati yenu . . .

44 Ninasikia, ya kwamba tangu nilipoondoka, kwamba watu wamehamia hapa kutoka sehemu mbalimbali nchini, kuifanya hii kuwa maskani yao. Ninashukuru, ninamshukuru Mungu, ya kwamba, ninaamini ya kwamba . . .

45 Asubuhi ile wakati nilipoliweka wakfu na kuliweka lile jiwe la pembeni pale, kama kijana mwanamume, niliomba lidumu lipate kuona kule Kuja kwa Yesu Kristo. Na nilipofanya jambo hilo, nikiwa nina deni la maelfu ya dola, nao . . . Ungeweza kuchukua sadaka katika kusanyiko la ukubwa huu na kupata senti thelathini ama arobaini, na malipo yetu yalikuwa kama dola mia moja na hamsini, mia mbili kwa mwezi. Ningelimudu jambo hilo namna gani? Nami nilijua ya kwamba nilikuwa ninafanya kazi, nami ningelilipa lote. Mimi . . . Miaka kumi na saba ya kazi ya uchungaji bila kuchukua senti moja, bali nikitoa kila kitu nilichokuwa nacho, mimi mwenyewe, nje ya riziki yangu; na zote hizo ziliwekwa kwenye kijisanduku kidogo kule nyuma, kwa Ufalme wa Mungu.

46 Na watu wakatabiri na kubashiri ya kwamba katika muda wa mwaka mmoja lingekuwa gereji. Shetani alijaribu kutunyang'anya hilo wakati mmoja kwa kesi, kesi ya mahakamani. Mtu fulani alidai aliumia mguu alipokuwa akifanya kazi hapo, halafu akaacha kazi, na halafu . . . ndipo

akashtaki na akataka kuichukua maskani. Nami kwa majuma kadha nilisimama mahakamani. Lakini ijapokuwa kulikuwa na kutoelewana kote huko na ubashiri mwingi, na yale waliyosema, linasimama leo kama mojawapo la majumba ya mikutano yaliyo mazuri sana na mojawapo la makanisa yaliyo mazuri sana yaliyoko Marekani. Hiyo ni kweli.

47 Kutoka hapa limetoka Neno la Mungu aliye hai, likaenda kila mahali ulimwenguni, unaona, kila mahali ulimwenguni; na daima limezunguka dunia nzima, kwa kila taifa chini ya Mbingu, kadiri tujuavyo sisi, kuzunguka na kuzunguka dunia. Na tushukuru kwa ajili ya jambo hili. Na tuwe wenye shukrani kwa ajili ya jambo hili.

48 Na sasa kwa kuwa tuna mahali pa kukaa, dari chini ya vichwa vyetu, kanisa zuri, safi la kukaa ndani, hebu na tujiweke wakfu upya kwa ajili ya kazi, na tujiweke wakfu kwa Kristo.

49 Na Ndugu Neville, ndugu yetu mzuri sana, mchungaji halisi, mtumishi wa Mungu aliye hai. Kadiri mtu huyo anavyoujua Ujumbe, anaushikilia, kwa yote aliyo nayo. Hiyo ni kweli. Yeye ni mtu mnyenyekevu. Yeye anaogopa kidogo kuninii . . . Ama, si kuogopa; simaanishi jambo hilo. Lakini yeye ni ninii sana, ni mpole sana, hata hakemei kitu, mwajua, kama vile ku—kusema jambo lililo kali na la kuumiza, ama, "Keti chini," ama, "Nyamaza!" Ni—nimeona jambo hilo, na kusikiliza kanda zake.

50 Lakini inakuwa kwamba mimi ninaweza kufanya hivyo. Kwa hiyo mimi—mimi . . . Nami na—nawatakeni mkumbuke maneno yangu, mnaona. Na haya yote yanarekodiwa, mnaona. Kila kitu kinarekodiwa. Na, tafadhalini, kila shemasi na asimame kwenye wajibu wake wa kazi, na kumbuka ya kwamba uko chini ya agizo la Mungu, kushikilia wajibu huo mtakatifu. Unaona? Kila mdhamini, vivyo hivyo. Mchungaji anapaswa kuleta . . .

51 Si wajibu wa mchungaji kupaswa kusema jambo hilo. Ni wadhamini . . . ama ninamaanisha mashemasi, kwa maana wao ndio mapolisi wa kanisa. Yaani, kama vijana waliofunga ndoa huko nje wanakuja na wanapiga honi, na, mwajua, jinsi wanavyofanya hivyo kwa kawaida, ama kitu kama hicho, mikutanoni, ama wanapotoka huko nje. Na mama anamtuma msichana wake huku, naye anaondoka aende zake na kijana fulani mhuni, nao wanatoka kwenda kutembea na gari, na mama yake anafikiri yuko kanisani, namna hiyo. Shemasi anapaswa kuangalia jambo hilo. "Aidha utaingia ndani hapa na uketi, la sivyo nitakuchukua kwenye gari langu na kukupeleka nyumbani kwa mama yako." Mnaona? Ninyi, hamna budi kufanya jambo hilo.

52 Kumbukeni, upendo husahihisha, unaona, daima. Upendo halisi husahihisha, kwa hiyo hamna budi kustahimili masahihisho. Na, enyi akina mama, jueni sasa ya kwamba kuna mahali kule kwa ajili ya watoto wenu wachanga. Ninyi vijana

wadogo mnajua isivyopaswa kukimbia-kimbia kote kote ndani ya jengo. Mnaona? Na ninyi watu wazima mnajua isivyopaswa kuzungumza na kuendelea na mazungumzo yenu ndani ya mahali pa kukusanyikia. Mnaona? Msifanye jambo hilo. Ni makosa. Halimpendezi Mungu.

53 Yesu alisema, "Imeandikwa, nyumba Yangu itakuwa nyumba ya ibada, maombi. Jinsi ilivyoitwa nyumba ya maombi, na mataifa yote!" Nao walikuwa wakinunua na kuuza, Naye akasokota kamba na kuwafukuza hao watu watoke pale mahali pa kukutania. Na bila shaka sisi hatutaki jambo hilo litukie kwenye madhabahu hii hapa. Kwa hiyo, hebu na tuyaweke wakfu maisha yetu, kanisa letu, kazi zetu, utumishi wetu, na kila kitu tulicho nacho, kwa Ufalme wa Mungu.

54 Sasa, sasa nataka kusoma Maandiko machache kabla ya maombi ya kuweka wakfu. Na—na, halafu, ni kuweka wakfu tena tu, kwa maana kuwekwa wakfu halisi kulifanywa miaka thelathini iliyopita. Sasa katika . . . Halafu, basi tunapo—tunaposoma Maandiko haya na kuyazungumzia kwa dakika chache, ninatumaini ya kwamba Mungu atatuletea baraka Zake.

55 Na sasa kulikuwa na jambo lingine nililokuwa ninataka kusema. Naam. Pale mahali tulipozoea kuwa tuna vinasasauti, na kadhalika, tuna chumba chenye utaratibu hapo, ambamo wale wanaotaka kunasa sauti. Kuna sehemu maalum za kuchomekea, na kila kitu humo, kinachotoka moja kwa moja kutoka kwenye kipaza sauti kikubwa, mle ndani.

Kuna vyumba, mavazi, kila kitu kwa ajili ya ibada ya ubatizo.

56 Na halafu tena jambo moja, watu wengi daima wamenikasirikia, watu wengi ambao kweli hawakujua Maandiko, kuhusu kuweka msalaba wenye sanamu ya Yesu kanisani. Ninakumbuka wakati mmoja jambo fulani lilitukia hapa juu ya jambo hilo. Nilikuwa na misalaba mitatu, na ndugu mmoja alishtuka sana kwa sababu alisikia madhehebu mengine yakisema ya kwamba msalaba wenye sanamu ya Yesu ulimaanisha Ukatoliki.

57 Ninataka mtaalumu fulani, ama mtu fulani, ama Mkristo fulani aliyezaliwa mara ya pili, kusema ya kwamba Wakatoliki ndio walio na haki ya kuwa na msalaba wenye ile sanamu. Msalaba wenye sanamu ya Kristo hauwakilishi Ukatoliki. Huo unamwakilisha Mungu, ule Ufalme. Sasa, watakatifu wanawakilisha Ukatoliki. Tunaamini kuna "Mpatanishi mmoja kati ya Mungu na mwanadamu, na huyo ni Kristo." Lakini Wakatoliki wanaamini katika kila namna ya wapatanishi, maelfu ya wanawake na wanaume, na kila kitu; Mkatoliki ye yote mzuri, karibu kila mmoja, anayekufa, huwa mpatanishi. Sasa, msalaba wenye sanamu ya Kristo unamwakilisha Yesu Kristo.

58 Je! ulijua ya kwamba Wakristo wa mwanzoni, kulingana na—na historia ya kale ya kanisa la mwanzoni, walivaa misalaba migongoni mwao, po pote walipoenda, kuonyesha na kujitambulisha kama Wakristo? Sasa, Wakatoliki wanadai ya kwamba hao walikuwa ndio wao. Bila shaka, wanadai walikuwa ndio wa kwanza, lakini kanisa Katoliki hata halikuwa limefanyika madhehebu wakati huo. Mnaona? Lakini Wakristo walivaa msalaba kwenye . . . Mmewasikia watu wakisema, "msalabamgongoni." Mnalichukulia hilo kuwa ni Wakatoliki?

59 Ni yule mkatoliki halisi, lile Kanisa la Roho Mtakatifu la mahali pote ulimwenguni, ndilo lililo sahihi. Sisi ni Wakatoliki. Sisi ndio wale wakatoliki wa mwanzoni, wakatoliki wanaoamini Biblia. Unaona? Wao ndio kanisa, Katoliki, madhehebu. Sisi tumetoka kwenye jambo hilo. Sisi ndio mfululizo wa Mafundisho ya mitume. Sisi ndio mfululizo wa ubatizo wa Roho Mtakatifu na mambo yote yale ambayo Kanisa la mwanzoni lilitetea, na kanisa Katoliki halina hata moja ya mambo hayo. Unaona?

60 Kwa hiyo, wao waliweka msalaba wenye sanamu ya Yesu hapa, ulioletwa, uliokatwa kutoka kwenye mti wa mzeituni chini ya mahali ambapo Yesu aliombea. Huo ndio msalaba wenye sanamu ya Yesu uliochukua miaka kadha, na niliupewa na Ndugu Arganbright. Nami nataka kuuweka wakfu pamoja na kanisa hili.

61 Na jinsi lilivyokuja sawa, jambo hilo, ye yote yule aliyeutundika pale. Sijui alikuwa ni nani, aliyeuning'iniza hapa kwenye—kwenye mkono wangu wa kushoto. Yeye alimsamehe yule mwizi aliyekuwa mkono Wake wa kulia; huyo ni mimi.

62 Na jambo lingine unalowakilisha, kwa kuwa kichwa Chake kimeinamishwa, unapoona mateso Yake. Watu wo wote ambao ananinii . . . Anaangalia madhabahuni. Naye anakutarajia wewe hapa, ewe mwenye dhambi, naye atakuwa anakuangalia wewe hapo chini. Baadaye wataweka taa ndogo hapa, ili kwamba wakati wito wa madhabahuni unapofanywa, nuru itamulikia hapo, ili kwamba wakati watu wakiwa wako hapa kwa ajili ya . . .

63 Unasema, "Unauhitaji huo kwa ajili gani? Hupaswi kuwa na sanamu."

64 Vema, basi, Mungu yule yule aliyesema, "Usijifanyie sanamu za kuchonga," Mungu yuyo huyo alisema, "Fanya makerubi wawili na ncha za mbawa zao zishikane, ukawaweke kwenye kiti cha rehema pale watu wanapoomba."

Unaona, ni—ni, kutokufahamu. Unaona?

65 Kwa hiyo, huo ni uongozi wa Mungu nao unaning'inia moja kwa moja mahali pake panapofaa. Nami ninashukuru sana kuwa upande wa kulia. Ninatumaini ya kwamba Yeye amenisamehe, kwa kuwa mimi, kuhusu kweli kuiba kitu cho chote, nijuavyo mimi, sijaiba maishani mwangu; lakini nimetumia vibaya sana

wakati Wake hata nikaiba namna hiyo. Na nimefanya mambo mengi ambayo sikupaswa kuyafanya. Nami ninamshukuru Mungu, asubuhi ya leo, ya kwamba amenisamehe dhambi zangu.

66 Na sasa ninataka kusoma kutoka katika Kitabu cha Mambo ya Nyakati wa Kwanza 17, na kuzungumza tu kwa yapata dakika tano kwa ibada ya kuweka wakfu, tuombe, kisha tuingie kwenye Ujumbe. Sasa, katika Mambo ya Nyakati wa Kwanza, su—sura ya 17.

> *Ikawa, Daudi alipokuwa akikaa nyumbani mwake, kwamba Daudi akamwambia nabii Nathani, Angalia, mimi ninakaa katika nyumba ya* mwerezi, *bali sanduku la agano la Bwana linakaa chini ya mapazia.*
>
> *Naye Nathani akamwambia Daudi, Haya, fanya yote yaliyomo moyoni mwako; kwa maana Mungu yu pamoja nawe.*
>
> *Ikawa usiku uo huo, ya kwamba neno la BWANA likamjia Nathani, kusema,*
>
> *Nenda, kamwambie* Daudi mtumishi Wangu... *Nenda, kamwambie, mtumishi wangu, Daudi*, (hasa), *BWANA asema hivi, Wewe hutanijengea nyumba ya kukaa;*
>
> *Kwa maana sikukaa ndani ya nyumba tangu siku ile nilipowaleta Israeli huku hata leo; lakini hema kwa hema nimehamia, na maskani kwa maskani.*
>
> Basi *katika mahali mwote nilimokwenda na Israeli wote, je! nimesema neno lo lote na mtu ye yote wa waamuzi wa Israeli, niliowaagiza kuwalisha watu Wangu, nikisema, Mbona hamkunijengea nyumba...?*
>
> *Basi sasa ndivyo utakavyomwambia....Daudi, BWANA wa majeshi asema hivi, Nalikutwaa katika zizi la kondoo, katika kuwaandama kondoo, ili uwe mkuu juu ya watu Wangu Israeli;*
>
> *Nami nimekuwa pamoja nawe* kila *ulikokwenda, na kuwakatilia mbali adui zako wote mbele yako; Nami nimekufanyia jina kama jina la...hao wakuu walioko duniani.*

67 Ningetaka kusema, mahali hapa, ya kwamba—ya kwamba Daudi aliona jambo lile lile tuliloona. Daudi alisema, "Si vizuri kwamba ninyi watu mmenijengea mimi nyumba ya mwerezi, na sanduku la agano la Mungu wangu lingali chini ya mapazia." Hayo yalikuwa ni ngozi zilizoshonwa pamoja, za kondoo na wanyama. Akasema, "Si vizuri kwangu kuwa na nyumba nzuri, na sanduku la agano la Mungu wangu likiwa linakaa katika hema." Kwa hiyo, Mungu akaweka ndani ya moyo wake kujenga maskani.

68 Lakini, Daudi, ingawa alikuwa m—mtu wa—wa upendo na wa kujitolea kwa Mungu, hata hivyo alikuwa amemwaga damu nyingi sana. Kwa hiyo akasema . . . Daudi, akisema haya mbele ya nabii wa wakati huo, ambaye alikuwa ni Nathani. Naye Nathani, akijua ya kwamba Mungu alimpenda Daudi, akasema, "Daudi, fanya yote yaliyomo moyoni mwako, kwa kuwa Mungu yu pamoja nawe." Ni maneno ya ajabu jinsi gani! "Fanya yote yaliyomo moyoni mwako, kwa maana Mungu yu pamoja nawe." Na usiku uo huo . . . Ikionyesha kujiweka wakfu kwa Daudi kwa kumpenda Mungu.

69 Na halafu kuona, usiku uo huo, akijua ya kwamba alikuwa makosani, ya kwamba hakuruhusiwa kufanya jambo hilo, Mungu alikuwa mwingi wa neema vya kutosha kushuka na kunena na Nathani. Nami daima nimeyapenda maneno haya, "Nenda ukamwambie Nathani nanii Wangu . . . Nenda kamwambie Daudi mtumishi Wangu, ya kwamba, 'Nalikutwaa katika zizi la kondoo.'" Ni kwamba, si kwamba hakuwa cho chote.

70 Nami ni—ningetaka kulitumia jambo hilo hapa, kwa muda kidogo tu. "Nalikutwaa ukiwa hu cho chote, nami ni—ni—nikakupa jina. Una jina kama la watu wakuu walioko duniani." Nami ningetaka kutumia jambo hilo katika—katika njia ya kibinafsi, walakini katika njia—njia ya kusema jambo fulani. Nilikuwa nikifikiri ya kwamba . . .

71 Miaka michache iliyopita, mimi nikiwa nimesimama mjini hapa, wala hakuna mtu aliyenijali. Hakuna mtu aliyenipenda. Nami niliwapenda watu, lakini hakuna mtu aliyenipenda, kwa sababu ya historia ya jamaa yangu. Si kuwadharau mama na baba yangu wapendwa.

72 Jinsi ninavyotamani kwamba mama angaliishi hata afikie wakati atembee katika madhabahu hii, asubuhi hii. Wengi wa watu wa zamani waliotoa pesa zao kusaidia kupajenga mahali hapa, labda Mungu, asubuhi hii, atawaruhusu kuangalia upande wa pili wa safu ya pazia.

73 Lakini ukoo wa Branham haukuwa na jina zuri sana mahali hapa, kwa sababu ya ulevi. Hakuna mtu aliyejihusisha nami. Nami ninakumbuka kumwambia mke wangu si muda mrefu uliopita, kumbuka tu ya kwamba si—sikuweza kumpata mtu wa kuzungumza nami. Hakuna mtu aliyenijali. Na hivi sasa inanibidi kujificha, kusudi nipate kupumzika kidogo.

74 Na sasa Bwana ametupa mahali hapa pazuri sana, na—na mambo haya makubwa ambayo Yeye amefanya. Naye amenipa mimi ninii . . . Mbali na ji—jina baya, Yeye amenipa jina kama la baadhi ya watu wakuu. Naye amewakatilia mbali adui zangu po pote nilipokwenda. Hakuna kitu kilichowahi kusimama mbele Yake, po pote ulipokwenda. Lakini, na jinsi ninavyoshukuru kwa ajili ya jambo hilo.

75 Nami ningepataje kujua; nikiwa ni mtoto mdogo anayevaa matambaa juu hapa, umbali wa safu ya majumba mawili ama matatu ya mji kutoka hapa, hadi kwenye Shule ya Ingramville, wakati nilipokuwa ni kicheko cha shule, kwa kuvaa nguo zilizoraruka sana, na kujitelezesha kwenye kidimbwi kilichokauka? Nilipataje kujua ya kwamba kule chini ya kidimbwi hicho kulikuwa na mbegu ya yungiyungi ambalo lingeweza kuchanua namna hii? Na nilipataje kujua, ya kwamba, hakuna mtu wa kuongea nami, na hata hivyo Yeye angenipa ji—jina ambalo lingeheshimiwa miongoni mwa watu Wake?

76 Na, sasa, Daudi hakuruhusiwa kujenga lile hekalu. Hangeweza kufanya jambo hilo. Lakini alisema, "Nitainua katika mzao wako, naye atajenga hekalu hilo, na hekalu hilo litakuwa hekalu la milele. Na kwa mwanao, mwana wa Daudi, utakuwako ufalme wa milele; yeye atatawala." Sulemani, mwana wa Daudi kimwili, kutokana na nguvu zake za kimwili, alimjengea Bwana nyumba, hekalu.

77 Lakini wakati Mzao wa kweli wa Daudi ulipokuja, Mwana wa Daudi, Yeye aliwaambia utakuja wakati ambapo hapatasalia jiwe juu ya jiwe, la hekalu hilo. Lakini alijaribu kuwaonyesha hekalu lingine.

78 Yohana, mfunuzi, katika Kitabu cha Mafunuo, aliiona Maskani hii. Mafunuo 21, yeye aliona, "Lile Hekalu jipya likija, likishuka chini kutoka Mbinguni, limepambwa kama bibi-arusi aliyekwisha kupambwa kwa mumewe. Na Sauti kutoka katika lile Hekalu, ikasema, 'Tazama, Maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu, Naye Mungu atakuwa pamoja nao, nao watafuta machozi yote katika macho yao. Wala njaa haitakuwapo tena, wala huzuni tena, wala maumivu tena wala mauti; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita.'"

79 Basi Mwana halisi wa Daudi, kama tutakavyoona katika masomo haya yajayo kwenye juma hili, atakuja kwenye Hekalu Lake, Hekalu la Mungu, ile Maskani halisi ambayo Yeye ameondoka kwenda kuitengeneza sasa. Kwa kuwa, Yeye alisema, katika Yohana 14, "Nyumbani mwa Baba Yangu mna makao mengi, nami nitaenda. . ." Yeye alimaanisha nini kwa jambo hilo? Tayari limekwisha amriwa tangu zamani. "Nami nitaenda kuwatengenezea Mahali, kisha nitarudi, na kuwapokea Kwangu." Na, bila shaka, tunajua hilo litakuwa katika Wakati ule mkuu ujao. Na yule Mzao wa kweli wa Daudi atatawala kwenye Kiti cha Enzi, ambaye ni Yesu Kristo, Naye pale atatawala juu ya Kanisa, kama Bibi-arusi Wake, katika Nyumba hiyo pamoja Naye, na juu ya yale makabila kumi na mawili ya Israeli, katika Milele yote.

80 Na maskani hizi ndogo ndogo; kama vile Daudi, hangeweza kujenga Maskani ya kweli ya Mungu, kwa maana yeye hakuwa amejitayarisha kuijenga. Hakuna kitu yeye angeweza kufanya.

Yeye alikuwa mwanadamu, na alimwaga damu. Ndivyo na ilivyo leo, kwetu sisi, hatujawa tayari kuijenga Maskani ya kweli ya Mungu. Kuna Mmoja tu anayeweza kuijenga hiyo, na hivi sasa ndiyo inajengwa.

81 Lakini maskani hii ndogo, pamoja na lile hekalu ambalo Sulemani alimjengea Yeye, na pamoja na zile nyingine, ni mahali pa muda tu pa kuabudia mpaka utakapowadia wakati ambapo Maskani ya kweli itakapojengwa duniani. "Na haki itatawala kutoka mbingu hadi mbingu. Na hakutakuwako na huzuni tena." Hakutakuwako na mazishi yatakayohubiriwa katika Maskani hiyo. Hakutakuwapo na arusi tena, kwa maana Arusi itakuwa ni Arusi moja kuu ya Milele. Itakuwa ni wakati wa namna gani!

82 Lakini hebu na tukusudie moyoni mwetu, leo, ya kwamba kwa ukumbusho na kwa kungojea kuja kwa Maskani hiyo, ya kwamba tutajifananisha sana na Roho Wake, hivi kwamba tutaabudu katika mahali hapa kana kwamba tulikuwa katika Mahali pale pengine, tunapongojea Mahali pale paje.

83 Sasa hebu na tusimame kwa miguu yetu, wakati napo nisoma Maandiko Matakatifu.

> *Kisha nikaona mbingu mpya na nchi mpya; kwa maana mbingu za kwanza na nchi ya kwanza zimekwisha kupita, wala hapana bahari tena.*
>
> *Mimi Yohana nikauona mji ule mtakatifu, Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mungu, umewekwa tayari, kama bibi-arusi aliyekwisha kupambwa kwa mumewe.*
>
> *Nami nikasikia* ninii . . . *sauti kubwa kutoka mbinguni ikisema, Tazama, maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu, naye atafanya maskani yake pamoja nao, nao watakuwa watu wake. Naye Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao, nao watakuwa watu wake.*

Na tuinamishe vichwa vyetu sasa.

84 Baba yetu aliye Mbinguni, tunasimama kwa kicho. Tunasimama kwa heshima na katika uchaji Mtakatifu. Nasi tunakuomba, Bwana, ukubali zawadi yetu, kwamba umetupa neema, fedha, kutayarisha mahali pa kukuabudia. Hakuna kitu cho chote, ama hakuna mahali ambapo tungetayarisha duniani, ambapo pangefaa kwa—kwa Roho wa Mungu kukaa. Lakini tunakutolea mahali hapa kama ishara ya upendo wetu na nia ya moyo wetu Kwako, Bwana. Nasi tunakushukuru kwa ajili ya mambo yote ambayo umetufanyia.

85 Na, sasa, jengo na viwanja vyake viliwekwa wakfu muda mrefu uliopita, kwa ajili ya ibada, nasi tunakushukuru kwa ajili ya kumbukumbu la yale yaliyotokea. Na sasa, Bwana Mungu, kama vile ono lilivyotokea, miaka mingi iliyopita, likionyesha jambo hili, ya kwamba niliona majengo ya kale ambamo

watu waliishi wakati mmoja, na yalikuwa yamekarabatiwa na kufanywa mapya, nami nikatumwa nirudi kutoka ng'ambo ya mto.

86 Sasa, Bwana Mungu, Muumba wa mbingu na nchi, tunasimama kama watu wa zizi Lako. Tunasimama kama wa—wa—watu wa Ufalme Wako. Na pamoja na mimi mwenyewe, na mchungaji, na kanisa, watu hawa, tunaliweka wakfu jengo hili kwa ajili ya utumishi wa Mwenyezi Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, Mwanawe, kwa ajili ya utumishi wa Mungu, na kwa uchaji na heshima ya Mungu. Na naomba Injili imiminike kutoka mahali hapa kiasi kwamba itaufanya ulimwengu uje kutoka pande nne za dunia, kuona Utukufu wa Mungu ukitoka kutoka kwake. Kama vile Wewe ulivyotenda huko nyuma, naomba wakati ujao uwe wenye nguvu mara nyingi zaidi.

87 Baba, sasa tunajiweka wakfu kwa ajili ya ibada, kwa Neno, kwa yote yaliyomo ndani yetu. Bwana, kusanyiko hili pamoja na watu, wanajiweka wakfu, asubuhi hii, wapate kulisikia Neno. Nasi, kama wahudumu, tunajiweka wakfu, "Kwa ajili ya kulihubiri Neno; tukiwa tayari wakati ufaao, wakati usiotufaa; tukikaripia, tukikemea kwa uvumilivu wote." Kama ilivyoandikwa pale kwenye jiwe la pembeni, toka miaka thelathini iliyopita. Wewe ulisema, "Utakuja wakati watakapoyakataa Mafundisho yenye uzima; ila watajipatia waalimu makundi makundi, kwa kuwa wana masikio ya utafiti; nao watajiepusha wasisikie yaliyo Kweli, na wazigeukie hadithi za uongo." Bwana, kama vile tulivyojaribu kuwaonyesha watu Neno, twaomba utujalie tuvuviwe na kutiwa nguvu kwa jitihada maradufu. Bwana, wakati sehemu maradufu ya Roho inapopagusa mahali hapa, twaomba ujalie Roho Mtakatifu . . .

88 Kama ilivyokuwa katika ile siku ya kuwekwa wakfu kwa lile hekalu, wakati Sulemani alipoomba; Roho Mtakatifu, katika mfano wa Nguzo ya Moto pamoja na Wingu, aliingia kupitia mlango wa mbele, akawazunguka wale Makerubi, akaenda pale Mahali Patakatifu na hapo akapatwaa mahali Pake pa mapumziko. Ee Mungu! Sulemani alisema, "Kama watu Wako wakiwa katika shida mahali po pote, wakiangalia Mahali hapa Patakatifu na kuomba, basi sikia kutoka Mbinguni."

89 Bwana, jalia Roho Mtakatifu, asubuhi ya leo, aingie katika kila moyo, kila nafsi iliyowekwa wakfu iliyopo hapa ndani. Na Biblia inasema, ya kwamba, "Utukufu wa Mungu ulikuwa mwingi sana mpaka hata wahudumu hawakuweza kuhudumu, kwa ajili ya Utukufu wa Mungu." Ee Bwana Mungu, jalia irudie tena tunapojitoa Kwako, pamoja na kanisa hili, katika kujiweka wakfu kwa ajili ya ibada. Na imeandikwa, "Ombeni, nanyi mtapokea."

90 Nasi tunajitoa, pamoja na matoleo yetu ya kanisa hili, asubuhi hii, Kwako, kwa ajili ya ibada, kwa ajili ya Nuru za siku

za mwisho, kwa ajili ya Nuru za wakati wa jioni; ili kwamba tupate kuleta faraja na imani kwa watu wanaongojea ambao wanangojea kule Kuja kwa Bwana Arusi, kumvalisha Bibi-arusi Injili ya Kristo, Bwana Yesu apate kumpokea. Tunaliweka hili wakfu, mimi mwenyewe, Ndugu Neville, na kusanyiko, kwa utumishi wa Mungu, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mnaweza kuketi.

91 Daudi alisema, "Nilifurahi waliponiambia, 'Na twende nyumbani kwa Bwana.'" Basi jalia daima iwe kwetu, kwamba, wakati jambo hilo linapotajwa, tutafurahi kukusanyika katika nyumba ya Bwana. [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Amina.

92 Sasa, baada ya hiyo ibada ndogo ya kuweka wakfu, nina saa moja sasa.

93 Na, sasa, kumbukeni tu sasa tumejiweka wakfu kwa ajili ya kitu gani; kwa uchaji, utakatifu, utulivu mbele za Bwana, kuabudu mbele za Bwana. Na mwe wenye uchaji tu mwezavyo kuwa, katika nyumba ya Bwana. Na, sasa, na wakati ibada inapofungwa, mara baada ya ibada kufungwa, tokeni humu jengoni. Mnaona? Na jambo hilo linampa bawabu wakati wa kuingia hapa na kulisafisha kwa ajili ya wakati mwingine, na kulitayarisha. Ndipo hapatakuwa na machafuko katika nyumba ya Bwana. Na . . .? . . . Ninafikiri ninyi . . . mahali hapa patasafishwa katika muda wa kama dakika kumi na tano baada ya ibada kufungwa. Hakikisheni mnashikamana. Peaneni mikono na kila mtu, na alikeni kila mtu arudi tena.

94 Na—na tunatarajia kupata, juma hili lijalo sasa, moja ya ibada takatifu sana ambazo zimewahi kufanywa hapa maskanini. Tunatazamia jambo hilo. Sasa, mimi—mimi . . . sikung'amua hata kidogo jambo hilo mpaka jambo fulani . . . mpaka usiku sana, majira ya usiku sana jana usiku, katika maombi, nilianza kuona jambo fulani. Kwa hiyo, ninatumaini huu utakuwa ni wakati mkuu, ambao ninaamini utakuwa mkuu, kama Bwana atatusaidia. Sasa, sasa, niliposema, "wakati mkuu," sasa, nitazungumzia jambo fulani kuhusu jambo hilo, asubuhi hii. Mnajua, yale mwanadamu anayoita "makubwa," wakati mwingine si makuu. Lakini yale Mungu anayoita "makubwa," mwanadamu huyaita upumbavu; na yale Mungu anayoita "upumbavu," mwanadamu huyaita makubwa. Kwa hiyo hebu na tuweke jambo hilo niani mwetu, tupime kila Neno.

95 Sasa ibada ni ndefu. Zitakuwa ndefu, kwa sababu ni ibada ngumu, mafundisho mengi, kujiweka wakfu. Nami ninaninii . . .

96 Mahali ambapo ninakaa, watu wanajaribu tu, wanataka kunilisha kila kitu, lakini mimi . . . Kasema, "Vema, umepoteza uzito mwingi mno, Ndugu Branham, kila kitu." Lakini daima nimekuwa katika utumishi. Sina budi kuondoka hapa Jumapili ijayo usiku, kwenda kwenye ibada nyingine, upesi sana, huko

Meksiko. Kwa hiyo, ni jambo tu gumu. Kwa hiyo, lakini ninajaribu tu kuacha kula sana, na—na ninajitayarisha.

97 Nami nina furaha, asubuhi ya leo, kumwona Ndugu Junior Jackson, na—na Ndugu Ruddell, na—na wahudumu mbalimbali, na kadhalika, hapa. Mungu awabariki nyote.

98 Sasa na—nataka ku—kuwazungumzia asubuhi ya leo juu ya somo ambalo nimeliandika mihtasari michache hapa. Nami nataka kusoma kwanza kutoka katika Kitabu cha Isaya, sura ya 53. Sasa, wakati mnapoifungua, ningetaka kutangaza tangazo moja, ama mawili.

99 Ya kwamba, usiku wa leo, ninataka kuzungumza juu ya Kitabu *hiki*, kukiunganisha kati ya wakati wa mwisho wa kanisa na kule kufunguliwa kwa ile Mihuri. Sasa, pana pengo kubwa sana hapo.

100 Na, hapo nyuma, nilipomaliza zile nyakati saba za kanisa, nilizungumza pia pale juu ya yale majuma sabini ya Danieli, mara baada yake, maana hayo yaliunganisha. Nami nikasema, "Sasa, kama nikiwahi kuhubiri ile Mihuri Saba, itanibidi kumaliza majuma haya sabini ya Danieli, kusudi nipate kuingiza ile Mihuri." Nikiacha jambo moja wazi, na hilo lilikuwa ni sura ya 5, ya kile Kitabu Kilichotiwa Muhuri Saba. Nasi tutakichukua hicho usiku wa leo.

101 Tunataka kujitahidi kuanza mapema usiku wa leo. Jinsi ambavyo mimi . . . Tayari umelitangaza jambo hilo, sivyo, kuanza mapema? [Ndugu Neville anasema, "Ndiyo."—Mh.] Vipi kuhusu, je! kila mtu anaweza kuwa hapa kwenye kama saa moja hivi? [Kusanyiko linasema, "Amina."] Vema. Hebu na tuanze ibada ya kawaida saa kumi na mbili na nusu, ibada ya nyimbo, nami nitakuwa hapa kwenye saa moja. Na halafu katika juma lote zima tutaanza mapema. Na—nasi, sasa, tunakuja . . .

102 Hakuna mtu anayependa kuimba kama vile Wakristo wanavyopenda kuimba. Tunapenda kuimba. Tunapenda mambo hayo.

103 Lakini sasa tuko—tuko kwenye jambo lingine sasa. Tuko—tuko kwenye Neno, unaona, kwa hiyo hebu—hebu na tuendelee moja kwa moja na jambo Hilo sasa. Tutafanya hivyo. Tuko—tuko kwenye kufundisha. Nanyi mnaweza kujua jinsi nilivyo na uchovu mkuu wa akili, unaona, kwa sababu, kama nikifundisha jambo lo lote makosa, itanibidi kuja kujibu kwa ajili ya jambo hilo. Mnaona? Na kwa hiyo sipaswi kuchukua lile analosema mtu mwingine ye yote. Sina budi . . . Halina budi kuvuviwa. Nami ninaamini ya kwamba wale Malaika Saba, Ambao wanazishikilia hizi Ngurumo Saba, watatujalia. Unaona?

104 Na sasa katika Isaya, sura ya 53 ya Isaya, aya ya 1, ama mbili. Ninataka kuuliza swali hili.

105 Sasa, hili halihusu ile Mihuri Saba, hata kidogo. Huu ni Ujumbe tu. Kwa kuwa, nilijua ilinibidi kufanya ibada ya kuweka wakfu, nami singeweza kuingilia Hilo kwa maana nisingekuwa na wakati. Lakini nilifikiria, kwa ajili tu ya ibada ndogo ya kuweka wakfu, ibada ndogo ya kumbukumbu kwa ajili ya kanisa hili, ama ibada ndogo ya kuweka wakfu, hasa, basi wao—wao . . . kusingekuwa na wakati basi wa kuingilia jambo ninalotaka kusema, unaona, juu ya huku kufunguliwa kwa Kitabu hiki, kwa hiyo nitafanya hivyo usiku wa leo. Na sasa hii ni ibada ndogo tu, ambayo, ita—itaingiana moja kwa moja Nayo, hata hivyo.

106 Kwa hiyo, sasa, sikiliza kila Neno. Likamate. Na—na iwapo mnaunasa Huo kwenye kanda, ama cho chote kile, basi shikilieni kabisa Mafundisho hayo ya kanda. Msiseme kitu ila kile kanda hiyo inachosema. Semeni tu yale hasa kanda inayosema. Mnaona? Sasa, kwa maana, baadhi ya mambo hayo, tutafahamu mengi sana kuhusu jambo hili sasa, ni kwa nini linafahamika vibaya. Unaona? Nanyi mwe na hakika, semeni tu yale tu kanda inayosema. Msiseme jambo lingine lo lote. Mnaona? Maana, sisemi jambo Hilo kwa nafsi yangu mwenyewe. Yeye Ndiye anayesema Hilo, mnaona. Na mara nyingi sana, vurugu, watu wanainuka na kusema, "Vema, *Fulani* alisema ilimaanisha *hivi-na-hivi*." Liache tu jinsi lilivyo.

107 Unaona, hivyo ndivyo tunavyoitaka Biblia. Ni jinsi vile Biblia inavyosema tu, hivyo ndivyo jinsi tunavyotaka iwe, namna—namna Hiyo tu. Usiweke maelezo yako Kwake. Tayari imefasiriwa, unaona. Sasa:

> *Ni nani aliyesadiki habari tuliyoileta? na mkono wa BWANA amefunuliwa nani*?

108 Hebu nipasome tena sasa, kwa makini.

> *Ni nani aliyesadiki habari tuliyoileta*? (Swali!) *na mkono wa BWANA amefunuliwa nani*?

109 Kwa maneno mengine, "Kama umesadiki habari tuliyoileta, basi mkono wa Bwana umefunuliwa." Unaona?

> *Ni nani aliyesadiki habari tuliyoleta? na mkono wa BWANA amefunuliwa nani*?

110 Sasa nataka kusoma pia katika Kitabu cha Injili ya Mathayo Mtakatifu, sura ya 11 ya Mathayo Mtakatifu. Na, sasa, leteni makaratasi yenu na kadhalika, kwa sababu daima tutaninii . . . Kama huna kinasasauti, le—lete ninii . . . karatasi yako ili kwamba tuweze kulichukua. Sura ya 11 ya Mathayo Mtakatifu, aya ya 25 na 26, 11:26 na 27. Vema, Yesu akinena, katika maombi. Ninataka kuanzia nyuma kidogo ya hapo. Hebu na tuchukue aya ya 25 na 26. Naamini hapo ndipo nilipotangaza, hata hivyo, kwa maana nilikuwa nimepatia alama hapa katika Biblia yangu.

> *Wakati ule Yesu akajibu, akasema, Nakushukuru, Ee Baba, Bwana wa mbingu na nchi, kwa kuwa mambo haya uliwaficha wenye hekima na akili, ukawafunulia watoto wachanga.*
>
> *Naam, Baba, kwa kuwa ndivyo ilivyopendeza mbele zako.*

111 Yashike Maandiko hayo mawili. "Ni nani aliyesadiki habari tuliyoleta? Na mkono wa Bwana amefunuliwa nani?" "Hata wakati huo Yesu akamshukuru Mungu ya kwamba alikuwa amezificha zile siri kwa wenye hekima na akili, na angewafunulia watoto wachanga ambao wangejifunza, kwa kuwa ndivyo ilivyompendeza Mungu kufanya jambo hilo." Sasa, kutoka kwenye fungu hili la maneno, ama ninii . . .

112 Kutoka kwenye somo hili la Maandiko, ninatoa fungu hili la maneno: *Mungu Akijificha Katika Urahisi, Halafu Akijifunua Kwa Jinsi Hiyo Hiyo*. Sasa, kwa ajili ya kanda ninarudia na kurudia namna hiyo, kwa ajili ya kanda, mnaona, maana wao—wao wanarekodi Haya. Mnaona? *Mungu Akijificha Katika Urahisi, Halafu Akijifunua Kwa Jinsi Hiyo Hiyo*.

113 Ni ajabu kuwazia jinsi Mungu anavyofanya jambo kama hilo. Mungu atajificha katika kitu ambacho ni rahisi sana ambacho kitawafanya wenye hekima kukikosa maili milioni moja; kisha ageuke moja kwa moja, katika jambo hilo, jambo fulani rahisi katika urahisi wa njia Yake ya kutenda kazi, na kujifunua Mwenyewe moja kwa moja tena. Nilifikiri lilifanya so—somo, ili kwamba tujifunze jambo hili kabla hatujaingilia yale ma—ma—masomo makuu ya ile Mihuri Saba. Wengi humkosa kwa njia anayojifunua Mwenyewe.

114 Sasa, watu wana mawazo yao wenyewe ya vile Mungu anavyopaswa kuwa na yale Mungu anayoenda kufanya. Na kama vile nilivyotoa yale matamshi yale ya zamani mara nyingi, ya kwamba, mwanadamu bado anabakia kuwa mwanadamu. Mwanadamu daima anamsifu Mungu kwa yale aliyofanya, na daima anatazamia yale atakayoyafanya, huku akipuuza yale anayofanya sasa hivi. Unaona? Unaona? Hivyo ndivyo wanavyolikosa. Wanaangalia nyuma na kuona ni jambo kuu jinsi gani alilofanya, lakini wanakosa kuona ni kitu rahisi jinsi gani alichotumia, kulifanya jambo hilo kwa kitu hicho. Unaona? Na halafu wanaangalia mbele na kuona jambo kubwa linalokuja, litakalotukia, na, mara tisa ya kumi, tayari linatendeka papo hapo walipo. Nalo ni rahisi mno hivi kwamba hawana habari nalo. Unaona?

115 Siku moja, m—mtu fulani juu hapa huku Yutika . . . Na kama baadhi ya watu wake wako hapa, sisemi jambo hili kwa ajili ya jambo lo lote—kwa ajili ya jambo lo lote la kumwaibisha mtu huyo. Alikuwa a—askari mzoefu wa Vita vya ndani. Nami naamini alikuwa . . . Sijui alikuwa ni wa upande gani, lakini

naamini alikuwa ni Mwasi. Lakini, a—alikuwa ni kafiri, naye alidai kwamba hakukuwa na kitu kama Mungu. Aliishi huko Yutika. Jina lake lilikuwa ni Jim Dorsey. Wengi wenu ninyi watu huenda mlimjua.

116 Amenipa matikiti maji mengi, nilipokuwa mvulana mdogo. Alikuwa akilima matikiti maji mtoni, kule—kule mabondeni. Naye alikuwa rafiki sana wa baba yangu. Lakini yeye alisema, siku moja, moja ya mambo makuu sana yaliyopata kusemwa kumhusu yeye mwenyewe, dhidi yake. Sasa, mimi nilikuwa ni kijana mdogo tu siku hizo. Lakini, kinyume cha aliyoamini, jambo hilo lilimfanya aondoke na kuinamisha kichwa chake na kulia. Nami nalisikia kwamba, kwa jambo hili, mtu huyo aliokolewa kiajabu kwa Kristo akiwa na umri wa yapata miaka themanini na mitano.

117 Yeye alimwuliza msichana mmoja mdogo, siku moja, ambaye alikuwa anatoka shule ya Jumapili, kwa nini alipoteza wakati wake akifanya jambo kama hilo? Akasema, ni kwa sababu aliamini ya kwamba kulikuwako na Mungu. Naye Bw. Dorsey akasema ya kwamba, akasema, "Mtoto, umekosea mno, kuamini kitu kama hicho."

118 Naye akasema ya kwamba huyo msichana mdogo aliinama chini akachuma ua do—dogo kutoka . . . kutoka ardhini, akaling'oa kutoka kwenye petali zake, na kusema, "Bw. Dorsey, unaweza kuniambia jinsi hili linavyoishi?"

119 Hivyo ndivyo ilivyokuwa. Wakati alipoanza kuwazia akilini mwake, angaliweza kumwambia yule mtoto, "Vema, linaota ardhini." Na ndipo maswali yangezuka tena, "Hiyo ardhi ilitoka wapi? Hiyo mbegu ilifikaje hapa? Ilitokeaje?" Kuendelea, na kuendelea, na kuendelea, na kurudi nyuma mpaka akaona. Unaona?

120 Si yale mambo makuu yanayovutia macho kwa uzuri tunayowazia habari zake, bali ni yale mambo rahisi ambamo humo Mungu ni halisi sana, ule urahisi. Kwa hiyo, inampendeza Mungu kujifunua, na kisha ajifiche; halafu anajificha, na kujifunua, katika mambo madogo, yaliyo rahisi. Hayo yana—yanaruka juu ya kichwa cha binadamu.

Kwa sababu, kama ungesema, "Kwa nini Mungu mwenye haki afanye jambo hilo?"

121 Ni kwa sababu kwamba binadamu alifanywa, hapo mwanzo, kutojaribu kujichunga yeye mwenyewe. Mwanadamu alifanywa apate kumtegemea Mungu kabisa kabisa. Hiyo ndiyo sababu tunafananishwa na wana-kondoo, ama kondoo. Kondoo hawezi kujiongoza; hana budi kuwa na kiongozi. Naye Roho Mtakatifu anapaswa kutuongoza. Kwa hiyo, mwanadamu ameumbwa namna hiyo.

122 Na Mungu alifanya kazi Zake zote rahisi sana, ili watu wa kawaida wangeweza kufahamu. Na Mungu hujifanya rahisi,

pamoja na walio rahisi, kusudi apate kufahamika na watu wa kawaida. Kwa maneno mengine, Yeye alisema, katika Isaya 35, ninaamini. Yeye alisema, "Ajapokuwa mjinga, hatapotea katika njia hiyo." Ni rahisi sana!

123 Na tunajua ya kwamba Mungu ni mkuu sana, mpaka tunatarajia iwe ni kitu fulani kikuu, nasi tunakosa jambo lililo rahisi. Tunajikwaa kwenye jambo rahisi. Hivyo ndivyo tunavyopitwa na Mungu, ni kwa kukosa kuona urahisi wa jambo. Mungu ni rahisi mno mpaka wanachuoni wa siku hizi, na wa siku zote, wanamkosa maili milioni moja. Kwa sababu, katika akili zao, wanajua ya kwamba hakuna kitu kama Yeye, aliye mkuu sana; lakini, katika kujifunua Kwake, Yeye hulifanya jambo hilo rahisi sana watu wanaliruka na kulikosa.

124 Sasa, jifunzeni jambo Hilo. Jifunzeni Hilo sana. Nanyi watu ambao ni wageni hapa, mtakaporudi kwenye vyumba vyenu vya hoteli, yachukueni mambo hayo na kuyatafakari. Hatuna wakati wa kuyavunja-vunja kama vile yanavyopaswa kuvunjwa-vunjwa, lakini nawatakeni mfanye hivyo mtakapofika kwenye loji, ama hoteli zenu, ama po pote pale mnapokaa, ama nyumbani. Kusanyikeni na kujifunza jambo Hilo.

125 Wanamkosa kwa njia ambayo anayojifunua; kwa kuwa Yeye ni mkuu sana, hata hivyo, Yeye hujificha katika urahisi, apate kujijulisha kwa watu wa chini kabisa. Mnaona? Usijaribu kupata yaliyo makuu, kwa maana Yeye huyaruka hayo. Bali sikiliza urahisi wa Mungu, na ndipo unampata Mungu papa hapa katika njia rahisi.

126 Watu wenye akili nyingi, wenye hekima ya kilimwengu, walio na elimu, sikuzote humkosa. Sasa, mimi siko hapa . . . Nami ninajua kuna waalimu wa shule, wawili ama watatu, ninaowajua, wanaoketi hapa. Nami siko hapa kupinga shule na elimu, na kujaribu kuunga mkono kutojua kusoma. Siko hapa kwa ajili ya jambo hilo. Lakini, vile ilivyo ni kwamba, watu wameweka juhudi zao sana juu ya hilo mpaka wao wananinii, hata katika seminari na kadhalika, wanakosa jambo lenyewe hasa ambalo Mungu ameweka mbele zao.

127 Hiyo ndiyo sababu mimi siwapingi ndugu walio katika madhehebu, lakini ninapinga mfumo wa madhehebu, kwa maana unajaribu kujitukuza wenyewe, na—na—na kuwaelimisha wahudumu wake hivi *kwamba*, endapo, kama wao hawana elimu ya kutosha na kisomo, wanafukuzwa. Nao—nao hawana budi kupita mtihani wa kuchunguza mawazo, na kadhalika. Sijawahi kuwazia yalikuwa ni mapenzi ya Mungu kumhakiki mhuhumu kwa elimu ya mawazo, bali ni kumhakiki kwa Neno. Unaona? I—i—ingekuwa ni njia ya Mungu ya kumpa jaribio mtu Wake aliyemtuma, kuwa analo Neno.

128 "Hubiri Neno!" Sasa, siku hizi tunahubiri falsafa, tunahubiri kanuni ya imani na umadhehebu, na mambo mengi

sana, na kuliacha Neno, kwa sababu wao wanasema haliwezi kufahamika. Linaweza kufahamika. Yeye aliahidi kufanya jambo hilo. Sasa tunamwomba afanye jambo hilo.

129 Sasa tutachukua watu wachache hapa kwa dakika chache.

130 Hebu na tuone katika siku za Nuhu. Siku ya Nuhu, Mungu alipoona hekima ya ulimwengu ikiwekewa sana mkazo na kuheshimiwa, Yeye alituma ujumbe rahisi kwa mtu wa kawaida, apate kuwaonyesha ukuu Wake.

131 Sasa, tunajua ya kwamba katika siku ya—ya—ya Nuhu, wanadai ya kwamba ustaarabu ulikuwa wa hali ya juu sana, wakati huo, hata hatujafikia kiwango hicho bado, katika ustaarabu wetu wa kisasa. Nami ninaamini ya kwamba hatimaye kitafikiwa, kwa sababu Bwana wetu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika Kuja Kwake Mwana wa Adamu." Yeye alitoa mifano.

132 Nao walijenga piramidi na sfinksi kule Misri, nao walijenga madubwana makubwa mno ambayo hatuna uwezo, leo, ya kuyajenga. Walikuwa na da—da—dawa ya kuhifadhi maiti, hivi kwamba wangeweza kuuhifadhi mwili, kuufanya uonekane mzima kabisa hata unadumu mpaka leo. Sisi hatuwezi. Hatuwezi kutengeneza mumiani leo. Hatuna vitu vya kuutengenezea. Walikuwa na rangi ambazo—ambazo zinashika sana, kwa miaka elfu nne ama elfu tano iliyopita, zingali zinabaki rangi za namna ile ile tu zilivyokuwa. Unaona? Hatuna vitu kama hivyo leo.

133 Na mambo mengi makuu ya ustaarabu huo yanaonyesha umaarufu wake juu ya ustaarabu wetu wa kisasa. Na kwa hiyo unaweza kuwazia jinsi elimu na sayansi, kuhusu amana kuu tulizo nazo ulizoacha, kuonyesha ya kwamba kulikuwako na ustaarabu kama huo. Hapana budi huo ulikuwa ni u—ustaarabu mkuu sana, naam, kumbukumbu hizi, jinsi ambavyo sayansi na—na ustaarabu wa kisasa na elimu vilikuwa—vilikuwa ni vya lazima kwa hao watu. "Iliwabidi. Ilipaswa." Ilikuwa ni vigumu kabisa, nadhani, kumpata, ye yote asiyesoma kati yao, hata kidogo.

134 Na kwa hiyo, Mungu, akichunguza katika uchumi ule mkuu wa siku ile, katika taratibu zao, hakuweza, labda, kumpata mtu anayefaa, mpaka alipompata mtu asiye na elimu, labda, mkulima jina lake Nuhu, mchunga kondoo. Naye akampa ujumbe Wake apate kuwahubiria watu, ambao ulikuwa mrahisi sana, kwa nanii yao—kwa elimu yao ya siku hiyo, hata watu wakajikwaa katika urahisi wa ujumbe huo. Na, hata hivyo, huo ujumbe ulikuwa, mbele ya sayansi, "Wa kimapinduzi! Kungewezaje kuwe na mvua huko juu, wakati hakukuwako na mvua huko juu?" Unaona? Na ule ujumbe mrahisi wa—wa kujenga safina, kujenga kitu fulani cha kuingia humo, kwamba hakuna maji ya kuifanya ielee. Mbona, yeye amekuwa ni

mshupavu wa dini. Na akawa wa—wa—wa—wa . . . kile ambacho tungeita, kama mkiruhusu msemo wa siku hizi, "mtu wa kipekee."

135 Na karibu watu wote wa Mungu ni "watu wa kipekee," unaona. Wao ni watu wa kipekee. Nina furaha kuwa mmoja wao. Kwa hiyo, mnajua, wao—wao ni tofauti na—na mwelekeo wa sasa wa ustaarabu, kwa hiyo wanakuwa wa kipekee, wasio wa kawaida. Yeye alisema watu Wake walikuwa "Watu wateule, wa kipekee, wasio wa kawaida; lakini ukuhani wa kiroho, taifa la kifalme, wanaomtolea Mungu dhabihu za kiroho, matunda ya midomo yao, wakilisifu Jina Lake." Ni watu wa—wa ajabu jinsi gani! Yeye anao.

136 Na sasa, angalia, hapana budi hilo lilikuwa jambo kubwa katika siku hiyo, kwa mshupavu fulani wa dini kuja kanisani; mshupavu wa dini, na kuhubiri injili ambayo ilionekana imeruka mstari, kwa jinsi wao walivyoamini. Na wanasayansi, "Mbona, ili—ilikuwa ni wenda wazimu kabisa." Jinsi wangeweza kuthibitisha kisayansi hakukuwako na mvua kule!

137 Lakini huyu mchungaji wa kawaida wa kondoo aliamini, "Kama Mungu alisema itanyesha, itanyesha." Unaona?

138 Na kwa hiyo hebu linganisha tu jambo hilo na siku hizi, kuhusu mtu kuponywa. Wao husema, "Ni kuhamanika moyo tu. Ninaweza kuthibitisha kisayansi ya kwamba hiyo kansa, ama dutu lake, ama—ama—ama kitu hicho kingalipo." Lakini, kwa mwamini wa kawaida, imeondoka. Mnaona? Kwa sababu, yeye haangalii hilo dutu, anaangalia ahadi, kama vile vile tu alivyofanya Nuhu.

139 Hivi hamwoni, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika Kuja Kwake Mwana wa Adamu"?

140 Kisayansi, hakuna mtu . . . Daktari angeweza kusema, "Angalia hapa, uvimbe wako ungalipo. Kansa yako ipo. Mkono wako ungali umelemaa kama ulivyopata kuwa. Wewe una kichaa."

141 Na, kumbuka, hiyo ndiyo roho ile ile ya tokea zile siku za Nuhu, ambayo ilisema, "Hakuna mvua huko juu. Tunaweza kuulenga mwezi kwa vyombo, wala hakuna mvua kule." Lakini kama Mungu alisema kutakuwako na mvua kule!

142 "Kwa maana imani ni hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana." Nayo imani huchukua mahali pake pa mwisho pa kutulia juu ya Neno la Mungu. Hapo ndipo inapopata mahali pake pa kutulia. Mnaelewa? [Kusanyiko, "Amina."—Mh.] Mahali pake pa kutulia ni kwenye Neno la Mungu.

143 Hapo ndipo Nuhu alipoiweka, "Ndivyo Mungu alivyosema." Hilo lilitosha. Sasa kama ukiangalia tena, wakati huo, sasa, Nuhu, katika kuamini jambo hilo, alikuwa mshupavu wa dini.

144 Na watu wa leo wanaoamini katika ubatizo wa Roho Mtakatifu. Sasa, kanisa linasema, "Watu hawa ni washupavu wa dini. Si cho chote bali ni kundi la watu waliochochewa, wenye mwamsho, waliojaa woga mwingi." Lakini hawajui ya kwamba Neno la Mungu linafundisha jambo hilo. Ni ahadi.

145 Na, kwa Nuhu, haidhuru walisema mangapi, "Mzee huyu amerukwa na akili; ya kwamba alikuwa amekosea kulingana na sayansi; na—na—na, kimawazo, alikosea." Lakini, kwa Nuhu, lilikuwa ni Neno la Bwana, naye Nuhu alidumu nalo. Nao wenye hekima na akili wakajikwaa juu ya urahisi wake, na kupoteza maisha yao. Ni ke—ke—kemeo la jinsi gani sasa, lilivyo, kwa kizazi kile!

146 Watu wengi wanasema, "Laiti ningaliishi zama zile!" La, ungalichukua msimamo ule ule. Kwa sababu, leo, katika jambo lile lile likitendeka tena leo, ila tu katika namna nyingine, wao wanajikwaa kwenye Hilo leo kama tu walivyokwazwa wakati huo.

147 Hapana shaka, katika siku hizo, walikuwa na wahubiri wengi sana, lakini Nuhu alikuwa ametiwa upako na Mungu. Naye Nuhu angaliweza kuangalia huko nje na kuona yale yaliyokuwa yanakaribia kutukia, na kujua ya kwamba kizazi kizinifu na kiovu, kama hicho, ya kwamba Mungu hangeweza kukiacha kiendelee. Kwa hiyo tunaweza kufanya nini, leo, ila kuona jambo lile lile! Sodoma na Gomora ya kisasa, unaona, watu waovu, wazinzi, waliosoma sana hivi kwamba wanajikwaa katika urahisi wa madhihirisho ya Mungu ya Utu Wake na Neno Lake, akionyesha Neno Lake.

148 Hakuna mtu duniani, Rosella, ambaye . . . ama, na—na anayeweza kusema ya kwamba—ya kwamba hatuoni Neno lile lile la Mungu likidhihirishwa kati yetu. Ahadi ile ile ya siku za mwisho, Nuru zile zile za jioni zilizopaswa kuangaza, sisi ni watu waliotunukiwa kuona jambo hilo. Na, ambapo, ulimwengu uliosoma sana, limefichwa kwao. Yesu alimwambia Mungu, Baba, alisema, "Ilikupendeza kuwaficha. Hata hivyo, Baba, Wewe umelificha." Waache, na hekima yao . . .

149 Unaona, hekima ndiyo iliyofanya jambo lote kuanza kuvingirika katika kinyaa cha dhambi, hapo mwanzo; kwa maana Hawa alikuwa akitafuta hekima wakati alipokutana na Shetani, naye Shetani akaimpa, unaona. Na hekima ni kinyume cha Neno. Hatutakiwi kuwa na hekima. Tunatakiwa kuamini yale yaliyokwisha kusemwa. Kwa hiyo, unaona? Lakini, leo, wanachuoni wanaliwekea elimu hivi kwamba, na kuliweka kule, na kuweka tafsiri yao wenyewe Kwake, wamefanya hivyo daima. Wanafanya jambo lile lile leo; ni katika kipimo kile kile. Sasa, watu, lakini ninii . . .

150 Ama, watu basi walilikosa, kama vile tu wanavyolikosa na kufanya hivyo leo. Jambo lile lile. Wanafanya jambo lile lile. Kwa

kuwa, wao. . .Sababu ya wao kulikosa, ni kwamba walikuwa wenye akili sana kuweza kuliamini. Unaona? Sasa, ujumbe wenyewe ulikuwa ni rahisi sana, hivi kwamba watu werevu walikuwa ni werevu mno kuamini urahisi wa huo ujumbe. Loo! jamani! Mungu aliufanya rahisi sana, katika Kweli, hivi kwamba watu werevu na wenye akili walishindwa kuuona, kwa maana ulikuwa ni rahisi sana. Naam, hilo ndilo linaloufanya ukuu wa Mungu kuwa mkuu hivyo; kwa sababu, Yeye akiwa ni mkuu kuliko wote, anaweza kujifanya rahisi.

151 Wanadamu leo, wakionyesha ya kwamba wao si wa Mungu, eti wao ni wakuu na wanajaribu kujifanya wakuu zaidi, na kujionyesha kwamba ni wakuu zaidi, na, "Askofu mkuu, Daktari Papa Mtakatifu," kila kitu, wakijifanya wao ni kitu fulani ambacho kwa kweli hawako hivyo. Naye Mungu, akiwa ni mkuu hivi, anajishusha kwa urahisi. Urahisi ni ukuu.

152 Tunaweza kutengeneza ndege aina ya jeti, tunaweza kutupa roketi kwenye. . .kwenye. . .ama kutupa ko—ko—kombora kwenye obiti. Nasi tunaweza kufanya mambo yote haya, hata hivyo, lakini hatuwezi kutengeneza jani hata moja. A-ha. Amina. Mnaonaje hilo? Lakini badala ya kujaribu kurudi na kuona ni kitu gani kitengenezacho jani hilo, na kumkubali Mungu Mwenyewe aliyeumba unyasi ule, tunajaribu kuunda kombora litakalofika kule haraka zaidi ya mwingine awezavyo kuunda lingine. Mnaona?

153 Sisi ni werevu sana na wenye akili nyingi, makanisani mwetu, hata tunaweza kujenga jengo la dola milioni moja, ama jengo la dola milioni kumi, lakini, hata hivyo, na kujaribu kujenga moja lililo bora kuliko la Wamethodisti, ama Wabatisti wanajenga moja bora zaidi kuliko la Wapresbiteri, na Wapentekoste wameingia katika mashindano haya yasiyo na mwanzo wala mwisho. Lakini jambo lenyewe ni kwamba, ni hili; sisi ni, hata hivyo, sisi ni werevu sana na tumeshikilia njia zetu sana hata tunashindwa kujinyenyekeza kumtambua Mungu aliye kwenye misheni ndogo pale pembeni. Mnaona? Hiyo ni kweli. Vema, hiyo ni kusema, tunajikwaa kwenye urahisi. Wamefanya hivyo daima.

154 Sasa, wao, walikuwa—walikuwa werevu sana wasingeweza kuamini ujumbe rahisi kama huo. Haukuwa sanifu vya kutosha kwa utafiti wao wa kisayansi waliokuwa nao. Haukuwa—haukuwa sanifu, ujumbe huo haukutosha, kwa ajili ya mipango yao ya elimu waliyokuwa nayo siku hiyo. Unaona? Walikuwa wamesoma kujua ya kwamba kulikuwako na Mungu, nao walisoma kujua ya kwamba Yeye alikuwa ni mkuu, nao wakajaribu kujijenga wawe wakuu kama Yeye. Ambapo, njia ya kupanda juu daima ni kushuka.

155 Sasa, ni nani anayejua kama Ncha ya Kaskazini ni Kaskazini, ama Ncha ya Kusini ndio Kaskazini? ama Ncha

ya Kaskazini ni Kusini, Ncha ya Kusini ni Kaskazini? Ni upande gani ulio juu na ni upi ulio chini? Tunaning'inia angani. Tunasema, "Ncha ya Kaskazini ni upande wa juu." Mnajuaje? Ncha ya Kusini huenda ikawa upande wa Kaskazini. Mnaona, hujui. Kwa hiyo hebu na tukumbuke, na Neno hili . . .

156 Ungesema, "Basi ungewezaje kusema, Ndugu Branham, ya kwamba, 'Juu ni chini'?"

157 Juu ya msingi wa Neno la Yesu Kristo! Yeye alisema, "Yeye ajidhiliye atakwezwa, bali yeye ajikwezaye atadhiliwa, atashushwa." Kwa hiyo basi, kwa kweli, juu ni chini, na chini ni juu.

158 Kama yule mtakatifu wa zamani alivyosema huko Chicago, ya kwamba . . . Mtu fulani, mhudumu fulani kutoka katika madhehebu fulani, aliinuka katikati ya Wapentekoste. Alikuwa amekusanya mambo yake yote ya kielimu. Alipanda akaenda kule na kutumia maneno ambayo Wapentekoste hawakujua kitu cho chote juu yake, naye akapanda akaenda kule, ndipo akaona wale Wapentekoste hawakuwa wanayaelewa. Basi akapanda juu, kifua mbele, naye alikuwa "Mtakatifu Daktari *Fulani*," mwajua, kutoka shule *fulani* kubwa kule Chicago. Basi akaangalia pande zote, nao hao Wapentekoste walikuwa wanatazamana. Hata hawakujua alichokuwa anasema; alikuwa na elimu nyingi sana, mwerevu sana, mwenye akili. Hawakujua.

159 Ilikuwa kitu kama mbunge fulani, ama mtu ambaye alipigiwa kura siku za karibuni awe raisi lakini akashindwa. Tuck Coots aliniambia. Nilipokuwa nikihubiri kwenye mazishi ya Mama Ford, nami nilikuwa nikihubiri juu ya ufufuo, uhakika wa kufufuka, "Kwa hakika tu kama vile jua linavyochomoza, vivyo hivyo nami nitafufuka. Kwa hakika tu kama vile nyasi zinavyokufa katika msimu wa Kupukutika Majani, na jani linaanguka kutoka mtini, linarudi tena. Wakati dunia inapojiratibisha katika mzunguko wake, halina budi kufufuka tena."

160 Tuck akasema, "Nilifurahia Ujumbe huo, Billy." Mimi pamoja na Ndugu Neville tulikuwa tumeketi pamoja kwenye gari. Ndipo nikasema, "Tuck . . . " Yeye akasema, "Mimi hufurahia Jumbe zako."

Nikasema, "Tuck, mimi sina elimu," nikasema.

Akasema, "Huo ndio uzuri wake." Unaona?

161 Na, sasa, yeye alisema alienda kumwona . . . Vema, nadhani mtu huyo atanisamehe, simaanishi . . . Adlai Stevenson, mwajua. Naye alisema alimsikiliza kwa dakika kumi na tano. Naye Bw. Stevenson ni mnenaji mwenye akili nyingi sana, watu wanaamini hivyo, mwajua, mpaka Tuck akasema . . . Nadhani ana elimu ya chuoni. Akasema aliketi pale na akalala usingizi. Na akasema aliingia usingizini, akiwa anamsikiliza, katika dakika kumi na tano. Lakini akasema, "Akiwa na elimu ya

chuoni, sikuelewa ila maneno machache tu aliyosema; yalikuwa yenye ufasaha sana." Akasema, "Hujaniona hata kidogo nikilala katika moja ya ibada zako, sivyo, Ndugu Branham?"

162 Kwa hiyo, unaona, ni ule urahisi Wake, ni rahisi sana, hapo ndipo Mungu alipo.

163 Sasa, wao—wao walikuwa werevu sana, katika siku hiyo, hata hawangeweza kufahamu maana ya njia rahisi ya Mungu ya kufanya mambo. Haikuwa ya kielimu kwao. Haina budi kuwa ya elimu sana, haina budi kuwa imeng'arishwa sana, vinginevyo wataikosa. Sasa, lakini, yule Yehova mkuu alikuwa amefichwa katika Neno Lake. Naye alijijulisha kwa watu walioliamini Neno Lake, kwa kuwaokoa, na kuutimiza ujumbe rahisi. Ule ujumbe rahisi wa Nuhu, Mungu aliutimiza. Sasa angalia jambo hilo.

164 Sasa, basi, tena katika siku za Musa, angalia wakati mwingine wa ukombozi.

165 Wakati Mungu anapokaribia tu kufanya jambo fulani kuwakomboa watu Wake, Mungu huwatumia hao watu Ujumbe. Na, Huo huwa rahisi sana, kama tutakavyoona katika kuvunjwa kwa Mihuri hii. Hilo ndilo lililokuwa kusudi langu la kulileta hili kwanza. Ya kwamba, tunaona ya kwamba kuvunjwa kwa Mihuri hiyo ni rahisi mno, wenye—wenye—wenye akili wanalikosa Hilo, maili milioni moja. Unaona? Natumaini ya kwamba Mungu atanitia mafuta kwa ajili ya jambo Hilo. Unaona? Unaona? Linapitia tu juu yao. Na hiyo ndiyo sababu nilifikiri Ujumbe huu, asubuhi hii ya leo, ungefaa, ili kuweka msingi, juu ya urahisi wa Mungu, unaona, jinsi Mungu anavyojificha katika urahisi.

166 Hebu wazia, wao wanaweza kuvunja atomi na kufanya cho chote kile; lakini inapofikia kwenye kugusa uhai, hata hawawezi kukwambia unakotoka. Unyasi wa kawaida, na Mungu amejificha ndani yake. Wanaweza kutupa roketi mwezini, na—na kutupa rada kule juu, ama cho chote kile, na hata hivyo hawawezi kuelezea uhai ulio katika unyasi. Hiyo ni kweli. Mnaona? Ni kwa sababu huo hauwezi kuelezewa. Ni rahisi sana, wanalipuuza hilo.

167 Sasa angalia Musa, katika siku ambayo Mungu alikuwa anaenda kuwakomboa wana wa Israeli, kulingana na Neno Lake. Yeye, Yeye alifanya nini? Alichagua jamaa ya kawaida. Hatuna kumbukumbu yao. Unaona, yote tujuayo tu ni, "mwana wa Lawi". Mnaona? Na kwa hiyo sisi . . . na mke wake. Wa kawaida tu, labda m—mkanyaga matope, vile ambavyo ulimwengu ungefikiria, huko nje wakiwafyatulia adui matofali. Yeye alikuwa mtumwa wa kawaida tu katika Israeli, lakini Mungu aliichagua jamaa ile kumleta mkombozi; jamaa ya kawaida tu ya Kiyahudi. Yeye kamwe hakuondoka akaenda na kuchukua watu wa jamaa ya mfalme ama watu maarufu, ama cho chote kile, ama hata kumchukua kuhani fulani. Alichukua jamaa ya kawaida,

jamaa ya kawaida. Unaona? Urahisi! Angalia alichofanya, basi, Yeye alimzaa mwana, mwanadamu duni. Yeye kamwe . . .

168 Angeweza ku—angeweza kuchagua jua, kama angalitaka kufanya jambo hilo, kuwaokoa. Angeweza kuchagua upepo kuwakomboa. Angeweza kumchagua Malaika kuwakomboa. Loo! haleluya! Mungu anaweza kufanya lo lote analotaka kufanya.

"Vema, unajuaje jambo hilo, Ndugu Branham?"

169 Mungu hataacha mpango Wake. Hiyo ndiyo sababu tunajua ya kwamba, siku hii ya leo, halina budi kuwa rahisi. Unaona? Sasa, Yeye daima hutenda kazi katika urahisi. Lakini Mungu, hapo mwanzo, ambaye angeweza kulifanya jua lihubiri Injili, ama pepo zihubiri Injili, ama Malaika ahubiri Injili, bali Yeye aliwachagua watu kwa kusudi hilo, Naye habadilishi jambo hilo hata kidogo. Yeye hakuchagua katika . . . Hakuyachagua madhehebu kamwe. Hakuchagua kamwe makundi ya watu. Aliwachagua binadamu wahubiri Injili; si mitambo, vitu vya kimitambo, au Kiumbe cho chote cha Kimalaika. Ilikuwa ni mwanadamu!

170 Na wakati alipowaletea watu ukombozi kule chini, alimtuma mwanadamu wa kawaida, aliyezaliwa na jamaa ya kawaida katika kundi la watumwa. Loo, jamani! Yeye ni Mungu wa jinsi gani, akijifunua katika urahisi!

171 Sasa angalia. Naye alimfundisha katika hekima ya kilimwengu, ili kwamba apate kushindwa, na aonyeshe ya kwamba hatutakombolewa kamwe na hekima. Tunakombolewa kwa imani. Alimwachia aende akapate elimu nyingi sana hivi kwamba aliweza kuwafundisha Wamisri hekima; alikuwa mwerevu sana. Mungu alikuwa na jamaa hiyo ya kawaida ambao hawangeweza, labda, kuandika jina lao. Naye Musa alichukuliwa akapelekwa katika kisomo kilichozidi kisomo chote, akapata elimu nyingi sana, hata angeweza kuwafundisha hekima waalimu. Aliweza kuwafundisha watu walio na bongo kupita kiasi. Naam. Na Mungu akamwacha awe hivyo kusudi aweze kujionyesha Mwenyewe katika unyenyekevu, apate kuonyesha ya kwamba hekima haina uhusiano wo wote na jambo hilo. Naye Musa alishindwa kwa aibu katika akili zake nyingi sana. Yeye alimwacha awe namna hiyo kwa ajili ya kusudi Lake, ili kwamba apate kushindwa. Naye alishindwa, na akaanguka.

172 Kwa hiyo, ili kuonyesha, "Si kwa uweza, wala si kwa nguvu," lakini si kwa hekima ya Misri, wala si kwa hekima ya shule zetu, wala kwa nguvu za seminari zetu, lakini si kwa wingi wa madhehebu yetu, wala si kwa nguvu za mafundisho yetu ya kielimu, "bali ni kwa Roho Yangu, asema Mungu." Hekima Yake yake ilikwisha, na kufikia mwisho wake, wakati alipokutana na Mungu katika kile kijiti kilichowaka moto pale. Alivua viatu

vyake na kujinyenyekeza mwenyewe katika unyenyekevu, na akasahau yote yanayohusu hekima yake.

173 Mungu, akileta ukombozi, ilimbidi amfundishe hekima, kumwacha aanguke, kuonyesha ya kwamba huwezi kutegemea mkono wa akili zako mwenyewe, ama akili za mtu mwingine ye yote. Akaacha aanguke, apate kuonyesha mkono Wake. Unaweza kuona jambo hilo? [Kusanyiko, “Amina.”—Mh.] Kusudi la Mungu katika kufanya jambo hilo, lilikuwa ni kujionyesha Mwenyewe katika unyenyekevu. Naye alimwachia Musa ainuke juu sana kuliko wote, mpaka yeye ange—angekuwa Farao anayefuata. Yeye alikuwa jemadari hodari. Kulingana na historia, alishinda, Musa mwenyewe, nchi jirani. Ndipo wakati alipoigeukia kazi ya Bwana, na yote aliyojaliwa nayo, Mungu alimwacha aanguke vibaya sana, kusudi aweze kumweka nje kule jangwani na kumwondolea hayo yote; ndipo amtokee, katika unyenyekevu, na kumtuma ashuke kule na fimbo mkononi mwake, kuwakomboa wale watu.

174 Wakati, yeye hangeweza kufanya jambo hilo kwa mafunzo ya kijeshi, kwa elimu, kwa elimu ya kisayansi. Na kwa nguvu za kijeshi hangeweza kufanya jambo hilo. Ndipo akampa fimbo ya zamani iliyopinda kutoka jangwani, na akawakomboa kwa kumtumia yeye. Mungu katika unyenyekevu, urahisi! Mungu alikuwa ndani ya ile fimbo na ndani ya Musa. Na alimradi tu Musa alikuwa na ile fimbo, basi Mungu alikuwa nayo, kwa sababu Mungu alikuwa ndani ya Musa. Hakika.

175 Angalia, “Si kwa uweza, wala si kwa—kwa nguvu, bali ni kwa Roho Yangu.” Lakini ni kwa imani rahisi!

176 Musa alifahamu ya kwamba alikuwa awe mkombozi, kutokana na mafundisho ya mama yake. Ndipo akajipa mazoezi katika nguvu za kijeshi, kwa madhumuni ya kufanya jambo hilo, lakini ilishindikana. Unaona? Yeye alikuwa na akili, na alikuwa na elimu, lakini hilo halikufaa kitu. Kwa hiyo ilimbidi kusahau hayo yote, na aje kwenye jambo rahisi la kumchukua Mungu kwenye Neno Lake, na ndipo akawakomboa hao watu. Naam, bwana.

177 Mungu hukomboa kwa (kitu gani?) imani katika Neno Lake. Daima imekuwa hivyo. Tungeangalia kama tungalikuwa na wakati. Bado tuna kama dakika ishirini na kitu. Tulikuwa . . .

178 Tungeweza ku—kumwangalia Kaini na Habili, jinsi ambavyo—ambavyo Kaini alijaribu kumpendeza Mungu kwa uzuri fulani.

179 Njia nyingine, watu wanafikiri, “Kwa—kwa makusanyiko makubwa, yaliyovalia vizuri, kwa kasisi aliye na—aliye na . . . wahudumu wenye majoho, na kwaya zilizovalia majoho, na ninii yote—vitu vya kuvalia, eti hivyo vinampendeza Mungu.” Unaweza kuona vinakotoka? Kaini alijaribu kitu kile kile. Naye

akamjengea madhabahu, hapana shaka kwamba aliifanya ya kupendeza.

180 Na mtu huyo alikuwa mwaminifu. Aliabudu. Aliwazia, "Mradi tu mimi ni mwaminifu, haileti tofauti yo yote." Inaleta tofauti. Unaweza kuwa mwaminifu makosani.

181 Angalia, yeye—yeye alijenga madhabahu hii naye, namna hiyo, akaweka maua na kuyapamba vizuri, na kuweka matunda mazuri, kisha akawazia, "Hakika, Mungu mkuu, mtakatifu, msafi, na mzuri ataikubali dhabihu hiyo." Lakini, unaona, alifanya jambo hilo kwa hekima yake mwenyewe. Alifanya hivyo kwa mawazo yake mwenyewe.

182 Na hivyo ndivyo ilivyo leo. Yeye—yeye . . . Wanafanya jambo hilo kwa hekima yao wenyewe, kwa kisomo chao, kwa elimu yao na maadili ambayo wamejifunza.

183 "Lakini Habili, kwa ufunuo, kwa imani, alimtolea Mungu dhabihu iliyo bora zaidi." Haina cha usafi wo wote, kadiri ilivyoonekana, tukinena kibinadamu. Maskini jamaa huyo, naye akimshika kwa nguvu shingoni na kumfunga kwa mzabibu, namna *hiyo*, na kumkokota kwenda kwenye madhabahu hii. Hapakuwapo na uzuri wo wote sana kwenye jambo hilo. Akimweka juu ya madhabahu, na kukata koo lake dogo kwa—kwa mwamba mkali, mpaka damu yake ikamrukia kila mahali, naye huku analia, akifa. Lilikuwa ni tamasha la kutisha, unaona, kuliona. Lilikuwa ni jambo rahisi, hata hivyo.

184 Kwa urahisi, yeye alijua ya kwamba alizaliwa kwa damu ya mama yake na baba yake, alizaliwa katika damu ya mama yake, kwa damu ya baba yake; na ilikuwa ni damu ambayo ndiyo ilisababisha kule kuanguka, kwa hiyo damu ndiyo ambayo ingelirudisha hilo. "Kwa hiyo akamtolea Mungu dhabihu iliyo bora zaidi, kwa maana ilifunuliwa kwake."

185 Na baadhi ya ndugu, leo, wanaofikiri ya kwamba walikula matofaa na mapera! Nami niliona jambo la kiwenda wazimu kabisa hivi majuzi, gazetini. Walisema, "Sasa wamethibitisha ya kwamba Hawa hakula tofaa." Kwamba, na—nafikiri wanadai, "Ilikuwa ni aprikoti." Kwa hiyo, loo! unaona mahali roho hiyo inakotoka!

186 Nao walisema, ya kwamba, "Musa hakuvuka hasa Bahari ya Shamu. Ya kwamba, ilikuwa ni ki—kichaka cha matete sehemu zile, bahari ya matete. Naye aliwapitisha wana wa Israeli katika bahari ya manyasi. Huko mwishoni mwa—mwa bahari, kuna kichaka kikubwa cha matete huko. Naye Musa alivuka bahari. Lakini ilikuwa ni bahari ya matete ambayo alivuka; mwajua, nyasi, ndefu, kama manyasi makubwa na kadhalika, ambayo alivuka pale." Ni upuuzi jinsi gani!

187 Wakati, "Hayo maji," Biblia ilisema, "yaligawanyika kutoka kushoto kwenda kulia, na Mungu akasababisha upepo wa—wa nguvu utokao mashariki kuyagawanya." Unaona? Unaona?

188 Wao, wanataka kujaribu kuliwazia katika njia yao wenyewe. Na hivyo ndivyo jinsi walivyoshindwa siku zote, nao wataendelea kushindwa. Wajua, mambo haya yote!

189 Naye Kaini alikuwa mfano halisi wa mtu wa nia ya kimwili leo, ambaye ni mcha Mungu kwa nje. Anataka kufanya jambo fulani kwa nje, lakini yeye ni . . . Anaenda kanisani, na—na atafanya mambo mengi sana kwa ajili ya—ya jengo.

Kuna Kanisa moja tu, na hujiungi na Hilo.

190 Haya ni maloji. Mnaona? Unajiunga na loji la Kimethodisti, loji la Kibatisti, loji la Kipresbiteri, loji la Kipentekoste.

Lakini unazaliwa katika Kanisa. Naam, bwana. Unaona?

191 Haya yote ni maloji. Si makanisa. Ni maloji. Wala hakuna kitu kama "kanisa" la Kimethodisti, ama "kanisa" la Kipentekoste. La, hakuna kitu kama hicho. La, hayo yote ni makosa. Unaona? Hayo ni . . . Hiyo ni kweli. Hayo, hayo ni maloji ambayo watu wanajiunga nayo.

192 Lakini unazaliwa katika Kanisa la Mungu aliye hai, na hilo ni mwili wa Mungu wa Yesu Kristo unaoundwa.

193 Sasa, lakini, ilimpendeza Mungu kumfunulia Habili siri Yake, kwa imani nyofu katika damu iliyomwagika. Loo! laiti ningalikuwa na wakati wa kuelezea hilo kwa muda mrefu kidogo. Unaona?

194 Hata hivyo, naye Kaini, na hekima yake yote, mtu mwerevu! "Loo!" unasema, "sasa, Ndugu Branham, ulisema yeye . . . Unajaribu kumfanya kuwa msomi wa bongo za kupindukia?" Alikuwa hivyo. Ati alikuwa mwerevu? Fuatilia ninii yake—fuatilia ukoo wake. Angalia watoto wake. Wote walikuwa ni wanasayansi, na madaktari, na watu werevu, kila mmoja.

195 Bali, hebu fuatilia uzao wa Sethi, walikuwa ni wanyenyekevu, wakulima wadogo-wadogo, na wakulima, na kadhalika, na kuendelea hata kwenye yale maangamizi.

196 Lakini watoto wa Kaini walikuwa ni werevu, kundi lenye elimu. Hata wao, wanadai, waliweza kufua shaba nyekundu, na hufua vyuma; na ni wajenzi. Nao walikuwa ni watu werevu.

197 Ambapo—ambapo, watu hawa wengine waliishi tu kwenye mahema, na kuchunga kondoo wao, na kusimama kwenye ahadi za Mungu. Unaona? Unaona? Unaona jinsi ilivyokuwa? Sasa hebu wewe fuatilia tu hivyo vizazi vyao toka mwanzo hadi mwisho, uone kama jambo hilo si kweli. Unaona? Walidumu kwenye ahadi ya Mungu.

198 Hivyo ndivyo Nuhu alivyochaguliwa, kutoka katika watu wa namna hiyo. Hivyo ndivyo Paulo alivyotolewa kutoka katika kundi lake. Unaona? Hivyo ndivyo John Wesley, Martin Luther, na kadhalika. Hivyo ndivyo unavyokuja kuwa wewe leo hii,

unaona, kitu kile kile, mnyenyekevu, kuamini ahadi rahisi ya Mungu.

199 Sasa, angalia, ilimpendeza Mungu ku—kujitambulisha. Sasa, Mungu daima atathibitisha kama ni Kweli ama si kweli. Unaona? Sasa, watu wengi wanajaribu kujiingiza kwenye kitu fulani ambacho Mungu yuko umbali wa maili milioni moja nacho. Hiyo ni kweli. Lakini unapomwona Mungu akirudi hapo, aseme ni . . . analiitikia, anasema, "*Hilo* ni kweli, *Hilo* ni kweli, *Hilo* ni kweli," basi unajua Hilo ni kweli.

200 Sasa, wakati matoleo yalipokuwa kwenye ile madhabahu, Mungu alikataa wazo lake la kiakili la Mungu. Lakini wakati alipomwona Habili, kwa imani rahisi ya kuamini kwamba hayakuwa ni matofaa wala matunda ya shambani, lakini ilikuwa ni damu; kwa imani aliamini hilo, kwa ufunuo kutoka kwa Mungu. Mungu alimthibitisha Adamu kwa kukubali sadaka yake. Unaona?

201 Hapo ndipo tunapofikiria juu ya kuwaombea wagonjwa, cho chote kile. Yesu alisema, "Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu likae ndani yenu, ombeni tu mtakalo nanyi mtapewa."

202 Sasa tunapomalizia moja kwa moja, upesi sasa, tumebakiza dakika ishirini.

203 Angalia, siku za Eliya, Mungu alichagua kujificha katika mtu wa kawaida. Sasa hebu wazia tu jambo hilo. Mungu alichagua. Hilo lilikuwa ni chaguo Lake. Kumbuka, walikuwa na marabi, makuhani. Walikuwa na watu mashuhuri katika siku hizo. Hata Mfalme Ahabu, mwenyewe, alikuwa Myahudi. Alikuwa na watu mashuhuri nchini, katika siku hizo. Lakini Mungu alijificha katika mtu rahisi; si msomi; la, si mtu aliyetukuka wa dunia, mwanajeshi fulani hodari sana ama kitu fulani; la, si jina kubwa. Hata hatujui baba yake na mama yake walikuwa ni nani. Hatujui kitu kuhusu ukoo wake. Ni mzee mkulima tu wa kawaida mahali fulani, aliyeinuliwa kusudi awe nabii. Mungu alimfanya kuishi peke yake huko jangwani. Jambo pekee tunalojua, yeye alitokea tu mahali pasipojulikana, akaingia na moja kwa moja akaukemea utaratibu wote wa kidini. Jamani!

204 Na unajua vile walivyomfikiria? "Alitokea kwenye shule gani?" Unaona? "Yeye ni wa madhehebu gani? Yeye yuko pamoja na Mafarisayo, Masadukayo," ama wo wote wale wengine waliokuwa nao? Yeye hakuwa mmoja wao, lakini alilikemea jambo hilo lote. Unaona? Mungu alichagua kufanya hilo.

205 Lakini, mtu wa kawaida, hana elimu. Hatuna mahali ambapo alipata kwenda shuleni. Hatuna habari zo zote zake. Ni mtu wa kawaida tu, lakini Mungu alipendezwa kujificha katika mtu huyo mnyofu. Mungu, kule nyuma, akiwa na mtu huyu mnyofu, akijificha katika mwanadamu. Unaweza kulielewa jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

206 Mungu akijificha katika "mtu wa kipekeepekee asiye na elimu," kwa ulimwengu. Maana, mwajua, wao—wao walimnenea kila kitu, hata ya kuwa ni "mchawi," Eliya. Manabii wote wanasemwa, jambo hilo, unaona.

207 Kwa hiyo, Yesu alisemwa kuwa ni mchawi, unaona, "Beelzebuli; kuwa mwenye kichaa." Kasema, "Mbona, Wewe ni mwenda wazimu. Naam, tunajua una pepo. Wewe—wewe umerukwa na akili." Unaona?

208 Hapo ndipo alipowaambia, "Wakati itakapofikia siku za mwisho, ya kwamba wao wanaku-. . .hilo lingekuwa ni kukufuru, kufanya jambo hilo." Aliwasamehe, lakini halitasamehewa katika siku hizi za mwisho. Litabidi kulipiwa, kwa kutengwa Milele, "Wala kamwe halitasamehewa, katika ulimwengu huu wala ulimwengu ule ujao."

209 Lakini walimchukulia Eliya kuwa ni mwenda wazimu. Ungeweza kuwazia akiwakabili. . .Hao—hao wanawake wote walikuwa wakikata nywele zao kama siku hizi, naona, na kujipodoa kama Yezebeli, bibi wa rais nchini. Na—na wahubiri wote wamekuwa wa kilimwengu na kila kitu. Na halafu ni kitu gani kilitokea? Ndipo hapa akaja mzee Eliya, akikaripia jambo zima, kuanzia Yezebeli kwenda chini.

210 "Mbona," akawazia, "si lazima tukusikilize! Sisi tuna wachungaji."

211 Hakika, haikuwalazimu kumsikiliza, lakini alikuwa ni mchungaji wao hata hivyo. Alikuwa ni mchungaji wa Yezebeli. Yezebeli hakutaka jambo hilo. Huenda alikuwa na wa aina nyingine. Lakini, lakini, Eliya alitumwa na Mungu. Mnaona? Alikuwa ni mchungaji aliyetumwa na Mungu kwa ajili yake. Alimchukia, bali alikuwa mchungaji hata hivyo. Angalia.

212 Naye Eliya alijinyenyekeza na kudumu na yale Mungu aliyosema, hivi kwamba, ilimpendeza Mungu kuchukua Roho hiyo hiyo kutoka kwa Eliya na kuahidi kuisukuma tena mara tatu katika siku zijazo tangu wakati huo. Unaona? Amina. Na alifanya jambo hilo. Amina. Hakika, alilifanya. Hakika. Aliahidi jambo Hilo, ya kwamba Hiyo ingekuja. Nayo ikaja juu ya Elisha, aliyemfuata; kisha ikaja juu ya Yohana Mbatizaji; na, kulingana na Malaki 4, inapaswa kuwa hapa tena katika siku za mwisho. Mnaona?

213 Mungu aliipenda Roho hiyo iliyokuwa juu ya mtu huyo mnyofu, asiyekuwa na elimu, mtu anayeishi mwituni aliyetokea huko msituni ndani ndani mahali fulani. Na, kwa hiyo, ilikuwa ni mtiifu sana kwa Neno Lake, hata angeweza kusema, "Eliya, fanya *hivi*," naye Eliya angelifanya hivyo. Na Mungu akajificha mle ndani, katika urahisi sana!

214 Wote walimsema, "Yule mzee mwenda wazimu, msiwe na uhusiano wo wote naye," na kadhalika.

215 Lakini siku moja, wakati yeye a—alipokuwa mzee, na kichwa chake kina upara, na ninii yake—na masharubu yake yakining'inia, yenye mvi, na nywele chache alizokuwa nazo zikining'inia mabegani mwake; maskini mikono ya kizee iliyokonda, na nyama zilizotepwereka namna hiyo; anashuka akija barabarani akienda zake Samaria, na hayo macho yakiangalia juu mbinguni, akiwa na fimbo iliyopindika mkononi mwake. Hakuwa mtu wa kutamanika ukimwangalia, lakini alikuwa na "BWANA ASEMA HIVI" kwa ajili ya siku hiyo. Hakusitasita na Hiyo. Hakusema kwa kitata. Yeye hakusema, "Sasa, ewe *mtukufu* Ahabu." Alitembea kupanda juu na kusema, "Hata umande hautaanguka kutoka mbinguni mpaka nitakapouagiza." Haleluya! Unaona? Mungu aliheshimu unyofu wake.

216 Sasa, unaona, wakati ilipokuwa ni katika njia rahisi, na kila mtu—kila mtu anampinga, kila mtu alimkabili. Shirika lote la wahudumu, cho chote kile, kilimkabili, hiyo ni kweli, wakijaribu kumwondosha, cho chote kile. Lakini, katika urahisi huo, ingawa hawakuwa na ushirikiaano na mikutano yake na yo yote yale zaidi aliyokuwa nayo. Kila mtu alifikiri alikuwa mwenda wazimu. Mungu alikuwa akijificha.

217 Lakini wakati ulipofikia kwa ile mbegu kukomaa, ambayo ilikuwa imepandwa, Mungu alijidhihirisha Mwenyewe kwa kutuma Moto kutoka Mbinguni na kuilamba ile dhabihu. Mungu akijificha katika urahisi, halafu akijifunua Mwenyewe tena. Unaona? Hakika. Ilimpendeza Mungu kufanya jambo hilo. Yeye daima ametenda kwa jinsi hiyo. Naam, bwana. Sasa, tunaona ya kwamba Yeye—Yeye aliahidi mambo haya.

218 Shida ni kwamba, leo, kwa walio wengi wetu sisi watu, tunataka kuwa wa ninii, mwajua, kuwa wa kiseminari sana, na wa kimadhehebu, wenye nia ya kielimu, hivi kwamba Mungu hawezi kututumia. Mungu anaweza kumpa mtu uwezo wa kuanza jambo fulani, na kumpa huduma fulani; muda si muda wajua, yeye ataanza kushughulikia yale watu wengine wasemayo, na, muda si muda wajua, atakuwa amefungwa kabisa katika upuuzi fulani mkubwa. Na ndipo Mungu anaondoa tu mikono Yake kutoka kwake, na kumwacha peke yake. Unaona? Unaona?

219 Ndipo atajaribu kujipatia mtu mwingine, mtu fulani atakayefanya jambo hilo. Unaona? Hana budi kupata kitu ambacho kitaninii—kitachukua Neno Lake, kitachukua ufunuo wa Mungu na hataondokana nao, atadumu imara na Neno hilo. Hivyo ndivyo Yeye a—anavyofanya jambo hilo. Yeye amelifanya hivyo daima.

220 Kwa hiyo wakati mtu anapopata elimu nyingi sana na ni mwerevu, hata, yeye hujaribu kuweka tafsiri yake mwenyewe. Vema, kama wanavyosema, "Ubatizo wa Roho Mtakatifu,"

watasema, "loo! huo ulikuwa wa siku za huko nyuma." Lakini, kama hawasemi hivyo, vema, "Haukuwa wa siku za zamani, lakini, nitakwambia, hauji kama vile tu ulivyokuja katika Siku ile ya Pentekoste. Tunampokea Roho Mtakatifu tunapoamini." Na—na kila namna ya upuuzi kama huo, unaona. Na hebu zungumza juu ya ubatizo katika Jina la Yesu Kristo, wao. . . ambapo Biblia inaufundisha namna hiyo; vema, unasema, "Vema, lakini, seminari inasema! Na *fulani* anasema!" Huko ni kupatana. Unaona? Mungu hawezi kumtumia mtu kama huyo. Unaona?

221 Anaweza kumwacha mtu ataabishwe kila mahali nchini namna hiyo, na mtu huyo atupwe nje na kuchekwa, na kufanyiwa mzaha, na kila kitu kinginecho namna hiyo. Lakini wakati onyesho halisi linapokuja, Mungu husimama na kujithibitisha papo hapo kwenye urahisi huo huo.

222 Anainuka moja kwa moja, kama ua. Ile mbegu, inaonekana kama yote yamekwisha, inakufa na kuanguka ardhini. Chimbua mbegu hiyo ndogo, na imeoza, na inaonekana kama ni mchafuko. Lakini kutokana na hapo uzima unatoka upate kuzaa tena ua lingine tena.

223 Mungu katika urahisi. Yeye hufanya jambo lile lile. Njia ya kupanda juu ni kushuka chini, daima. Jinyenyekezeni. Hata kidogo msiseme, "Vema, nina *hiki* na *kile*." Huna kitu. Ku—kumbuka tu, kama una neema ya Mungu, shukuru tu kwa ajili yake, na uwe mnyenyekevu kwa ajili yake. Unaona, endelea tu kujinyenyekeza.

224 Sasa itanilazimu kuharakisha, maana saa. . .Sitaki kuwacheleweshení sana, maana sitaki kuwachosha, mnaona. Tuna wakati mrefu sana bado katika juma hili.

225 Sasa, na sasa tunaona ya kwamba watu wanakuwa werevu sana na wenye elimu.

226 Sasa nataka kuwaonyesha jambo lingine. Hao—hao wengine wanaenda mbali sana upande ule mwingine, wanakuwa washupavu wa dini, wakijaribu kuwa watakatifu. Sasa, tunajua tuna kundi hilo. Unaona? Wanaenda upande ule mwingine.

227 Hapo ndipo sikubaliani na lile kundi la ndugu waliotoka si muda mrefu uliopita hapa kutoka kwenye—kwenye njia ya Nuru. Wao, wasingeweza kuona maajabu yaliyokuwa yanafanywa wasipojifanyia kundi fulani, kwa hiyo wakakusanyika huko Canada na—na kuunda kundi la watu ambao walikuwa wanaenda kutoa na kuwekana mitume na manabii wenyewe kwa wenyewe, na mambo mengine mengi. Nalo lilitawanyika moja kwa moja. Unaona? Na daima litatawanyika. Unaona? Wakawa. . .Wanajisikia ya kwamba kwa sababu wao ni. . . kwamba hawaninii. . .Wanalaumu sana mambo hayo mengine, na—na mambo kadha wa kadha, mpaka wanaenda moja kwa moja upande ule mwingine. Unaona?

228 Kuna upande mmoja ambao ni wa kiakili sana, baridi na usiojishughulisha na cho chote, hapo wanakana kila kitu. Na hao wengine wanaenda upande huo mwingine, upande huo mwingine wakiwa na kundi la kimapinduzi lenye mwamsho moto moto, na kukana Neno.

229 Lakini Kanisa halisi la kweli linakaa moja kwa moja katikati ya barabara. Sasa, kama ukiangalia, lina—lina—lina maarifa ya Biblia ya yale aliyosema Mungu, na ni—ni la kiroho vya kutosha kuwa na joto moyoni mwake, na liko tu barabarani. Isaya alisema ingekuwa namna hiyo. Alisema, "Hapo patakuwa na njia kuu . . . "

230 Na marafiki wabarikiwa, watakatifu, wapendwa wa kanisa la Kinazarayo, ufufuo mdogo wenye nguvu ambao Mungu alianzisha, lakini walipata nini? Wakati Mungu alipoanza kunena kwa lugha kanisani, wao walikuwa wa kidini sana na wanye majivuno sana, hata waliita jambo hilo, "Ibilisi." Nanyi mnaona kile kilichowapata? Mnaona? Mnaona? Wao, wao, "Mtakatifu kuliko wewe." Na—nasi tunaona ya kwamba mambo hayo yana mwisho na yanakufa moja kwa moja. Mnaona? Na upande huo mwingine.

231 Sasa, upande mmoja unakuwa mshupavu wa dini. Upande huo mwingine unakuwa baridi na mkavu.

Sasa, Isaya alisema, "Hapo patakuwa na njia kuu . . . "

232 Nao Wanazarayo, na wengi wa hao watu wa holiness wa zamani, walizoea kusema, "Ile njia kuu ya kale iliyobarikiwa! Utukufu kwa Mungu! Tunatembea kwenye njia kuu ya kale!" Lakini, mnakumbuka, hivyo sivyo alivyosema hasa.

233 Yeye alisema, "Kutakuwako na njia kuu, na," *na* ni kiunganisho, "na njia." Wala haitaitwa njia kuu ya utakatifu, bali, "Njia ya utakatifu."

234 Sasa, njia kuu ya utakatifu, watu hujaribu kujifanya watakatifu. Na unapofanya jambo hilo, ni kama nilivyosema hapo awali, ni kama ninii . . . Ingekuwa ni kama koho akijaribu kuvaa manyoya ya hua, kujifanya hua, wakati asili yake ingali ni koho. Unaona? Yeye, ni . . . Ingekuwa ni kama kunguru akijaribu kuvaa manyo—manyoya ya njiwa, ama ya tausi, na kusema, "Mnaona, mimi ni ndege anayependeza." Unaona, ni kitu cha kujitengenezea.

235 Lakini tausi hana haja ya kufadhaika kama atakuwa na manyoya ya tausi ama la. Hua hana haja ya kufadhaika kama atakuwa na manyoya ya hua ama hatakuwa nayo. Mradi tu tabia yake ni ya hua, atakuwa na manyoya ya hua.

236 Na, mnaona, watu wa holiness wanaanza kusema, "Wanawake hawana budi kuwa na nywele ndefu na mikono mirefu ya mavazi, na—na vitu hivi vyote, na marinda marefu, na hawapaswi kuvaa pete zo zote za arusi ama johari za namna

yo yote." Unaona, unakuwa utakatifu wa kujitengenezea. Unaona? Unaona? Huo—huo—huo ni utakatifu wa kujibunia. Lakini kanisa halisi la Mungu aliye hai ni...Tena angalia kile kilichoyapata madhehebu hayo. Sasa wote wamekata nywele zao, kama Wapentekoste, na—na kadhalika. Na—nao wote, karibu wote, wanavaa pete na kadhalika. Waangalie Wapentekoste, miaka mingi iliyopita, jinsi walivyoyakazia mambo hayo, unaona, na, "Sisi, kanisa! Sisi, kanisa!"

237 Kanisa ni Mwili wa Kristo. Ni mtu binafsi, miongoni mwa watu wengine binafsi, ambaye anazaliwa katika Ufalme wa Mungu. Hilo linatoka ndani kuja nje. Liko ndani ya mtu linaishi lenyewe.

238 Humwombi kondoo kutoa sufu...ama, kujitengenezea sufu, namaanisha. Kondoo halazimiki kujitengenezea sufu. Aseme, "Sasa, bwana wangu anataka nipate sufu kidogo mwaka huu. Sina budi kujitahidi." La, jambo pekee analopaswa kufanya ni kubaki kuwa kondoo tu. Hiyo ni kweli. Sufu itatoka yenyewe... Itatoka. Itatoka. Yeye ataitoa kwa sababu...

239 Nasi hatuombwi kutengeneza matunda. Tunapaswa kuzaa tunda, unaona, kuzaa matunda. Unaona? Tunapaswa kuzaa tunda. Na mradi tu wewe ni mti wa matunda wa Mungu, ukiwa na Neno la Mungu, Neno la Mungu litajithibitisha Lenyewe. Litazaa matunda mradi tu Neno Hilo limo mle. Yesu alisema, "Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu likikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nalo litatendeka." Mnaona? Hujitengenezei hilo. Hujishughulishi kulipata. Kwa kweli lipo tu pale, na linaendelea na kuendelea.

240 Sasa hebu na tuendelee, kuharakisha tu sasa, tukiwa tu na dakika chache zilizosalia, na ndipo tutafunga.

241 Sasa, sasa, wengine wanaenda mbali hata wanakuwa washupavu wa dini. Sasa, wao wanaenda upande ule mwingine. Nao wanafikiri, kwa sababu eti tu wanaruka-ruka, ama wanapata namna fulani ya mwamsho ama mhamaniko, wananena kwa lugha, ama—ama—ama wanatoa unabii uliotokea kuwa ni wa kweli, ama kitu fulani kama hicho, wanafikiri hilo ndilo jambo lenyewe, ya—ya kwamba wamelipata. Lakini, sivyo.

242 Yesu alisema, "Wengi watanijia Mimi siku ile, na kusema, 'Bwana, sikutoa unabii katika Jina Lako? Katika Jina Lako nikafanya kazi nyingi, na kutoa pepo?'" Alisema, "Ondokeni, sikuwajua." Mnaona? Hilo silo. Hilo silo, ewe rafiki.

243 Hiyo ndiyo sababu...Na, lugha, ati ni ushuhuda? Ninaamini katika kunena kwa lugha, lakini sikuchukui kuwa ndio ushuhuda pekee wa Roho Mtakatifu. La, bwana. Tunda la Roho Mtakatifu ndio ushuhuda. Unaona? Naam. Sasa, unaona, hiyo ndiyo sababu nimehitilafiana na mwenendo wa ndugu wa Kipentekoste, katika njia hiyo, kwamba wao wanasema, "Kama

mtu akinena kwa lugha, yeye ana Roho Mtakatifu." Sikubali. Hiyo si ishara ya kwamba yeye ana Roho Mtakatifu. Unaona?

244 Nimesikia pepo wakinena kwa lugha haraka tu walivyoweza kunena, wanakunywa damu kutoka kwenye fuvu la kichwa cha mwanadamu, na kumwita Ibilisi aje.

245 Nimewaona Wahindi wakichukua nyoka na kuwasokotea kwenye miili yao katika—katika dansi la mvua huko Arizona; wanainua mikono yao juu namna *hiyo*, na kuzunguka mbio moja kwa moja. Mchawi anatokea, akijichanjachanja. Kisha anaweka penseli chini, nayo inaandika katika lugha isiyojulikana, na kuifasiri. Unaona?

Kwa hiyo, usininii, usiniambie jambo hilo. Mimi ni mzee sana wa mambo hayo. Unaona?

246 Kwa hiyo—kwa hiyo tunda la Roho ni ninii . . . Yesu alisema, "Kwa matunda yao," si lugha wala miamsho, "lakini kwa tunda lao mtawatambua." Unaona? Kwa hiyo hilo ndilo tunda la Roho. Ni Mungu akijifunua Mwenyewe katika unyenyekevu, utamu, na kila siku ni vile vile. Ni kitu fulani kuhusu jambo hilo, mtu ambaye hudumu moja kwa moja na Neno. Kila wakati anapoliona Neno, yeye huliitikia kwa "amina," haidhuru watu wengine wanasema nini. Hilo, yeye huliamini, unaona. Vema. Unaona?

247 Lakini tunaenda umbali wa kutosha, halafu, kutegemea kitu cha ushupavu wa dini, na Shetani anaingia kati ya watu. Hiyo ndiyo kazi ya Shetani. Naye ni mfanya biashara hodari. Naye anaingia kati ya watu, anawafanya kufikiri ya kwamba wamempata ati kwa sababu tu wanaweza kuruka-ruka. Halafu ati umchukie jirani yako? La. Unaona? . . . ku—kusema mambo, na kunena kwa lugha vizuri sana tu, na mambo kama hayo.

248 Na, kumbuka, unaweza kunena kwa lugha halisi za Roho Mtakatifu na bado usiwe na Roho Mtakatifu. Biblia ilisema hivyo. "Nijaposema kwa lugha za wanadamu na za Malaika, na nisiwe na upendo, hainifaidii. Nimekuwa kama shaba iliayo, na upatu uvumao." Wakorintho wa Kwanza 13. Unaona? Kwa hiyo huninii . . . Si kwa hilo, unaona.

249 Mmethodisti akasema, "Tulipopaza sauti kwa nguvu, tulimpata," lakini hawakumpata. Mnazarayo akasema, "Walipoishi kitakatifu, walimpata," bali hawakumpata. Mpentekoste akasema, "Tunanena kwa lugha, tumempata," lakini hawakumpata. Unaona? Unaona?

250 Mungu, akijifunua, si katika misisimko. La, hiyo . . . Misisimko, hata hivyo, huambatana Naye. Mnapaona mahali hapo? Linakuwa la kinyofu sana hata mtu ye yote anaweza kuliona, kama hu—kama hujaribu kuweka, kuingiza akili yako mwenyewe katika Hilo, unaona, na mawazo yako mwenyewe. Ni Mungu.

251 Sasa, na ndipo wao wanakuwa kundi la washupavu wa dini. Halafu, *hapa* kuna wale baridi wa kidesturi upande huu; *hapa* kuna washupavu wa dini upande huu mwingine; na *huyu hapa* Bibi-arusi akienda moja kwa moja kuyapita hayo yote, akiita kutoka pande zote mbili. Hiyo ni kweli. Mungu akithibitisha jambo hilo anapoendelea, Neno Lake.

252 Sasa, loo, sina budi kuruka baadhi ya haya kwa sababu nina mengi sana hapa. Nami nina—nina . . . Wakati wangu umekwisha. Nitaharakisha upesi niwezavyo sasa.

253 Tangu Edeni, limekuja toka Edeni, ime—imetabiriwa atakuja Masihi; kote kote tangu Edeni.

254 Sasa nitaruka baadhi ya Maandiko yangu machache niliyoandika hapa chini, na mihtasari, kusudi tuumalize Ujumbe huu, mapema, kama nikiweza. Mungu akijificha katika unyenyekevu. Sasa, nitazungumza kwa haraka, lakini, hata hivyo, ni—ninawataka mlipate jambo hili. Mnaona?

255 Tangu Edeni, ilikwisha kutabiriwa ya kwamba atakuja Masihi. Ilitabiriwa atakuwa ni mtu wa namna gani. Tungekaa kwa muda mrefu. Mnajua Biblia, kile Yeye angekuwa, angekuwa ni mtu wa namna gani. Musa alisema, "Bwana Mungu wako atakuondokeshea Nabii, kama nilivyo mimi." Wao walijua ya kwamba Masihi huyo alikuwa awe nabii, namna ya huduma atakayokuwa nayo. Manabii wote walinena juu ya yale ambayo angefanya. Walinena habari zake katika mifano. Nalo likapita moja kwa moja juu ya vichwa vyao, na moja kwa moja chini ya wengine wao. Mnaona? Mnaona? Ikapita chini ya mmoja, na juu ya mwingine. Unaona?

256 Hata wakati alipowasili kwenye jukwaa la wakati, watu ambao alitumwa kwao walikuwa na tafsiri yao wenyewe wa yale aliyopaswa kuwa, katika fasiri yao ya kujiwazia.

257 Biblia haikubadilika kamwe. Biblia daima ni ile ile. Hiyo ndiyo sababu ninasema, "Maandiko yalisema, nami nadumu na Hilo, 'Biblia si ya kufasiriwa atakavyo mtu mwenyewe.'"

258 Kwa hiyo, Wamethodisti, Wabatisti, Wapentekoste, msijaribu kuweka fasiri zenu Kwake, kusema, "Halimaanishi Hivyo. Linamaanisha *hivi*."

259 Linamaanisha vile tu lilivyosema, ni sawa tu kabisa. Mtu fulani alisema, "Inawezekanaje?" Sijui ni jinsi gani. Hilo si juu yangu kusema jambo hilo. Mungu ndiye anayepaswa kushughulikia jambo hilo. Yeye ndiye aliyesema jambo hilo, si mimi, unaona, Naye atawashughulikia walio Wake.

260 Lakini sasa, lakini, Masihi huyu alikuwa ametabiriwa. Hao manabii walisema vile hasa Yeye atakavyokuja, yale atakayofanya atakapokuja. Lakini, tafsiri yao wenyewe ya jambo hilo, miongoni mwa watu! Na wakati alipokuja, alikuwa katika namna rahisi sana, katika urahisi, mpaka kundi lote

zima la kanisa likajikwaa kwenye jambo hilo. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hapo, watu wale ambao walifundishwa . . .

261 Mtu hangeweza kuwa mwalimu, kuhani, mpaka awe alizaliwa katika ukoo fulani, wa Lawi. Na, wazia tu, babu wa babu wa babu wa babu wa babu wa babu wa babu yake alikuwa kuhani, amedumu moja kwa moja katika hilo Neno, hekaluni, usiku na mchana.

262 Kama vile kasisi wa Kikatoliki ama mhudumu ambaye—ambaye amerithi cheo hicho, kutoka kizazi, kwa makanisa fulani, na kadhalika, "Babu wa babu wa babu yangu alikuwa askofu wa Kimethodisti. Babu yangu alikuwa askofu, na kadhalika." Unaona?

263 Hao wote, waliishi kulingana na Neno, bali walikuwa wametengeneza njia yao wenyewe ya jambo hilo. Na watoto wao walikuwa wamelikubali hilo kulingana na jinsi ambavyo baba zao walikuwa wamelifundisha. Mpaka, baba zao walikuwa wamelifundisha vibaya kutoka kwenye ile njia halisi, nao walikuwa wamejiundia madhehebu, mpaka, wakati Roho Mtakatifu alipojaribu kuwaonyesha ile kweli, hawakuweza kuipokea.

264 Na ndio jambo lile lile leo. Sina maana ya kuwa mkali, bali hiyo ni kweli. Ni jambo lile lile leo. Wao wanalifanya kuwa ninii sana—gumu sana, na—na kuliweka vinginevyo. Wanafundisha nanii wao . . . Kama tu vile ilivyokwisha kunenwa, "Mungu hana wajukuu wo wote." Mnajua jambo hilo? Mungu ana wana, na ana mabinti, bali hana wajukuu wa kiume na wa kike. Kila mtu hana budi kulipia gharama ile ile na kupitia njia ile ile. Kama tu vile alivyofanya baba yako, nawe huna budi kufanya vivyo hivyo.

265 Sasa, kwa hiyo, Yeye alikuwa ni mnyenyekevu sana. Wakati Masihi huyu . . . Kwa miaka elfu nne, kila nabii alinena habari Zake; Daudi aliimba sifa Zake, na tokea zamani zote. Na hapo Yeye alipokuja, watu walikuwa wamejijengea wazo lao wenyewe, yale Yeye anayopaswa kufanya, jinsi gani ataenda kutekeleza. Jinsi yote yalivyoelezewa, yakachorwa kwenye ramani na kadhalika, hivi kwamba, wakati alipokuja kwa njia hiyo rahisi kabisa, jambo hilo lilininii tu—lilibomoa tu theolojia yao. Unaona, wao hawakujua jambo hilo.

266 Yeye alikuja kulingana na Neno. Sasa, unaamini ya kwamba Mungu alinena kupitia kwa manabii, ya kwamba Masihi huyo angekuja kwa njia fulani? Ninasikitika sana hatuna kama saa moja nyingine ambayo tungeweza kupitia hapo na kueleza jinsi ilivyokuwa. Unaona? Sote tunajua jinsi ilivyokuwa, hata hivyo, wengi wetu. Jinsi Mungu alivyosema angekuja, na jinsi ambavyo, "Nawe, Bethlehemu wa Yuda, hu mdogo kamwe katika . . ." Na kupitia nyakati zote kule, na jinsi vile angefanya, na yale angelifanya. Unaona?

267 Na, hata hivyo, Yeye alikuwa ni mnyenyekevu sana! Mpaka, wale wanachuoni wakuu walichanganyikiwa sana na jambo hilo, hata wakalikosa. Lakini, mnajua Yesu hakuja kinyume na Neno. Alikuja kulingana na Neno, lakini kinyume na fasiri yao. Unaona? Alifundisha mambo ambayo yalikuwa kinyume na mafundisho yao ya kidini kumhusu Yeye.

268 Sasa, wao walisema, sasa, kwa mfano, "Masihi ajapo, bila shaka, Yeye atakuja hekaluni na kusema, 'Kayafa,' ama ye yote yule aliye kuhani mkuu, 'nimewasili.' Atakuja na gwaride la heshima la Malaika milioni kumi. Ndipo Mungu atasema, 'Sawa, jamani, ninyi kule chini, kwa kweli ninyi ni—ni kanisa kuu. Ninyi ndio watu wangu. Nitapiga hendeli hapa na kushusha chini vipandio vya Mbinguni. Ninawatumieni Masihi, asubuhi ya leo. Nitazishushia papo hapo uani, na watu wote na wakusanyikie hapo.' Aseme, 'Daktari *Fulani*, wewe na Daktari *Fulani*, nyote mtangulie mbele ya wote, mpate kuwa wa kwanza kumsalimia, mnaona.'"

269 Sasa hilo labda ndilo jambo fulani ambalo ni kama lile wanaloliwazia leo. Sasa, ninajua kidogo ni . . . Linasikika kidogo kama ni la kijinga. Lakini mimi sininii . . . Ninajaribu kusema jambo muhimu.

270 "Na—na, hapo, hivyo ndivyo itakavyokuwa. Na kama haiji hivyo, si sawa; ni pinga-Kristo. Mnaona? Kama tu haliji namna hiyo, ni upinga-Kristo, unaona, kwa hiyo haitakuwa. Na kwa hiyo, basi, kutakuwako na. . . . Halafu, kitu kingine kitakachoshuka, kitakuwa ni gwaride la heshima la Malaika kama milioni kumi, pamoja na bendi zao. Nao watashukia kule nje uani, pale ambapo Sulemani alijenga hekalu, na, loo! kila mahali hapa kupanda na kushuka, mahali hapa patakatifu ambapo walifika watakatifu na wenye hekima, na kadhalika!"

271 "Naam," Yesu alisema, "enyi wanafiki! Enyi wana wa Ibilisi!" Kasema, "Mnayapamba makaburi ya manabii, na baba zenu ndio waliowaweka mle." Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Mnaona? "Ni watu wangapi wenye haki na manabii waliotumwa kwenu, na hata hivyo mkawaua kila mmoja wao!" Mnaona? Lakini ni akina nani ambao Yeye angewaita "wenye haki" basi? Wale ambao wao wanawaita, 'washupavu wa dini na wenda wazimu." Naam.

Hapo, wao walidhani ndivyo ingetukia.

272 Lakini, wakati, Yeye alipokuja kwenye hori, amezaliwa na bi—bikira, huku seremala wa kawaida tu akiwa ndiye baba yake wa kambo, na ma—maskini msichana mdogo asiyejulikana. Unaona, si binti wa kuhani mkuu, ama cho chote kile. Yeye—Yeye alikuja kama . . . kutoka mama mdogo aliyeishi huko katika—katika maskini, nchi duni ya kale iliyoitwa Nazareti. Na ni mwanamume mjane wa kawaida tu; mkewe alikuwa amekufa. Alikuwa na watoto wachache; Yusufu. Na—yeye naye akaposwa.

Na halafu Yeye akaja na jina baya, kwanza. Wao walisema Yeye alizaliwa kiharamu. Loo, jamani!

273 Hilo lilitwanga elimu yao kwa nguvu sana. Unaona? Maadili ya elimu yao hayangeweza kumeza hayo. Fasiri yao ya Maandiko haikujua kitu juu ya jambo hilo, lakini hata hivyo ilikuwa ni BWANA ASEMA HIVI. Loo, jamani!

274 Linanitetemesha, kuliwazia jambo hilo, na kuona jambo lilo hilo likitukia tena. Mungu hawezi kubadilika.

275 Ni saa sita tayari. Nawaombeni mninii tu . . . Nikome, ama ni ninii tu . . . [Kusanyiko linasema, "La. Endelea."—Mh.] Asanteni. Hebu tulieni tu kwa muda kidogo zaidi, mnaona. ["Endelea tu."] Sasa, hii ni, ninawekea msingi jambo fulani hapa kwa ajili ya Ujumbe unaokuja, unaona. Nami nitajaribu kuwaachilieni mtoke upesi sana, labda katika dakika nyingine kumi ama kumi na tano, tukiweza. Mungu awabariki.

276 Angalia, sasa, ni rahisi sana, hata li—li—lilikosa tu shabaha, kwao. Lakini lilipiga shabaha ya Mungu. Unaona, liligonga Neno. Yeye alikuja sawasawa tu kulingana na alivyosema. Lakini, wao, tafsiri zao za jambo hilo zilikuwa mbaya. Tafsiri ya mkombozi katika wakati wa Musa ilikuwa ni ya makosa. Tafsiri katika wakati wa Nuhu ilikuwa ni ya makosa, unaona, lakini Mungu huja kulingana na Neno Lake.

277 Na ndipo Yesu akaja, Naye—Naye alifundisha mambo yaliyokuwa kinyume. "Kama Wewe ndiwe Masihi, fanya *kadha na kadha*," unaona. "Kama Wewe ni nanii, shuka msalabani na utuonyeshe jambo hilo waziwazi." Unaona? Lakini Mungu si mtumbuiza watu kwa kuwachekesha. Mungu hufanya tu mambo yanayopendeza na yaliyo kweli.

278 Wao walidhani Mtu kama huyo bila shaka hana budi kuja na gwaride kuu la heshima la Malaika. Lakini alikuja kwa njia ya hori la ng'ombe. Na, kwa maadili yao ya kielimu, ilikuwa ni jambo la dhihaka kwa mwanadamu wa kawaida kufikiri ya kwamba Mwenyezi Mungu, yule Yehova mkuu na mwenye nguvu, Ambaye ndiye mwenye nchi na aliyeumba kitu hicho chote, hangeweza kumtengenezea Mwanawe Mwenyewe mahali pa kuzaliwa, mahali palipo pazuri zaidi kuliko zizi fulani la ng'ombe juu ya lundo la samadi. Kungewezaje . . . Unaona?

279 Ilikuwa ni nini? Mungu katika urahisi. Hilo ndilo lililomfanya kuwa mkuu sana. Unaona, maadili ya elimu hayawezi kujidhili yenyewe namna hiyo; unaona, hayawezi kustahimili jambo hilo. Lakini Mungu ni mkuu sana hata alijishusha hadi kufikia hapo, hana hata nguo ya kumvalisha Mtoto Wake Mwenyewe. Wazia jambo hilo! Na ulimwengu . . . Hapakuwepo na nafasi katika nyumba ya wageni. Naye akaingia kwenye hori la ng'ombe, mwamba m—mdogo, pango do—dogo, kitu kama hicho, nyuma huko kwenye mimba ya kilima. Ndipo

huko kwenye kitanda cha manyasi makavu akaja Mwana wa Mungu. Loo! hiyo ilikuwa ni tofauti sana na mkutuno kule . . .

280 Naye mama yake alikuwa anatazamia kujifungua. Alionekana ana mimba, loo! miezi kadha hata kabla wao hawajafunga uchumba wapate kufunga ndoa . . . ama hata kufanya ndoa. Unaona? Alikuwa anatazamia kujifungua. Nao watu waliona jambo hilo, nao walijua hali ilikuwa ya namna hii. Na, Mariamu, katika moyo wake mwenyewe, alijua yaliyokuwa yanatendeka.

281 Na Yusufu hakuelewa. Lakini Malaika wa Bwana alimjia usiku, akisema, "Yusufu, wewe ni mwana wa Daudi. Usihofu kumchukua Mariamu mkeo, kwa sababu hilo si jambo baya, lakini huyo ni wa Roho Mtakatifu." Hilo lilitosha. Mtu huyo, Yusufu, alikuwa na uhusiano mkubwa sana na Mungu, mpaka Mungu aliweza kunena naye.

282 Lakini siku hizi tumevalia makoti yetu ya kidini yakiwa yametubana sana mpaka hakuna kitu kinachoweza kunena nasi, nje ya kundi letu la kanisa. Sitaki kuwa mkali ama mpinzani sana, kwa hiyo nitaachilia jambo hilo papo hapo. Angalia. Lakini mnafahamu ninalomaanisha. Angalia.

283 Zizi lilikuwa ni kichekesho, kwao, wasomi. Hata hatuna kumbukumbu yo yote ya mahali pale alipowahi kuhudhuria shule siku moja; na hata hivyo, akiwa na umri wa miaka kumi na miwili, mvulana wa kawaida aliwafadhaisha makuhani hekaluni, kwa mafundisho Yake. Loo, jamani! Ilikuwa ni nini? Mungu akijificha . . .? . . . Ninajisikia wa kiroho sana sasa hivi. Mungu akijificha horini. Mungu akijificha ndani ya Mtoto mchanga. Unaona? Angalia, itajidhihirisha, baada ya muda kidogo, hata hivyo, unaona. Ilimbidi kufanya hivyo.

284 Wakati alipopita mitaani, wazee, bila shaka, wangenena na kusema, "Msicheze na Mtoto yule. Msishirikiane Naye. Mamaye si kitu ila kahaba wa mitaani, mnaona. Na, huyo baba yake na mama yake, huyo Mtoto alizaliwa . . . Kabla kweli hawajafunga ndoa, alikuwa anatazamia kujifungua. Achaneni na kitu hicho."

285 Ni ya ajabu vipi yale Mariamu aliyowazia! Lakini, yote kwa jumla, haidhuru watu huko nje waliwazia nini, yeye aliyatafakari mambo haya yote. Waliyaficha mioyoni mwao. Walijua. Hawangesema jambo baya dhidi yake.

286 Mungu husema na mtu Wake, wakati mwingine, kama, "Tulia. Usiseme kitu juu ya jambo hilo."

287 Nimekuwa na watu katika mikutano yangu wakisema, "Vema, iwapo wewe ni mtumishi wa Kristo, unajua jambo *hili* linaendelea kule."

288 Hakika, nilijua lilikuwa linaendelea. Lakini basi utafanya nini wakati Yeye anaposema, "Nyamaza. Usiseme kitu juu ya jambo hilo"?

289 Niliwachukua watu fulani juzijuzi, na kuwaonyesha, kwenye kitabu. "Kitu fulani kilichonenwa, miaka mingi iliyopita," nikasema.

Kasema, "Vema, singeweza kuelewa na jambo hilo."

290 Nikasema, "Mnaona hapo?" Ilikuwa ni hili hapa, siku zilizopita huku nyuma, nimeandika tarehe yake na kila kitu, wakati lilipotukia huko nyuma. Watu wengi walikuwa wameliona humo kwenye kitabu. Nikasema, "Itaja kuwa ya kwamba hili litafanyika *hivi* na *vile*."

291 Kasema, "Vema, mbona hukusema neno juu ya jambo hilo?" Ingesababi- . . . Ilipaswa kuwa namna hiyo. Unaona?

292 Naye Yusufu alijua vinginevyo. Alijua Mtoto huyo mchanga alikuwa ni wa Nani. Mariamu alijua alikuwa ni wa Nani. Yesu alijua Baba Yake alikuwa ni Nani. Yeye alisema nini? "Sina budi kuwa katika kazi ya Baba Yangu." Si kupasua mbao kwa msumeno na—na kutengeneza mlango; lakini katika kazi ya Baba Yake. Amina. Alimwambia hayo mama Yake, "Je! hamwezi kuelewa ya kwamba, Mimi, ni wakati Wangu wa kuwa katika kazi ya Baba Yangu?"

293 Sasa, wao wakidhani, "Maskini Mtoto huyu aliyerukwa na akili . . . " Mtoto ye yote haramu kwa namna fulani amekaa kiajabuajabu, kitu cha ajabu, hata hivyo. Na hivyo ndivyo ilivyo, unaona, lakini, Mungu akijificha. Sikilizeni. Mungu akijificha katika yale yaliyowaziwa, na ulimwengu, kama, "Uchafu, upotovu, haramu."

294 Angalia, Mungu hujificha katika kuoza kwa mbegu iliyokufa, apate kuleta uhai. Unaona? Mnalipata? [Kusanyiko, "Amina."]

295 Mungu hujificha katika maskini mwanamke dobi wa kawaida. Ama wa mwanamume wa kawaida anayebeba chakula chake mkononi, anawaaga mkewe watoto wake kwa busu, na kutoka aende zake huko, na pengine ajifiche katika mtu huyo apate kufanya kitu fulani ambacho askofu mkuu hangejua kitu hicho ni nini. Unaona? Humsikii akipiga mbiu zo zote na kutangaza. Yeye, Mungu, Ndiye anayepata tu utukufu, hivyo tu. Watu wa kawaida wanalisikia na wanafurahi, unaona.

296 Sasa, Mungu alikuwa akijificha Mwenyewe katika urahisi wa Mtoto Mchanga, akijificha Mwenywe katika urahisi wa jamaa ya ka—kawaida. Mungu! Nao watu wa dini, na watu wakuu, wenye bongo, wenye akili nyingi sana, na—na hao wote, na akina Herode, na kadhalika, wa siku zile, na akina Nero, na hao wote walilipuuza. Mungu akijificha katika urahisi.

297 Sasa, upesi. Yohana Mbatizaji, katika Isaya 40. Tungeweza kuifungua kama mkitaka. Malaki 3. Yote, naam, iandikeni kama mkitaka. Isaya 40, yote, mnajua, ikinena amani kwa . . . kama ilivyo. Labda mimi . . . Huenda likawa ni jambo zuri

ya kwamba ni—ni—ningeisoma papa hapa, kama mna—mna wakati wa kufanya hivyo. [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hebu na tufanye hivyo, kwa muda mfupi tu. Tutafungua hapa katika Kitabu cha Isaya, sura ya 40, na—na tusome hapa na tuone tu yale anayosema juu ya jambo hili sasa. Angalieni hapa, "Watulizeni mioyo, watulizeni mioyo, watu wangu." Sasa, kumbukeni, hii ilikuwa ni miaka mia saba na kumi na miwili. Angalia kwenye kichwa cha maneno pale, unaona. Miaka mia saba na kumi na miwili kabla yeye hajazaliwa, huyu hapa nabii akinena habari zake.

> *Watulizeni mioyo, watulizeni mioyo, watu wangu, asema BWANA.*
>
> *Semeni* maneno ya kuutuliza *Yerusalemu, kauambie kwa sauti kuu ya kwamba vita vyake vimekwisha, ya kwamba uovu wake umeachiliwa; kwa kuwa amepokea. . .Mkono wa BWANA adhabu maradufu kwa dhambi zake zote.*
>
> *Sikiliza, ni sauti ya mtu. . .*akilia nyikani, *Itengenezeni njia ya BWANA; nyosheni jangwani njia kuu kwa Mungu wetu.*
>
> *Na kila bonde litainuliwa, na kila mlima na kilima kitashushwa; palipopotoka patakuwa pamenyoka, na palipoparuza patasawazishwa*;

298 Loo, jamani, jamani! Huyo alikuwa awe ni mtu wa namna gani! Unaona? Sasa fungua Malaki, pamoja nami, Kitabu cha mwisho cha. . .nabii wa mwisho katika manabii wa Agano la Kale. Sasa, katika Malaki, sikilizeni hapa. Malaki analichukua, ilipofikia tu wakati wa mwisho, basi uhakikishe hutalisahau. Malaki, sura ya tatu.

> *Angalieni, namtuma mjumbe wangu, naye ataitengeneza njia mbele yangu; naye Bwana mnayemtafuta atalijilia hekalu lake ghafula; naam, yule mjumbe wa agano mnayemfurahia, angalieni, anakuja, asema BWANA wa majeshi.*

299 Angali akinena kuhusu Yohana, "Nitamtuma mjumbe Wangu mbele Zangu, kuitengeneza njia." Yesu alinena habari zake, katika Mathayo 11:10, alisema:

> Kama mnaweza kulipokea, huyo ndiye aliyenenwa habari zake, *Tazama, Mimi namtuma mjumbe wangu mbele ya uso* wangu,. . .

300 Unaona? Hiyo ni kweli. Sasa, jinsi hawa wote walivyonena! Wakati, ilikuwa kwa miaka mia saba, kulikuwa kuwepo na mtangulizi atakayekuja kabla ya Masihi. Lakini wakati alipotokea jukwaani, katika urahisi namna hiyo, liliwapita. Liliwapita.

301 Kumbukeni, yeye alikuwa mwana wa kuhani. Vema, angalia jinsi jambo hilo lilivyokuwa haliji yeye kutoirithi kazi ya babaye, arudi kwenye seminari. Lakini kazi yake ilikuwa ni muhimu mno. Akiwa na umri wa miaka tisa, aliendа jangwani. Na akatoka, akihubiri. Liliwapita. Alikuwa ni wa kawaida mno, rahisi kupita kiasi, kwa elimu yao ya hali ya juu kumwamini mtu kama huyo. Wakafikiria, wakati mtu huyu atakapokuja . . .

302 Vipi kuhusu, "Kila mahali palipoinuka patashushwa, na mabonde yote yatainuliwa, na mahali pote palipoparuza patasawazishwa"? Daudi aliliona jambo hilo, na akasema, "Mi—milima iliruka kama kondoo dume wadogo, na majani yakapiga makofi." [Ndugu Branham anapiga makofi mara kadha—Mh.]

303 Ati nini? Yalitukia? Maskini jamaa mwenye masharubu kama huyo, asiye na elimu hata kidogo, amevaa kipande cha ngozi ya kondoo, akija huku anajikwaakwaa akitokea katika nyika za Yuda, akisema, "Tubuni, kwa maana Ufalme wa Mbinguni umekaribia. Na ninyi kundi la majoka, msifikirie kusema, 'Mimi ni wa madhehebu fulani.' Mungu anaweza kutoka katika mawe haya kumwinuliwa Ibrahimu watoto." Jamani!

"Vema, huyo siye pale. Tunajua huyo siye."

304 Lakini ilikuwa Ndiye! Unaona, alikuwa akisafisha njia. Unaona? Hapo ndipo mahali palipoparuza paliponyoshwa. Hapo ndipo mahali palipoinuka paliposhushwa. "Msifikiri mna Ibrahimu kama baba yenu. Msianze kuniambia upuuzi kama huo, maana Mungu anaweza kutoka katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto." Mahali palipoinuka palishushwa. Loo, jamani! Hivyo ndivyo ilivyo. Naam. Unaona tofauti yake? Yeye alisema hivyo ndivyo ambavyo ingetukia.

305 Nao walipokuja, walidhani, loo, jamani, walikuwa tu tayari kumpokea, kama angekuja kwenye madhehebu yao wenyewe. Lakini kwa sababu . . . Yeye alikuja kwa namna hiyo, katika njia rahisi namna hiyo. Hata hivyo, katika kuyafasiri Maandiko, mahali palipoinuka palishushwa. Wao hawakutaka kukubali jambo hilo, lakini walishushwa.

306 Loo, aliwanyoa. Aliwachuna ngozi kweli kweli. Kasema, "Enyi kundi la majoka! Enyi nyoka nyasini! Ninawaambia, shoka limewekwa penye shina la mti. Na kila mti ambao hautazaa matunda, unakatwa na kutupwa motoni. Mimi kweli nitawabatiza kwa maji, lakini kuna Mtu anayekuja baada yangu, Ambaye ana nguvu kuliko Mimi; Yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa Moto. Na pepeo Lake liko mkononi Mwake. Atausafisha uwanda Wake kweli kweli. Ataku-. . . atayateketeza makapi kwa moto; na kuipeleka ngano ghalani." Amina.

307 Hapo ndipo mahali palipoparuza paliponyoshwa, unaona, lakini watu hawakufahamu jambo hilo. Lakini ni kulingana

kabisa na Neno, ni vile vile tu Neno lilivyosema. Ni rahisi sana, hivi kwamba wakalikosa. Walikosa kuliona.

308 Usiwe kipofu namna hiyo. Unaona? Usiwe kipofu namna hiyo. Kwa hiyo, sikiliza, sasa.

309 Wao walilikosa. Alikuwa wa kawaida mno, kwa yale waliyozoea kuamini kulingana na mtu kama huyo, hata akalikosa. Tena, ilikuwa ni kitu gani? Mungu, ambaye ni Neno, akijificha katika urahisi; si kasisi mwenye ukosi uliopinduliwa, aliyekuwa mwerevu, ana elimu.

310 Yesu aliwauliza jambo lile lile. Alisema, "Mlitoka kwenda kuona nini?" Wakati wanafunzi wa Yohana walipokuja. Kasema, "Mlienda kuona nini? Mlikwenda kuona mtu aliyevaa vazi la kuhani, wajua, na mavazi mororo," akasema, "mhubiri wa namna hi—hi—hi—hiyo?" Akasema, "Mlikwenda kumwona huyo?"

311 Kasema, "La. Watu wa aina hiyo hubusu watoto wachanga, na, wajua, na kuzika wafu. Wao, hawajui cho chote kuhusu upanga ukatao kuwili katika mstari wa mbele wa vita. Walikuwa wako huko nje na hotuba ya kielimu, kwenye Kilabu Cha Kiwani ama cho chote kile, wajua. Wao wanajisikia sawa huko. Lakini inapohusu vita huku nje, kupigana, hawajui lo lote kuhusu hilo. Wao—wao, wao wako kwenye nyumba za wafalme. Hujipumbaza na watu mashuhuri kama hao."

312 Lakini akasema, "Basi mlikwenda kuona nini? Mlikwenda kuona unyasi ukitikiswa na upepo wo wote? Mtu ambaye angeweza kusema...Mtu fulani aseme, 'Unajua, wewe ni wa—wewe ni wa Umoja; lakini kama utakuja huku kwa Waassemblies, nitakwambia nitakachofanya, tuta—tutalifanya...' 'Ninaamini nitafanya jambo hilo.' Aha! Ati unyasi, unaotikiswa? Si Yohana. La, la. La, la. 'Kama utakuja, uwe Msadukayo na si Mfarisayo, ama kitu fulani, halafu'? Hukuona mtu ye yote akitikiswa na upepo; si Yohana." La, bwana, ndugu; si yeye.

313 Akasema, "Basi mlikwenda kuona nini? Nabii?" Ingetakiwa nabii kufanya jambo hilo, unaona. Akasema... Sasa, hiyo ilikuwa ni ishara ya nabii, unaona, Neno la Mungu likiwa pamoja naye. Neno humjia nabii. Unaona? Kasema, "Mlikwenda kuona nini? Nabii?" Kasema, "Ndiyo, hiyo ni kweli. Lakini, ninawaambia, na aliye mkuu hata kuliko nabii, kwa maana alikuwa hivyo."

314 Kwa nini yeye alikuwa ni mkuu kuliko nabii? Yeye alikuwa ni mjumbe wa lile Agano, hakika alikuwa hivyo, kuunganisha njia kati ya torati na neema. Yeye alikuwa jiwe la pembeni, ndani pale, lililonenwa habari zake.

315 Akasema, "Ikiwa mnataka kukubali, huyu ndiye yule ambaye nabii alimnena habari zake, 'Tazama,' katika Malaki 3, 'Nitamtuma mjumbe Wangu mbele za uso Wangu, unaona,

naye ataitengeneza njia mbele Zangu.'" Unaona? Loo, alikuwa wa kawaida mno. Mungu akijificha tena katika urahisi.

316 Basi angalia alilofanya. Alihubiri juu ya Kristo ajaye mwenye nguvu sana, "Yeye ana pepeo mkononi Mwake. Ataninii . . . Anakuja akipepeta njiani Mwake. Loo, ninamaanisha, Yeye atausafisha uwanda Wake kweli kweli. Ataokota makapi, na kuyafagilia mbali na kuyateketeza kwa moto, pia. Hiyo ni kweli. Atakusanya ngano na kuiweka ghalani." Unaona, yeye alikuwa amevuviwa.

317 Lakini wakati Yesu alipokuja, wao walikuwa wakitazamia . . . Na hao mitume wote, wajua, walikuwa wanatazamia jambo fulani kubwa sana lije. "Jamani, jamani! Loo, Yeye anakuja. Hakuna lingine. Jamani, Yeye atakuwa mkuu. Atawafukuza hao Warumi watoke katika uso wa dunia. Jamani! Atawafanya hao Wayunani waende upande *huu*, na Warumi waende upande *ule*, atakapokuja."

318 Wakati alipokuja, ni maskini jamaa mnyenyekevu akisukumwa huku na huku. Ilikuwa ni nini? Mungu akijificha katika urahisi. Loo, jamani!

319 Ndipo akasimama mwishoni mwa Ujumbe Wake, na kusema, "Ni nani awezaye kunihukumu kwamba nina dhambi? Yote yale Biblia iliyosema kwamba ningefanya . . . Kama sizitendi kazi za Baba Yangu, basi nihukumuni. Lakini Maandiko yalisema ningefanya nini, ambacho sijakifanya?" Dhambi ni kutokuamini, mwajua. "Ni nani anayeweza kunilaumu? Kama nawatoa pepo kwa vidole vya Mungu, basi nionyesheni mnayofanya juu ya jambo hilo." Urahisi!

320 Hata alijinyenyekeza hata mauti! Lakini, loo, katika asubuhi ile ya Pasaka, haleluya, hapo ndipo alipousafisha uwanda. Akafagilia mbali makapi, vema, ndugu. Naam, kweli. Nayo ngano ilitiwa muhuri ikawekwa ghalani. Ikilala pale ardhini, ikiwa na Uzima wa Milele umepumzika ndani, ikingojea ile Siku kubwa ambayo tutanena habari zake, kule Kuja kwa Bwana, wakati uhai huo utakapopata Uzima; nasi tutafufuka katika ule ufufuo, tutanyakuliwa pamoja Naye hewani, na kukusanywa Ghalani. Nayo magugu yatateketezwa kwa moto kule; maganda yaliyoifunika, na kujaribu kuivuta *hivi* ama *vile*, yatateketezwa kwa moto usiozimika. Amina. Loo, Yeye si ni wa ajabu! [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

321 Wao walimkosa, Mungu katika urahisi. Kwa nini? Kwa nini? Yeye hata hakuhubiri katika maneno ya kidini. Hakuhubiri hivyo kamwe. Hakuhubiri kamwe kama mhubiri. Unaona? Alihubiri kama . . . Alitumia maneno ya urahisi ya Mungu, matamshi kama "shoka limewekwa," matamshi ya "mti," matamshi ya "majoka." Si mwalimu fulani wa seminari, kama vile katika dini za wakati huo, kama Daktari wa Uungu, Daktari *Fulani*. Hakufanya hilo. Alihubiri kama mtu wa mwituni huko

machakani ndani ndani mahali fulani. Alizungumzia kuhusu mashoka, na miti, na majoka, na vitu kama hivyo, na ngano, na maghala, na kila kitu namna hiyo. Angefikiriwa, siku hizi, nadhani, mhubiri wa mitaani. Nafikiri aliitwa "mhubiri mzushi wa mitaani." katika siku hizo, akiwa amesimama penye kisiki huko chini kwenye maeneo ya karibu na Yordani. Lab-. . . Mungu katika urahisi, akijificha mbali na hekima ya ulimwengu.

322 Sasa hebu na tuone. Yesu alisema, "Nakushukuru Baba, uliwaficha mambo haya wenye hekima wa dunia, na utawafunulia watoto wachanga ambao wanaweza kujifunza." Unaona? Mungu akijificha katika urahisi, katika Kristo. Mungu akijificha katika urahisi, katika Yohana. Unaona? Ninii tu. . . Unaona, Yeye—Yeye alikuwa. . . Wazia tu jambo hilo, Mungu katika urahisi, akijificha Mwenyewe mbali na hekima ya ulimwengu.

323 Sasa tutafunga, mnamo dakika moja tu, ama mbili, maana sitaki kuwaweka kwa muda mrefu zaidi tena.

324 Angalieni, hebu na tusimame kwa muda kidogo, jambo fulani la kibinafsi. Hebu wazieni siku hizi tunazoishi, tukimalizia hili sasa. Fikirieni siku hizi tunazoishi, Mungu anapokuja katika maskini mahali padogo pa hali ya chini ambapo tumekuwa tukiishi, akiwaponya wagonjwa. Na watu matajiri, na wenye kiburi, na wenye kisomo cha juu sana, "Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu."

325 Mnakumbuka ule Ujumbe niliohubiri moja kwa moja kutoka ile ng'ambo ya pili wa kisehemu hiki cha ardhi, ile asubuhi niliyoondoka, kuhusu Daudi na Goliathi?

326 Kasema, "Utakabilianaje na ulimwengu wenye elimu huko nje, Ndugu Branham, na mambo yote Haya?"

327 Nikasema, "Siwezi kujizuia jinsi vile nitakavyokabiliana nalo. Mungu alisema, 'Nenda." Unaona? Ni hilo tu, unaona. Ni Neno Lake. Yeye aliliahidi. Saa hiyo imewadia.

328 Wakati yule Malaika, ambaye mnamwona katika ile picha pale, aliposhuka kule mtoni siku ile, miaka thelathini iliyopita Juni hii ijayo, ama miaka thelathini na mitatu iliyopita, hasa, Juni hii ijayo; na kusema, "Kama vile Yohana Mbatizaji alivyotumwa," mbele ya watu elfu tano ama zaidi, "saa imewadia ambapo Ujumbe wako utakapotangaa dunia nzima."

329 Mnakumbuka zile lawama, kama ye yote wenu alikuwapo pale. Nafikiri, Roy Slaughter, ama baadhi yao wanaoketi hapa, wanaweza kukumbuka siku ile; ama baadhi yenu, Bibi Spencer, ama—ama ye yote yule angekuwa baadhi ya watu wale wa siku nyingi hapa ambao wange—wangejua, mnaona; George Wright, ama baadhi yao, unaona, wanajua jambo hilo, jinsi ilivyokuwa. Lakini je! Hilo halikutimia? [Kusanyiko, "Amina."—Mh.] Lilitimia.

330 Na halafu katikati, walipoukataa, na kusema, “Ni uponyaji tu wa kimawazo.” Ndipo Mungu akageuka moja kwa moja na kumleta maskini komba, asiyeweza kusema, pale ndani, naye akaponywa kwa Nguvu za Mungu.

331 Lyle Wood na Ndugu Banks, wakati tulipokuwa tumeketi pale, na kujua kweli iliyothibitishwa na Mungu. Wakati, maskini samaki mdogo wa mtoni aliyekufa, akielea majini. Na ndipo Roho Mtakatifu akanena, siku iliyotangulia, alikuwa anaenda kuwaonyesha Utukufu Wake na kufanya jambo fulani juu ya hilo. Na hapo asubuhi hiyo, nikiwa nimesimama pale, Na Roho Mtakatifu akashuka ndani ya mashua hiyo, nami nikasimama na kunena na samaki huyo. Naye akiwa anaelea pale majini, amekufa, kwa nusu saa; mashabu yake na matumbo yametokeza mdomoni mwake. Akafufuka, na akaogelea akaenda zake vizuri tu kama samaki mwingine ye yote. Ni kitu gani? Mungu akijificha katika urahisi.

332 Mungu anaweza kutoka kwenye mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto. Mungu anaweza kumponya komba, ama samaki, ama cho chote kile. Kama ataleta Ujumbe Wake, nao watu hawatauamini, Mungu anaweza kumwinua komba auamini. Haleluya! Mungu anaweza kumfufua samaki aliyekufa. Anaweza kumwinua komba aliyekufa. Anaweza. Anaweza kufanya lo lote analotaka kufanya.

333 Ni kemeo la jinsi gani kwa kizazi hiki! Wakati wanapojikwaa katika Hilo, na kuzozana juu Yake, na, “Hukufanya jambo *hili* na kufanya *lile*.” Na ndipo Mungu anamleta mnyama wa kawaida. Unaona? Ni kemeo la jinsi gani! Ilikuwa ni nini? Mungu katika urahisi, unaona, akijionyesha Mwenyewe kuwa mkuu, loo, jamani, anawakemea watu hawa wa kizazi hiki, kwa kutokuamini kwao.

334 Sasa, wanafikiri sasa kama vile walivyofikiria sikuzote, halina budi kutendwa jinsi vile wao watakavyo. “Sasa, kama kuna kitu kama kuponya Kiungu . . . ” Kama vile, mtu mmoja Mkatoliki alivyoniambia jambo hili. Jamaa mmoja, hivi majuzi usiku, aliniambia jambo hilo. Mnajua habari zake. Alisema . . . Huyu Ayers, niliyeenda kushughulikia habari za mvulana wake kule Houston, alisema—alisema, “Vema, sasa, kama—kama hiyo ni karama ya Mungu, ingepaswa kupitia katika kanisa Katoliki.” Mnaona? Mnaona? Naam, Wamethodisti walidhani ingebidi ije kwenye kanisa lao. Na Wapentekoste walidhani ingepaswa ije katika kanisa lao. Lakini haikuja katika lo lote la hayo.

335 Ilikuja katika Nguvu za kufufuka za Yesu Kristo akijidhihirisha Mwenyewe. Hiyo ni kweli. Hakika, Yeye hufanya hayo. Naam. Angalia tu jambo Hilo. Usiliache likupite. Liwekeni chini ya moyo we—wenu, na mlikumbuke. Yatafakarini hayo.

336 Halina budi kuja wapendavyo wao, kwa ajili ya ninii yao, kutokana na madhehebu yao wenyewe. “Na isipofanyika hivyo,

si Yeye, unaona. Ni saikolojia tu, ama ni Ibilisi. Ni—ni ninii . . . Si Mungu. Kwa sababu, kama ingalikuwa ni Mungu, Yeye angepaswa kuja," kwa njia yao wao wenyewe, unaona, "jinsi vile sisi tulivyolifasiri."

337 Hivyo ndivyo Yesu alivyokuwa amekuja kwa Mafarisayo. Ilipaswa iwe namna hiyo. Unaona? Kama ninii wao . . . Kama Mungu alikuwa anaenda ku—kumtuma Ma—Masihi, walikuwa wameisha tafsiri kabisa jinsi ambavyo ilivyobidi Yeye awe. Na kwa sababu alikuja tofauti, basi, "Haikuwa Masihi. Alikuwa kitu fulani cha haramu. Alikuwa Beelzebuli." Lakini ilikuwa ni Mungu akijificha katika urahisi.

338 Mtangulizi lazima awe ni mtu fulani mwenye elimu ambaye ninii yao . . . Vema, mtu, hapana shaka . . . Kila siku, kila mwaka ambapo wao, naam, walipowachagua wahudumu wao na kuwatuma huko nje kama wamishenari, kuongoa na kuwaleta; kila mmoja wao alidhani, "Huyu ndiye atakayekuwa yule mtangulizi ajaye." Lakini Mungu alimwinua kutoka jangwani ambako hakukuwako na seminari hata moja, unaona, na mambo kama hayo. Unaona? Mungu akijificha katika unyenyekevu na katika urahisi.

339 Lakini sasa ngoja. Katika kufunga, tunasema jambo hili. Lakini kuukataa Ujumbe rahisi wa Mungu; ku—ku—kuukataa Huo, njia rahisi ya Mungu, ni kuangamizwa Milele. Sasa, hivyo ndivyo kiasi ninii . . . Tunazungumza jinsi ulivyo rahisi, na watu wanafikiri, vema, wanaweza kuucheka na kutoujali, na kuufanyia lo lote watakalo, lakini huko ni kutengwa Milele na Mungu.

340 Wale waliokufa katika siku za Nuhu, na hawakuusikiliza ujumbe wake, waliangamia. Naye Yesu alienda na akawahubiri wakiwa katika vifungo vya giza, katika mauti Yake, kabla hajafufuka. Ndipo akaenda kuzimu, na kuwahubiri roho waliokaa kifungoni, watu wasiotubu hapo zamani katika uvumilivu katika siku za Nuhu; wakati ujumbe rahisi wa Mungu, kwa mtu wa kawaida, ulikuwa unahubiriwa. Alienda. Alisema, "Nuhu alihubiri ya kwamba ningekuja hapa, Na ndio Mimi hapa nimekuja." Hiyo ni kweli. Unaona?

341 Wale walioshindwa kuusikiliza ujumbe wa nabii huyo, Musa huko jangwani, ambao aliupokea kutoka kwa Mungu, uliothibitishwa vizuri sana na Nguzo ya Moto, na kuongozwa huko jangwani. Na halafu wanajaribu kuinuka na kujiundia madhehebu kwa ujumbe huo, nao wakaangamia na wakafa jangwani, kila mmoja wao, ukiondoa watu wawili, Yoshua na Kalebu.

342 Na kule, Ma—Mafarisayo walikuwa vipofu sana hawakuweza kuona jambo hilo, kwa hiyo waliangalia nyuma na kusema, "Baba zetu walikula mana, walikula mana jangwani."

343 Na Yesu akasema, “Nao, hao kila mmoja, amekufa.” Waliona utukufu wa Mungu. Walitembea katika Nuru ya ile . . . Walitembea katika Nuru. Walitembea katika Nuru ya ile Nguzo ya Moto. Walitembea katika Uwepo wa nguvu Zake. Walitembea kupitia sehemu ambazo Roho Mtakatifu aliwafanyia wapate kupita. Walikula mana iliyoshuka kutoka Mbinguni, ambayo Mungu aliwapa. Nao, wakapotea, na kwenda kuzimu. “Hao, kila mmoja wao, *amekufa*.” Kama ukilichukua Neno hilo, ni “Kutengwa Milele” na Uwepo wa Mungu. “Hao, kila mmoja, amekufa.” Unaona.

344 Kila mtu aliyemkataa Yesu ameangamia. Unaona ninalomaanisha? Kukataa urahisi huo wa Mungu! Si kitu tu cha ninii . . . Unasema, “Vema, nilifanya kosa.” Hulifanyi namna hiyo. Mungu halipokei namna hiyo. Unaangamia, Milele. Afadhali tuwe tunafikiria jambo fulani. Sasa, hauna budi kutambulishwa vizuri na Mungu, unaona, na halafu basi, kama umetambulishwa, unakuwa ni Neno Lake. Unaona? Loo! Kama wale waliomkataa Musa, waliomkataa Eliya, waliomkataa Yohana, waliomkataa Yesu, katika siku zao.

345 Hapa, hebu niwaambie tu jambo dogo sana. Na, basi, natumaini siwaudhi kupita kiasi. Lakini, angalieni. Juzijuzi niliitwa huko Houston, Texas, kujaribu kumwombea mtu msamaha. Kwa kuwakusanya watu pamoja, kuhubiri ujumbe, na kupata watu kule ili kutia sahihi msamaha wa—wa jamaa huyu mvulana kijana na kijana msichana. Mnajua waliingia katika ile shida. Nadhani mmesoma habari zao katika gazeti. Na huyo alikuwa ni mwana wa kambo wa Bw. Ayers.

346 Na Bw. Ayers ndiye aliyechukua picha ya yule Malaika wa Bwana, ile mnayoiona halisi pale. Mromani Katoliki; na mkewe alikuwa ni Myahudi. Naye alimwoa msichana huyu wa Kiyahudi. Hawangezungumza mambo ya dini kati yao, na kadhalika, namna hiyo. Naye Ted Kipperman, aliyekuwa pia pamoja naye katika biashara, alikuwa tajiri wa studio za Douglas.

347 Na wakati alipokuja kule, ambapo Bw. Best, Dk. Best, kanisa la Kibatisti, alipoweka ngumi yake chini ya pua ya Ndugu Bosworth, na kumtishatisha na hiyo ngumi, na kusema, “Sasa nipigeni picha, wakati nikifanya hivyo.” Kasema, “Nitaichuna ngozi ya mzee huyo na kuitundika kwenye chumba changu cha kusomea, kama kumbukumbu la uponyaji wa Kiungu.”

348 Nami kabla sijaenda huko Houston, Texas, Bwana Mungu aliniambia niende kule. Nami nilikuwapo kule katika Jina la Bwana. Na nyote mnajua ule mjadala na mambo yaliyotokea. Mmeyasoma katika vitabu, na kadhalika. Na hivyo ndivyo ilivyokuwa. Na usiku huo . . . Nilikuwa tu nikijaribu kutembea kwa unyenyekevu.

349 "Mbona," wao walisema, "wao ni kundi la majuha." Dk. Best alisema, "Hao si kitu ila kundi la majuha." Kasema, "Hakuna watu wanaoamini katika upuuzi wa kuponya Kiungu, kama huo. Hilo ni kundi la watu wa nyuma." Hawajui ya kwamba ilikuwa ni Mungu katika urahisi. "Mbona," walisema, "mtu huyo mwenyewe hana hata elimu ya sekondari."

350 Yeye alikuwa amehitimu kwa digrii zote za wanachuoni alizoweza, mpaka alidhani angeweza kumkaba koo Ndugu Bosworth, apendavyo. Lakini ilipofikia kwenye Neno, hakuwa hata sehemu moja ya kumi yake kuweza kushindana naye. Unaona? Naye Ndugu Bosworth alijua mahali alipokuwa amesimama. Watu wake wengi, walioketi hapa sasa hivi, walikuwapo kwenye yale mahojiano. Na hivyo ndivyo ilivyokuwa.

351 Ndipo akaturukia vizuri kabisa, akisema ya kwamba tulikuwa eti sisi ni kundi la majuha. Kasema, "Watu wenye mawazo ya maana hata hawaaamini jambo hilo."

352 Ndugu Bosworth akasema, "Hebu kidogo." Akasema, "Ni watu wangapi katika mji huu," wa watu kama elfu thelathini usiku huo, waliokuwa wameketi katikati yetu namna hiyo, "Ni watu wangapi wa mji huu hapa, wanaohudhuria makanisa haya makubwa, mazuri ya Kibatisti, wanaoweza kuthibitisha kwa maandishi ya daktari ya kwamba wameponywa na Nguvu za Mungu tangu Ndugu Branham alipokuwa katika jiji hili, wasimame." Na watu mia tatu wakasimama. "Na hao je?" Hilo lilitosha. Mungu alikuwa akijificha katika urahisi. Kisha akasema, "Ndugu . . . "

353 Akasema, "Mleteni huyo mponyaji wa Kiungu. Hebu nimwone akimnuizia mtu fulani, halafu hebu niwaangalie mwaka mmoja kutoka siku ya leo." Naye Ted Kip . . .

354 Naye Ayers pale, yule yule aliyepiga picha hiyo, akasema, "Bw. Branham si kitu ila mnuizaji. Nilimwona mwanamke, aliyekuwa na tezi shingoni, namna *hiyo*, na," kasema, "alimnuizia mwanamke huyo. Kesho yake nilizungumza naye, naye hakuwa na tezi yo yote." Kasema, "Mtu huyo alimnuizia." Na, loo, alinidhihaki tu. Kasema napaswa nifukuzwe niondolewe humo mjini, naye ndiye anayepaswa kufanya jambo hilo, unaona, na mambo yote kama hayo. Maandishi makubwa-makubwa kwenye ukurasa wa mbele wa gazeti la Houston Chronicle.

355 Mimi kamwe sikusema neno. Nilikuwa niko kule kutenda mapenzi ya Baba Yangu, na ni hivyo tu; kudumu na Neno hilo. Yeye alinituma kule, na ni wajibu Wake.

356 Usiku huo nilipoenda kule, nilisema, "Mi—mi—mi—mimi si mponyaji wa Kiungu. La. Kama mtu ye yote akisema jambo hilo," nikasema, "wamekosea." Kisha nikasema, "Mimi sitaki kuitwa mponyaji wa Kiungu." Nikasema, "Kama Dk. Best hapa

anahubiri wokovu, basi yeye hangependelea kuitwa Mwokozi wa Kiungu." Kisha nikasema, "Basi, mimi ninahubiri uponyaji wa Kiungu, sitaki kuitwa mponyaji wa Kiungu. Lakini yeye anasema yeye si Mwokozi wa Kiungu; bila shaka, yeye siye. Wala mimi si mponyaji wa Kiungu. Lakini, 'Kwa mapigo Yake sisi tuliponywa.' Mimi ninaelekeza kwenye jambo Hilo." Unaona?

Na kwa hiyo, yeye, "Upuuzi!" Unajua, akarandaranda huku na huko.

357 Basi nikasema, "Lakini kama Uwepo wa karama hii ya Mungu, huyu Malaika wa Bwana, kama Hilo linatiliwa shaka, Hilo linaweza kuthibitishwa." Yapata wakati huo, huyu hapa akaja, akishuka chini kwa upepo wa kisulisuli. Nikasema, "Hakuna haja ya kuzungumza sasa. Yeye tayari amenena kwa niaba yangu." Ndipo nikatoka.

358 Ndipo nikaenda huko Houston, jiji hilo kubwa, moja ya majiji mazuri sana yaliyopo nchini, mahali po pote. Nilipoingia humo, juzijuzi, ilikuwa ni aibu kuuangalia mji huo. Mitaa yake ilikuwa michafu. Kaunta za mahali hapo, moja kwa moja kupitia katika Mtaa wa Texas, ndipo nikaingia kwenye Hoteli ya Rice, ambapo wacheza sinema maarufu walikuwa wakikaa, na nikashuka nikaenda kwenye orofa ya chini, ule mkahawa, na dari imeanza kuporomoka, na lipu iko kwenye sakafu, na uchafu na takataka. Na ghasia miongoni mwa wahubiri ambako sijawahi kuishi ama kusikia maishani mwangu.

359 Kwa nini? Kukataa Nuru ni kutembea gizani. Hao hapo watoto wao wakingojea hukumu ya kifo. Kweli. Mungu akashuka. Wakati ule urahisi ulipoonyeshwa kisha ukakataliwa, ndipo Mungu akajionyesha Mwenyewe katika urahisi.

360 Na hapo wakapiga ile picha ambayo imesambazwa kote ulimwenguni. Hata wanasayansi walisema ya kwamba ndicho Kiumbe pekee cha kimbinguni kilichowahi kupigwa picha katika historia yote ya ulimwengu; na imetundikwa huko Washington, D.C., katika ukumbi wa sanaa za dini. Hilo hapo, urahisi ukidhihirishwa, basi. Unaona? Unaona? Mungu akijificha katika urahisi, kisha anajidhihirisha. Mnaona?

361 Sasa, Yeye alijificha katika mauti ya Kristo, lakini akajidhihirisha katika ufufuo. Loo, jamani! Na kadhalika, unaweza, tunaninii tu . . . tunaweza . . . Hakuna mwisho wake; tunaendelea tu kusema. Lakini hivyo ndivyo ilivyo, unaona.

362 Kukataa kusema kuna nuru ya jua, ni kuingia kwenye orofa ya chini na kufunga macho yako usione nuru. Na hiyo ni kweli. Na, kumbuka, jinsi tu unavyoweza kukosea, ni kwanza kukataa kweli. Unaona? Na kukataa kufungua macho yako, utaishi katika giza. Unaona? Kama ukikataa tu kuangalia, utaonaje? Unaona? Angalia mambo yaliyo rahisi. Ni yale mambo madogo unayoacha bila kuyashughulikia, si yale mambo makuu unayojaribu ku—kufanya. Loo, jamani!

363 Halafu, angalia hapa, hebu niwaambieni. Katika Mal-. . . katika Mathayo 11:10, Yeye alisema, “Kama mnataka kulipokea, huyu ndiye yeye.” Mnaona? “Huyu ndiye aliyetumwa mbele Zangu.” Ilikuwa ni urahisi.

364 Yeye aliulizwa siku moja, kasema, “Ni kwa nini waandishi wanasema basi ya kwamba . . . ”

365 Yeye, Yeye akasema, “Mwana wa Adamu anaenda Yerusalemu. Ninaenda kutiwa katika mikono ya wenye dhambi, nao watamwua Mwana wa Adamu. Naye atakufa, na katika siku ya tatu atafufuka tena.” Kasema, “Msimwambie mtu ye yote ono hilo, kule juu.”

366 Nao wale wanafunzi, sasa wazia jambo hilo, wale wanafunzi waliokuwa wametembea na Yohana, waliozungumza naye, wakala naye, huko jangwani, waliketi kingoni, ndipo wakasema, “Kwa nini waalimu wanasema ya kwamba imempasa Eliya kuja kwanza? Wewe unasema unapanda kwenda kusulibiwa, na ati utafufuka. Wewe ni Masihi, utachukua kiti cha enzi. Sasa kwa nini waandishi . . . Maandiko yetu yote yanasema hapa, Maandiko yanasema dhahiri, ya kwamba, kabla ya kuja kwa Kristo, ya kwamba Eliya atakuja kwanza.” Naam. Mnaona?

367 Akasema, “Amekwisha kuja tayari, nanyi hamkutambua jambo hilo.” Sasa, huyo alikuwa ni nani? Wanafunzi.

368 Hapa nitaumiza, kidogo tu sasa, lakini simaanishi kufanya hivyo, mnaona; kwa dakika chache zifuatazo, unaona, dakika moja tu, ama mbili, lakini ili kwamba mwe na hakika kufahamu. Mnaweza kunisikia? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

369 Angalia! “Mbona?” Hao watu waliokuwa wametembea pamoja na Kristo, “Mbona Maandiko, kwanza, yanasema ya kwamba imempasa Eliya kuja?” Nao walikuwa ni waongofu wa Yohana mwenyewe, wala hata hawakumjua. “Mbona Maandiko yamesema, hao waalimu?” Mnaona ninalomaanisha? Mnaona? “Mbona Maandiko yanasema ya kwamba Eliya hana budi kuja kwanza?” Wanafunzi waliotembea naye, “Kwa nini Maandiko yanasema yeye hana budi kuja kwanza, kabla ya mambo haya, na kuyatengeneza mambo yote?” Alikuja, kwa yapata watu nusu dazani, na ni hao tu waliokuwako. Unaona? Hao ndio tu waliopaswa kulipokea. Hao ndio waliochaguliwa kuliona.

370 Yesu alisema, “Amekuja tayari, wala hamkumtambua. Lakini alifanya yale tu ambayo Maandiko yalisema angefanya. Aliwarejesha, ninyi nyote mlionipokea Mimi na kuniamini Mimi. Alifanya kulingana kabisa na Maandiko yalichosema angefanya. Nao wakamfanyia yale Maandiko yaliyosema wangemfanya. Yeye amekuja tayari, nanyi hamkutambua.”

371 Mko tayari? Ninataka kuwashtusha kidogo. Kunyakuliwa kutakuwa namna hiyo hiyo. Kutakuwa rahisi sana, hapana shaka kutakuwa vile vile, hata Kunyakuliwa kutatukia moja ya siku hizi wala hakuna mtu atakayejua kitu juu yake. Sasa,

msininii, msininii, msiamke sasa, lakini hebu chunguzeni kidogo tu. Hakika ninamalizia. Kunyakuliwa kutatukia kwa njia rahisi sana hivi kwamba hukumu zitashuka, nao watamwona Mwana wa Adamu, ndipo watasema, "Je! hatukupaswa kuwa na *kadha na kadha*? Na je! si tulipaswa tutumiwe Eliya? Na si kulipaswa kuweko na Kunyakuliwa?

372 Yesu atasema, "Kumetukia tayari, nanyi hamkujua." Mungu katika urahisi. Mnaona?

373 Sasa, juma hili tutaingilia mafundisho yenye kilindi sana juu ya . . . ? . . . Sasa, angalieni, Kunyakuliwa, kutakuwako na wachache sana katika Bibi-arusi huyo! Haitakuwa . . .

374 Sasa mnaona jinsi waalimu walivyolipata? Wana michoro, nao wanaenda, wanaonyesha watu milioni kumi wanaokuja hapa; Wamethodisti wote, kama ni mhubiri wa Kimethodisti; kama ni Mpentekoste, Wapentekoste wote wakija. Haitakuwa hivyo kamwe.

375 Itakuwa, labda mmoja aondoke Jeffersonville, mtu fulani tu akosekane. Wao watasema, "Vema, hujaninii kamwe . . . " Hao wengine hawatajua. Kutakuwa na mmoja atakayetoka Georgia. Unaona? Kutakuwa na mmoja atakayetoka Afrika. Na hebu tuseme kungekuwa na watu mia tano, walio hai, watakaohamishwa. Sasa, hilo—hilo si shirika la kanisa. Huyu ni Bibi-arusi. Hilo si kanisa. Huyu ni Bibi-arusi. Unaona?

376 Ka—kanisa litafufuka kwa maelfu, lakini hilo ni katika ufufuo huo mwingine. "Hawakuwa hai hata itimie ile miaka elfu." Mnaona?

377 Lakini, katika Bibi-arusi, kama watu mia tano waliondoka duniani dakika ii hii, ulimwengu haungejua kitu juu yake. Yesu alisema, "Mmoja atakuwa kitandani; Nami nitamchukua mmoja, nimwache mwingine." Huo ni wakati wa usiku. "Wawili watakuwa kondeni," upande ule mwingine wa dunia, "Nitamchukua mmoja na kumwacha mwingine. Na kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwa Mwana wa Adamu."

378 Wazia! Kila kitu kitatenda kazi kwa kawaida tu kiwezavyo. Ujumbe wa ushupavu wa dini utatolewa, na, muda si muda wajua, jambo fulani, "Mhudumu huyu, alienda mahali fulani, hakurudi. Labda alienda mwituni, kuwinda. Hakurudi tena. Na jamaa *huyu* alienda mahali fulani. Unajua kilichotukia? Ninaamini, msichana huyo mdogo, hapana—hapana budi alitekwa nyara mahali fulani, wajua, mtu fulani alimpeleka msichana huyo huko na kumnajisi, labda amemtupa mtoni. Hakuwa na mtu ye yote." Nusu yake . . . tisini na tisa kutoka katika kila . . . Naweza kusema mmoja kutoka katika kila millioni mia moja atajua lo lote juu yake; mnaona, iwe ni mtu ambaye anamjua, aseme, "Yule msichana hayupo. Mbona, siwezi kufahamu. Yeye hajawahi kuondoka namna hiyo kamwe." La.

379 Na wakati wanaposema, “Ma—makaburi yatafunguliwa.” Makaburi yatafungukaje? Wakati, si—sina muda wa kuingilia jambo hili, lile nililotaka. Itanilazimu kuchukua jambo hili, unaona, kuwaonyesheni tu urahisi wa Mungu. Na hiyo chumvi, shura, na kila kitu, wakati—wakati . . . Kila kitu kilichoko ndani yako, maunzi, vinajaa kijiko kimoja tu. Hiyo ni kweli. Na vile hivyo vinavyofanya, vinavunjika-vunjika vikawa roho na uhai tena. Mungu anatamka tu, na Kunyakuliwa kutatukia. Si kwenda huko nje, na Malaika wanashuka na kuchimbua makaburi, na kuufukua mzoga wa kale hapa. Ni nini? Mwili huo ulizaliwa katika dhambi, kwanza. Lakini, Ule mpya, uliofanywa kwa mfano wake, mwajua. Unaona? Kama tuna *huu*, tutakufa tena. Unaona? Hakuna mtu . . . Mnasema, “Makaburi yatafunguka. Wafu watatoka.” Hiyo yaweza kuwa ni kweli, lakini si kufunguka jinsi unavyosema kufunguliwa. Unaona? Hiyo ni kweli. Unaona? Haitakuwa namna hiyo.

380 Itakuwa ni siri, kwa sababu Yeye alisema atakuja “kama mwivi usiku.” Yeye tayari amekwisha kutuambia jambo hili, kule Kunyakuliwa.

381 Ndipo hukumu zitapiga; dhambi, mapigo, maradhi, na kila kitu. Nao watu watalilia mauti iwachukue, wakati wa ile hukumu. “Bwana, kwa nini hukumu hii iko juu yetu, wakati Wewe ulisema kutakuwako na Kunyakuliwa kwanza?”

382 Yeye atasema, “Kumetukia tayari, wala hamkutambua.” Unaona? Mungu akijificha katika urahisi. Loo, jamani! Vema. “Ni hivyo tu, hilo limetukia tayari, na hamkujua.”

383 Kwa nini waamini hawaamini zile ishara rahisi za Kuja Kwake?

384 Wanatarajia mambo haya yote yaliyonenwa na Maandiko, na—na mwezi utatua mcha- . . . ama jua, litatua mchana, na kutakuwako na mambo ya kila namna. Loo, laiti tungalikuwa tu na . . . Nina mihtasari iliyoandikwa hapa juu ya hilo, unaona, kuwaonyesha mambo hayo ni nini. Nasi tutayapata katika kule kuvunjwa kwa Mihuri hii juma hili, hata hivyo, mnaona. Mnaona? Hilo hapo, mahali ambapo jambo hili limepita tayari, wala hamkutambua. Angalieni kama ndivyo ilivyo, kama Malaika wa Bwana ataivunja hiyo Mihuri kwa jambo hilo. Kumbukeni, kimetiwa muhuri na hizo Ngurumo Saba za siri. Unaona?

385 Sasa ni nini? Kwa nini watu wasiamini urahisi rahisi wa kundi la watu wanyenyekevu, mnaona, na Sa—Sauti ya ishara za Mungu? Kwa nini wasiamini jambo hilo? Ni kama tu vile ilivyokuwa siku zote, Neno la kweli la Mungu likidhihirishwa. Ni kwamba, wao ni werevu sana na wenye elimu sana hata hawawezi kuamini namna rahisi ya Neno lililoandikwa. Wanataka kuweka fasiri yao wenyewe Kwake. “Halimaanishi *hivi*. Halimaanishi *vile*.” Unaona? Linamaanisha Hivyo.

386 Sikilizeni. Hebu niseme jambo hili, upesi sana sasa. Hata yale maono ambayo Mungu anayaonyesha hapa mahali hapa, yanafahamika vibaya sana. Hiyo ndiyo sababu mnanisikia mimi kwenye kanda, nikisema, "Sema vile kanda zinavyosema. Sema vile maono yanavyosema." Sasa, kama mko macho kabisa, mtaona kitu fulani. Mnaona? Natumaini si lazima nikishike mkononi mwangu na kuwaonyesheni. Mnaona? Mnaona? Mnaona? Mnaninii . . . Liko—liko hapa. Tuko wakati wa mwisho. Mnaona? Naam, bwana. Watu werevu wenye elimu wanapitwa na jambo hilo. Yale maono rahisi, wakati yanapofunuliwa katika urahisi wa namna hiyo, mpaka linafunika juu ya vichwa vya watu. Unaona?

387 Kwa sababu niliona ono hilo, nikawaambia yote kuhusu kwenda huko juu kuwinda, na, mwajua, jambo hilo liliwakwaza watu. Na pale Mungu akalituma pale kwa kusudi lilo hilo, kisha akarudi na kulifasiri moja kwa moja, kuonyesha kuaga dunia kwa mama yangu, na mambo kama hayo. Kisha nikarudi na kuwaambia jambo hilo, kabla. Nalo likatukia kulingana kabisa tu na vile Yeye alivyosema litatukia. Mnaona?

388 Na, hata hivyo, Yohana alikuja moja kwa moja kule nje na kukiri. Alisema, "Mimi siye Masihi, lakini mimi ni sauti ya mtu aliaye nyikani."

389 Na halafu wanafunzi wao hao wanasema, "Mbona wananinii, waandishi wanasema Maan- . . . Maandiko yanafundisha ya kwamba Eliya hana budi kuja kwanza?" Unaona? Urahisi wa Mungu huenda, unapita tu moja kwa moja juu ya vichwa vya watu.

390 Hebu nichukue jambo hili, kisha nimalize. Nitamaliza, kwa msaada wa Mungu. Unaona? Angalia. Sasa hebu na tulichambue jambo hili. Halafu, ni—ninasikitika kuendelea kuwaambia ninyi nyote nitaondoka, na halafu . . . Angalieni. Nasikitika kuwachelewesha. Lakini, masaa machache tu, tutarudi.

Angalieni, hebu na tuchukue tone la kawaida la wino.

391 Kila kitu kina kusudi fulani. Mmekusanyika hapa asubuhi hii kwa kusudi fulani. Ninakula kwenu, Charlie; Nellie, ulinipikia, kwa kusudi fulani. Mimi . . . Kila kitu ni kwa kusudi fulani. Kanisa hili limejengwa kwa kusudi fulani. Hakuna kitu kisicho na kusudi na sababu.

392 Hebu na tuchukue tone la kawaida la wino sasa. Mnaweza kunisikia? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hebu na tuchukue tone la kawaida la wino na tuliangalie. Ni kitu gani? Tone la wino. Lilitoka wapi? Vema. Hebu na tulichukue tone hili la wino sasa, ni, na tuseme ni wino mweusi. Sasa, wino huo upo kwa kusudi fulani. Unaweza kuandika msamaha wangu katika gere- . . . kutoka gerezani. Unaweza kuandika msamaha wangu kutoka kwenye jela la mauti. Hiyo ni kweli? Inaweza kuandika Yohana 3:16, na kuokoa nafsi yangu kwa kuamini

Hilo. Sivyo? [“Amina.”] Ama, unaweza kutia sahihi hati yangu ya kuuawa. Mnaona? Unaweza kunihukumu Mahakamani. Una kusudi fulani. Hiyo ni kweli? [“Amina.”]

393 Vema, hebu na tuangalie wino huo mchache tuone mahali ulipotoka. Sasa, ni wino. Umeundwa, na kemikali na vitu mbali mbali, hata ukawa wino. Na ni mweusi. Ukiumwaga kwenye nguo zako, utazitia doa.

394 Lakini tumetengeneza kitu kinachoitwa kitakasaji. Ninyi wanawake mnatumia Kitakasaji cha Kloroksi. Vema, ninachukua tone hilo moja la wino na kulitia kwenye beseni lenye—lenye kitakasaji, sasa ni kitu gani kimetokea kwenye wino huo? Mnaona? Mbona? Kitakasaji kimetengenezwa, kimegunduliwa na ni kemikali zilizotengenezwa kiwandani, pamoja, ambazo zitavunjavunja hiyo rangi sana hata huwezi kuipata. Sasa, sehemu ya kitakasaji hicho ni maji.

395 Maji ni H_2O, ambayo ni haidrojeni na oksijeni. Na haidrojeni na oksijeni, zote mbili, ni baruti hatari. Na, tena, kwa kweli haidrojeni na oksijeni ni majivu. Hivyo ndivyo zilivyo, hiyo ni kweli, majivu ya kemikali, majivu tu ya kemikali. Sasa, sasa weka hizo mbili pamoja, nawe unapata maji. Lakini, zivunjevunje, nawe una haidrojeni na oksijeni, na unaendelea tu kurudi nyuma.

396 Sasa, katika kulipata jambo hili, hebu na tuchukue. . . Nami siwezi. Sasa huenda kukawa na wakemia wanaoketi hapa. Na sasa nataka kusema jambo hilo, maana kuta—kutakuwa na wakemia watakaosikiliza haya, mimi sijui fomula yake. Lakini nataka kuielezea kwa njia yangu mwenyewe ya kinyonge, nikitumaini ya kwamba Mungu atajifunua Mwenyewe katika jambo hilo.

397 Angalia, ninadondosha hilo tone la wino katika ki—ki—kitakasaji. Nini kinatukia? Mara moja doa hilo jeusi limetoweka. Hungeweza kulipata tena hata ukifanya nini, limetoweka. Hautaliona tena. Nini kilitukia? Sasa, huoni cho chote kikitoka kwake. Huoni. Kwa nini huoni? Kwa sababu limevunjwavunjwa.

398 Sasa, sayansi ingesema, “Lilirudi kwenye asidi zake za asili.”

399 Hizo asidi zilitoka wapi? Unaona? Vema, unasema, “Zinatoka—zinatoka kwenye vitu fulani.” Vema. Tuseme, kwa mfano, kama vile, “Moshi ulivyotengeneza asidi.” Moshi ulitoka wapi? “Vema, ulikuwa, tutasema, moshi ulitengenezwa na molekuli nyingi.” Molekuli zilitoka wapi? “Kutoka kwenye atomi.” Atomi zilitoka wapi? “Kutoka katika elektronikia.” Hizo zilitoka wapi? “Mialimwengu.” Unaona, umerudi nyuma kabisa kusikojulikana, kwa wakemia, sasa. Na, kama hicho ni kitu cha asili na ni kiumbe, hakina budi kutoka kwa Muumba.

400 Kwa hiyo, hamketi hapa kwa bahati. Mimi sishikilii mpaka saa sita na nusu, ama saa saba, kwa bahati. “Hatua za mtu

mwenye haki zaimarishwa na Bwana.” Unaona? Kuna sababu yake. Kuna sababu ya wewe kuamini. Kuna sababu ya wewe kutokuamini. Kama tu kwa—kwa ule wino.

401 Sasa hebu na tuvunjevunje jambo hilo. Sasa, jambo la kwanza, tuseme, baada ya sisi kurudi kwenye . . . Tunairudisha nyuma mpaka kwenye molekuli. Sasa, tulichukua molekuli, ningesema, namba 1 mara molekuli 9, mara molekuli 12. Sasa, kama ingalikuwa ni 11, ingelitokea nyekundu. Lakini ili—ilipaswa kuwa 12, ipate kuwa nyeusi.

402 Ndipo tutairudisha hiyo chini hata kwenye atomi. Ilikuwa ni atomi. Na 96 mara +43, ni sawasawa na atomi 1611. Kama zingalikuwa 1612, huenda zingalikuwa ni rangi ya zambarau. Unaona? Ndipo unaendelea kuivunjavunja.

403 Inaonyesha ya kwamba kulikuwako na kitu fulani kule ng’ambo, kwanza. Hiyo ni akili tu ya kawaida. Ni uumbaji. Hakina budi kuwa na Muumbaji. Nayo ilitoka kwenye Muumba, ndipo ikaamriwa na kuwekwa kwenye hizi, mbali mbali. Sasa, sayansi haiwezi kuchomoa atomi B16 mara 12, mara 14, mara cho chote kile, nje namna hiyo, kufanya jambo hilo. Ilibidi Mungu kufanya jambo hilo.

404 Na ndipo inaletwa mpaka mahali ambapo linafikia kwenye atomi, ndipo sayansi inaweza kuanza kuigusa. Ndipo inatokea kwenye molekuli, ndipo wanaweza kuanza kuiona vizuri zaidi. Ndipo inashuka, kutoka hapo, inakuwa kitu kingine. Ndipo, jambo la kwanza, inakuwa kemikali, kisha wanazichanganya hizi pamoja.

405 Sasa, wakati mwanadamu, kabla hajatenda dhambi. Ninafunga, lakini msilikose jambo hili. Wakati mwanadamu alipotenda dhambi, yeye alijitenganisha na Mungu, na kuvuka lile shimo kubwa, na kujitia katika mauti upande huu. Akaondoka. Hakuna njia ya kurudi. Kweli kabisa. Hakuna njia kwake kurudi. Lakini basi wakati alipofanya jambo hilo, Mungu alikubali kibadala, ambacho kilikuwa ni mwana-kondoo, ama mbuzi, ama kondoo, ama kitu fulani, kwa ajili ya damu; ambayo Adamu alinena habari zake, ama—ama Habili alinena habari zake, upande ule mwingine wa lile shimo.

406 Upande ule mwingine, yeye ni mwana wa Mungu. Yeye ni uzao uliotoka kwa Mungu. Yeye ni urithi wa dunia. Anaweza kutawala maumbile. Anaweza kunena na ikawa. Ni kwa nini, yeye ni muumba, yeye mwenyewe. Yeye ni uzao wa Mungu.

407 Lakini, wakati alipovuka, yeye alitenganisha uwana wake. Yeye ni mwenye dhambi, kwa maumbile. Yeye yuko chini ya mikono na utawala wa Shetani.

408 Naye Mungu alichukua dhabihu, kemikali, ya damu, lakini damu ya mafahali na mbuzi haikutaliki dhambi. Iliifunika tu dhambi. Kama nina doa jekundu mkononi mwangu, na

nilifunike kwa rangi nyeupe, lile doa jekundu bado lingalipo pale. Unaona, lingalipo pale.

409 Lakini Mungu alituma, kutoka Mbinguni, kitakasaji cha dhambi. Ilikuwa ni Damu ya Mwanawe. Ili kwamba, wakati dhambi yetu iliyoungamwa inapodondoshwa kwenye kitakasaji cha Mungu, jaribu kuipata tena! Ile rangi ya dhambi inarudi kupitia kwa wapatanishi, na kupitia katika wakati, mpaka kumfikia yule mshtaki, Shetani, na kukaa juu yake hata Siku ya Hukumu.

410 Ni kitu gani kinachompata mwana? Anakuwa katika ushirika mkamilifu na Baba tena, akiwa amesimama upande ule mwingine wa shimo, akiwa hana kumbukumbu la dhambi dhidi yake. Hana tena, hakuna tena doa la kitakasaji linaloweza kuonekana mahali po pote. Yeye yuko huru. Haleluya! Kama tu ile Kloroksi, ama ule wino usivyoweza kamwe kuwa wino tena, kwa sababu umevunjwavunjwa na kurudishwa tena. Na hapo wakati dhambi iliyotubiwa imetubiwa na imewekwa kwenye . . . Mwanamume ama mwanamke ambaye ametumbukizwa katika Damu ya Bwana Yesu Kristo, inaua dalili zote. Na kila molekuli ya dhambi inamrudia Ibilisi, na kuwekwa juu yake hata kwenye ile Siku ya Hukumu, ambapo kikomo chake cha Milele atatupwa kwenye Ziwa la Moto. Na lile shimo limewekwa daraja, wala halitakumbukwa tena. Na mtu anasimama amehesabiwa haki, kama mwana wa Mungu. Urahisi!

411 Musa, chini ya damu ya mafahali na mbuzi, na kukiri kwake Neno la Mungu! Naye Mungu angeweza kumchukua mtu huyo wa kawaida, na kuweka Maneno Yake katika kinywa chake. Naye alithibitisha ya kwamba alikuwa mtumishi wa Yehova, kwa kuwa angeweza kutembea huko nje na Yehova akanena naye kwa ono. Akatoka nje, akainyosha mikono yake kuelekea mashariki.

412 Na sasa, kumbukeni, Mungu alinena naye. Ni wazo la Mungu. Mungu humtumia mwanadamu. Mungu alinena naye. Ni kweli. Yeye alisema, “Nenda kanyoshe ile fimbo, iliyo mkononi mwako, kuelekea mashariki, na useme, ‘Nzi!’”

413 Musa, chini ya damu ya mbuzi huyo, kondoo, alitoka huko nje na akachukua fimbo ile, akaielekeza mashariki. “BWANA ASEMA HIVI. Na kuwe na inzi!” Hakusikia inzi. Akarudi. Limenenwa tayari. Ni wazo, sasa limenenwa, limetamkwa. Sasa ni Neno la Mungu. Linaingia kwenye mdomo wa mwanadamu, mtu wa kawaida chini ya damu ya ndama, fahali, fahali ama mbuzi.

414 Muda si muda wajua, inzi wa kijani akaanza kuruka-ruka. Muda si muda unajua, walikuwa ratili tano kwa yadi. Ilikuwa ni nini? Ilikuwa ni Neno la Mungu, lililonenwa kupitia kwa Musa, yule Muumba. Kwa sababu, chini ya damu, yeye

alikuwa akisimama katika Uwepo wa Mungu, na Maneno yake mwenyewe hayakuwa ni neno lake.

415 "Mkikaa ndani Yangu, na Maneno Yangu yakae ndani yenu, basi ombeni mtakalo, nanyi mtapewa." Kanisa linasimama wapi?

416 "Na kuwe na vyura!" Na hakukuweko na chura hata mmoja nchini. Katika muda wa saa moja, walikuwa wenye kina cha futi kumi, katika sehemu nyingine. Ilikuwa ni nini? Ilikuwa ni Mungu, yule Muumba, akijificha katika mtu wa kawaida.

417 Sasa nataka kuwauliza jambo fulani. Kama damu ya ndama ama ya mbuzi ikitumiwa kama kitakasaji, ambayo inaweza tu kufunika, ingemweka mtu katika mahali ambapo angenena Neno la kuumba la Mungu na kuwafanya inzi waweko, ungewezaje kukwazika kwenye kitakasaji cha Damu ya Yesu Ambaye angenena kindi ama kitu fulani kiweko?

418 Usifanye hivyo, usikwazike juu ya urahisi. Amina ya kwamba Yeye angali ni Mungu. Loo, jamani! Msamaha wa dhambi! Loo, jinsi ninavyotamani ningaliweza . . .

419 Halafu, katika Marko 11:22, "Kama ukiuambia mlima huu, 'Ng'oka,' wala usione shaka moyoni mwako, ila uamini ya kwamba hayo usemayo yatatukia, loo, yatakuwa yako."

420 Jamani, nina kurasa tatu ama nne. Hatuna budi kuyaachilia. Asanteni.

421 Mungu akijificha katika urahisi. Hamwoni? Kuna jambo fulani kasoro mahali fulani. Kuna jambo fulani kasoro mahali fulani. Wakati Mungu anapotoa tamshi, Yeye hawezi kusema uongo. Yeye alitoa ahadi. Unaona? Yeye hujificha katika urahisi. Ni rahisi sana!

422 Wenye elimu na wanachuoni wanasema, "A-ha, ni . . . Loo, ni kushirikishana mawazo ama cho chote kile. Mwajua, ni . . . "

423 Mungu anaweza kujirudisha kupitia katika mitiririko ya wakati, na kukwambia bila kukosea kule nyuma yale yaliyotukia hasa, akwambie vile ulivyo hasa leo, na kile utakachokuwa baadaye. Hiyo ingali ni kwa kitakasaji cha Yesu Kristo, Ambaye anaweza kumchukua mwenye dhambi na kumsafisha aingie Pale, na anasimama Mbele za Mungu.

424 "Na mkikaa ndani Yangu, na Maneno Yangu yakae ndani yenu; mnaweza kuomba mtakayo, nayo yatatendeka. Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo yeye naye atazifanya."

425 "Unanihukumuje Mimi? Loo, je! sheria zenu wenyewe hazikusema ya kwamba wale waliojiliwa na Neno la Mungu, hao manabii, je! mliwaita 'miungu'? Na basi mnaweza kunihukumu vipi ninaposema Mimi ni Mwana wa Mungu?" Wanakosa kuliona. Wanakosa kuliona.

426 Sasa, enyi Kanisa, katika Jumbe zinazokuja, tangu usiku wa leo na kuendelea, msikose kuliona. Unaona? Kuona siku tunayoishi. Na, kumbukeni, Damu ya Yesu Kristo inaondolea dhambi mbali sana na wewe, wakati hata hazikumbukwi na Mungu, tena. Inaondoa mawaa yote.

> Dhambi ilikuwa imeacha doa jekundu sana,
> Akaiosha ikawa nyeupe kama theluji.
> Basi mbele ya Kiti cha Enzi,
> Ninasimama mkamilifu ndani Yake.

427 Loo, jamani, ninawezaje kuwa mkamilifu? Ninawezaje kuwa mkamilifu? Kwa sababu ile Damu; si mimi, lakini ile Damu inasimama kati yangu na Mungu. Niliikubali. Naye aliiweka . . . mimi ni mwenye dhambi, lakini Yeye ni Mungu. Lakini ile kemikali inasimama kati yangu, kile kiua dhambi, kwa hiyo Mungu huniona mimi nikiwa tu mweupe kama—kama maji yaliyomo—yaliyomo kwenye kile kitakasaji. Dhambi yangu imeondoka. Haiwezi hata kumfikia Yeye, kwa sababu kuna Dhabihu ikaayo pale.

428 Imani yetu iko wapi ya kuliamini Neno rahisi la Mungu? Yale Mungu aliyosema tu, mchukue kwenye Neno Lake. Mungu hujificha hivi sasa katika urahisi, katika kundi dogo nyenyekevu, lakini moja ya siku hizi atajidhihirisha Mwenyewe kama vile alivyofanya sikuzote katika siku zilizopita. Mnampenda? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

> Ninampenda, ninampenda
> Kwani alinipenda kwanza
> Na kununua wokovu wangu
> Mtini Kalvari.

429 Mnampenda? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Jamani, je! Yeye si ni wa ajabu? ["Amina."] Ninatumaini na kuamini ya kwamba Ujumbe huu utatoa Kile ulichokusudiwa kutoa, ya kwamba utakufikisha mahali ambapo huangalii mambo yanayovutia kwa uzuri. Ama ninii . . . Unapomwona Mungu katika ukuu, wewe uangalie jinsi jambo hilo lilivyo rahisi, na ndipo utamwona Mungu. Usimtafute Yeye . . .

430 Wakati Eliya aliporudi kule kwenye lile pango, moshi ulitoka, damu, ngurumo, umeme; na, unaona, aina zote hizi za misisimko tuliyokuwa nayo, damu usoni na mikononi, na miamsho na kadhalika. Haikumhangaisha nabii huyo. Yeye alikaa tu pale mpaka alipoisikia ile Sauti ndogo tulivu, (ilikuwa ni nini?) Neno, ndipo akaufunika uso wake akatoka. Unaona, hilo lenyewe lilikuwa Ndilo.

431 Kumbuka, ewe rafiki, usitafute ninii kubwa mno, kubwa . . . Unasema, "Mungu, Yeye hunena juu ya mambo makubwa, makubwa mno. Utakuja wakati kutakapokuwa na *hiki, kile* ama kile *kingine*, mambo makubwa mno." Ninatumaini mnashika ninalozungumzia. Mnaona? "Mambo makubwa, makubwa mno,

unaona! Na, loo, wakati hili litakapotukia, litakuwa jambo kubwa, kubwa namna *hii*."

432 Nalo litakuwa ni rahisi sana, utapitwa na jambo zima, na unaendelea moja kwa moja tu. Unaona? Nawe utaangalia nyuma na kusema, "Vema, jambo hilo halikutukia kamwe . . . " Unaona, limepita moja kwa moja juu, na hata hukuliona. Lilipita tu. Unaona, ni rahisi sana. Unaona? Mungu anaishi katika urahisi, unaona, ili ajidhihirishe Mwenyewe katika ukuu. Ni kitu gani kinachomfanya kuwa mkuu? Kwa sababu anaweza kujifanya rahisi.

433 Mtu mkubwa, mkubwa mno hawezi kujifanya rahisi; hana budi kuwa mtu mashuhuri fulani. Unaona? Lakini yeye bado si mkubwa vya kutosha. Atakapokuwa mkubwa vya kutosha, basi anashuka namna *hii*, unaona, anaweza kujinyenyekeza.

434 Kama yule mtakatifu wa kale alivyosema kule Chicago, "Jamaa huyo alipanda akaenda kule, akiwa na elimu tele na kadhalika." Kasema, "Akashuka, ameaibika, kichwa kimeinamia chini. Akatoka nje, ameshindwa." Mtu fulani akasema, "Kama angalipanda vile alivyoshuka, angalishuka vile alivyopanda." Vema, hiyo ni kweli. Unaona?

435 Jinyenyekeze. Jinyenyekeze tu. Usijaribu kuwa mtu wa ajabu-ajabu. Wewe m—mpende Yesu tu. Unaona? Sema, "Bwana, kama kuna hila yo yote moyoni mwangu, kama kuna ubaya wo wote, Baba, sitaki kuwa namna hiyo. Uondoe. Sitaki kuwa namna hiyo. Loo, ninataka kuhesabiwa kama mmoja wao, katika Siku hiyo, Bwana. Nami ninaona siku hiyo ikikaribia."

436 Mtaona Mihuri hii ikianza, kama Mungu ataifunua kwetu. Kumbuka, Yeye pekee ndiye anayeweza kufanya hivyo. Tunamtegemea Yeye. Mungu awabariki.

437 Na sasa nadhani mchungaji wetu atasema nanyi, atawaongeleza; ama apate kusema, hasa, na—nanyi, kabla hatujakutana tena mchana wa leo. Nami nafikiri ibada itaninii . . . Ibada ya nyimbo saa kumi na mbili na nusu, mchungaji? Na ni . . . [Ndugu Neville anasema, "Tuanzie saa kumi na mbili na nusu."—Mh.] Saa kumi na mbili na nusu. Na ni . . . ["Milango inafunguliwa saa kumi na mbili."—Mh.] Milango inafunguliwa saa kumi na mbili. Ibada ya nyimbo itaanza saa kumi na mbili na nusu.

438 Na Bwana akipenda, nitakuwa nikihubiri, usiku wa leo, juu ya somo la kile Kitabu Kilichotiwa Mihuri Saba. Na halafu, Jumatatu usiku, yule mpanda farasi mweupe. Jumanne usiku . . . Mpanda farasi mweusi, Jumatano usiku. Farasi wa kijivu, farasi mwenye rangi ya kijivujivu. Na yule mpanda farasi mwekundu. Na halafu tutaenda kwenye ule wa sita . . . wa nne, wa tano na wa sita, na halafu Jumapili usiku. Jumapili ijayo asubuhi, huenda ikawa ni ibada ya uponyaji. Sijui.

439 Sasa kumbukeni, tumejiweka wakfu kwa Bwana, sisi wenyewe pamoja na kanisa, kwa ajili ya utumishi wa Bwana. Mungu awabariki.

440 Ni—nimechelewa saa nzima. Mtanisamehe? [Kusanyiko, "Amina."—Mh.] Si—sininii, unaona, sitaki kufanya jambo hilo. Lakini, unaona, ni—nitakuwa pamoja nanyi juma hili tu, kisha nitaondoka tena. Nami sijui nitakakokwenda; mahali po pote tu aniongozako. Nami ninataka kuchangia kila dakika niwezayo, kwa sababu ninataka kuishi Milele pamoja nanyi.

Mungu awabariki. Sasa, Ndugu Neville.

Ufunuo Wa Mihuri Saba

(The Revelation Of The Seven Seals)

Jumbe hizi za Ndugu William Marrion Branham zilihubiriwa kutoka tarehe 17 Marchi mpaka tarehe 24 Marchi, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, na Muhuri wa Saba ukaendelea tarehe 25 Marchi katika Hoteli ya Sherwood. Baada ya kupata kanda za awali ambazo zinasikika vizuri na ni kamilifu zaidi, kitabu hiki kimechapishwa tena kwa mpangilio wa sasa. Kila jitihada imefanywa kuhamisha kwa usahihi Ujumbe wa sauti kutoka kwenye kanda za sumaku zilizorekodiwa na kuuandika katika kitabu, na umechapishwa hapa bila kufupishwa na kusambazwa na Voice of God Recordings.

Haki zote zimewekwa. Kitabu hiki hakiwezi kuuzwa, kuchapishwa tena, ama kufasiriwa katika lugha zingine, ama kutumiwa kwa kuchangisha fedha bila barua ya kuruhusia ya William Branham Evangelistic Association. Kilichapishwa tena katika mwaka wa 2006.

SWAHILI

©2001 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings

P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.

www.branham.org